# FASIHI SIMULIZI

Expanded Features

**SEHEMU YA KWANZA**

# MHADHARA WA KWANZA

## MAANA YA FASIHI SIMULIZI

**MADHUMUNI**

Baada ya somo hili
Utaweza kueleza
(1) Maana ya Fasihi Simulizi
(2) Matumizi ya Fasihi Simulizi katika jamii
(3) Nafasi ya Fasihi Simulizi katika jamii

Njia muafaka ya kutangulizia somo hili ni kujiuliza:-

**Maana ya Fasihi Simulizi ni nini?**

Bila shaka tutakubaliana kwamba kuna fasiri nyingi za dhana ya Fasihi simulizi kama kulivyo na wahakiki na watafiti wengi katika taaluma hii:

Kirumbi (1975) atueleza kuwa;

> Fasihi simulizi ni masimulizi tunayopokea mdomo kwa mdomo. Katika Fasihi hii kuna utumiaji wa ulumbi ufundi wa kusema (uk 15)

Msimamo wa Kirumbi ni kwamba chombo cha kutongolea Fasihi Simulizi ni mdomo na kwa hivyo, katika Fasihi Simulizi tuna Masimulizi. Wataalamu wengine wameendeleza mawazo kuwa Fasihi Simulizi ni ya kale na ambayo hurithishwa kizazi kimoja hadi kingine. Kwa watu wengine, Fasihi Simulizi ikitajwa wanaichukua kama sanaa ambayo inashughulikia mambo ya kale. Kwa jina la kashifa fasihi hii huitwa Fasihi ya mapokeo. Mbali na ufafanuzi wa maana ya Fasihi simulizi, isitilahi yenyewe imekumbwa na migogoro. Baadhi ya wataalamu wametumia istilahi ya Fasihi zungumzwa kwa maana ya simulizi Fasihi. Kezilahabi (1989) anasema:

Complete Documents
Expanded Features

> Fasihi simulizi ni istilahi inayotumiwa kuelezea dhana ya Fasihi itolewayo kwa mdomo bila kuandikwa. Istilahi hii ina dosari kwani neno simulizi haina maana kitu kinachonenwa (oral) bali ina maana ya kitu kinachosimuliwa (narrative). Hivyo tafsiri ya simulizi katika kiingereza ni narrative literature siyo oral literature.

Pamoja na mgogoro huu kuhusu istilahi ya Fasihi Simulizi, kilicho muhimu kwetu ni kuelewa kwamba Fasihi Simulizi ni aina moja ya Fasihi. Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia mazungumzo na matendo katika kuwasilisha ujumbe fulani kwa watazamaji au wasikilizaji. Mazungumzo hayo yaweza kuwa yaimbwa, kutendwa au kuzungumzwa. Aina hii ya Fasihi Simulizi imepokelewa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo. Lakini pia, inaweza kuwasilishwa papo hapo.

Msimulizi katika fasihi simulizi mbali na kutumia mdomo wake hutumia viungo vyake vingine vya mwili kama mikono, miguu, au ishara mbali mbali katika uso wake hata kupandisha na kushusha sauti yake. Kwa jumla aweza kutumia mwili wake mzima katika kuwasilisha na kufanikisha ujumbe wake kwa hadhira yake ambayo huwa ana kwa ana nayo. Isitoshe anafaulu katika kutoa picha halisi ya dhana anayoitaka kuwasilisha kama ni ya huzuni, furaha, kuchekesha, na kadhalika. Msimulizi, katika kufanikisha usimuliaji wake, anaweza kujitathmini na kujua kama amefaulu au la, yaani huwa na fursa ya kuona kama hadhira yake inamsikiliza au la. Ikiwa haimsikilizi, msanii au fanani huwa na fursa ya kubadilisha kunga zake wakati huo huo anaposimulia ili aweze kuwavuta au kuwatega na kuwanasa wasikilizaji wake au watazamaji wake. Hapo ndipo hadhira hupata nafasi ya kubainisha wasanii wazuri waliokomaa na wasanii chipukizi.

Zaidi ya kusimulia, kuumba au kuigiza msanii wa Fasihi Simulizi huwa na nafasi ya kushirikisha hadhira yake kama wahusika katika sanaa yake. Aweza kutimiza hayo kwa kufanya mshiriki mmoja kuigiza matendo mbali mbali. Ufundi

Complete Documents
Expanded Features

wa aina hii huhitaji umahiri wa hali ya juu. Hali hii humpa msanii wahakiki wake papo hapo.

Kwa upande mwingine, hadhira nayo huwa na nafasi na uhuru wa kushiriki au kuuliza maswali pale ambapo haikuelewa. Vile vile wanapata fursa ya kuonyesha hisi zao, kuhimiza, kukumbushana na kwa hali hiyo, Fasihi Simulizi huwa na uwezo wa kufundisha zaidi.

Baada ya maelezo hayo, basi tunaweza kuafiki maoni ya Kirumbi (1976) kwamba fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia mazungumzo na matendo katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa watazamaji au wasikilizaji. Mazungumzo hayo huwa katika mfumo wa masimulizi kwa kuimbwa, kutambwa kughaniwa au kutongolewa. Fasihi simulizi hueleza jamii kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa. Fasihi hii huzungumzia juu ya yale ambayo huzunguka jamii husika. Fasihi simulizi huathiri malezi ya watu kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo au matendo. Fasihi simulizi huundwa sambamba na mabadiliko ya jamii na kwa hivyo nayo hubadilika kimaudhui na kifani kufuatia mabadiliko ya mifumo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Fasihi Simulizi basi twaweza kusema ni aina ya sanaa ilio hai na ambayo hukua na kubadilika kutokana na mabadiliko ya wakati na ya mifumo ya jamii.

**Vipengele muhimu vya Fasihi Simulizi.**

(a) Msimulizi (fanani)

Huyu huwa ni mtu ambaye anaitamba hadithi, kuimba wimbo au kutoa kitendawili au methali.

(b) Wasikilizaji au watazamaji (hadhira)

Hawa huwa ni washiriki katika kutazama au kusikiliza fani za fasihi simulizi na mara nyingine huwa wanatumiwa na fanani kama wahusika wa fani yake.

(c) Pahali

hapa ni jukwaa au pahali ambapo tukio la Fasihi simulizi litatendeka. Pahali hapa paweza kuwa nyumbani, uwanjani, kuzunguka moto baharini na kadhalika.

Complete Documents
Expanded Features

(d) Tukio

hili huwa tendo linalotendeka katika jukwaa ya Fasihi Simulizi. Tendo hilo laweza kuwa ni usimuliaji wa hadithi, kutega vitendawili, kuimba nyimbo/wimbo au kutoa methali.

Katika Fasihi Simulizi kuna falsafa na mantiki ambayo haistahiki kusahaulika wala kudharauliwa. Kwa mujibu wa maoni ya Kiango na Sengo (1977).

Fasihi huweza kulinganishwa na mwavuli unaokinga amali za maisha ya watu. Amali hizi hujengwa na binadamu ili kujenga msingi mzuri, hifadhi njema na maendeleo mema ya hadhi na taadhima yake. Amali hizo ndizo zijengazo fasihi. Fasihi huzihifadhi amali hizo na kuzifichua kwa kuonyesha watu ubora na uovu wa kila kipengele cha maisha.

| |
|---|
| Eleza maana ya fasihi simulizi. Fafanua baadhi ya vipengele vyake. |

Maelezo haya yajumuisha umuhimu wa Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Hapo ndipo tunajiuliza umuhimu au matumizi ya Fasihi Simulizi ni yapi katika jamii.

Kwanza ingefaa kudokeza kwamba Fasihi Simulizi ni chombo cha kuwaunganisha watu. Mara nyingi, Fasihi Simulizi huhitaji ushirika katika utendaji wake. Fasihi hii ni muhimu kwa vile watu wengi hata sasa katika jamii nyingi hawajui kusoma na kuandika. Wanajamii hawa hawana njia nyingine ya kutoa hisi zao za ndani isipokuwa kwa kutumia chombo hiki cha sanaa. Zaidi ya hayo hata katika nchi ambazo asilimia kubwa ya watu wamesoma, Fasihi Simulizi hutumiwa sana katika shughuli kadha za utamaduni kama sherehe za arusi, matanga, na siasa. Pamoja na hayo, Fasihi Simulizi hutumiwa katika shughuli za uzalishaji mali.

Isitoshe Fasihi Simulizi huwa na ufundi wa uzuri wa pekee ambao humganda na kumnata mtu ambao haupatikani katika Fasihi andishi. Pia, vitabu,

Complete Documents
Expanded Features

magazeti na majarida ambayo hutumiwa kutangaza biashara si vyombo ambavyo vinafikiria umma katika makao yao mashambani au vijijini. Nchi nyingi pia zimegundua umuhimu wa kutumia Fasihi simulizi katika harakati za kuleta maendeleo. Kwa mfano, katika kusambaza ujumbe kuhusu upangaji wa uzazi au kujihadhari na ugonjwa wa ukimwi, serikali ya Kenya imetumia makundi ya waigizaji kama wale walioigiza mchezo wa usiniharakishe ama Tushauriane . Pia kipindi cha vitimbi kumetumiwa kwasilisha ujumbe kwa umma.

Fasihi simulizi hudai ukale na pia inadai haki ya kujiri na kuendelea kujiri katika jamii zote. Fasihi simulizi huibuka na kuoana na utamaduni wa jamii husika na uhusiano wa watu pamoja na jumlisho la amali zao.

Katika amali zetu za kale kabla ya jamii kukumbwa na mifumo ya kibepari ambayo ilizaa matabaka katika jamii, kulikuwa na msisitizo wa ari na juhudi za kazi pamoja na uendelezaji wa sehemu kadha za utamaduni kama vile mambo ya ndoa, uzazi, malezi, marika, mafunzo mbali mbali ya mazingira na shughuli nyingine kama jando, sherehe maalum na pia amali zinazohusiana na imani katika miungu, mashetani na mizimu. Kwa wakati wote huo, Fasihi simulizi imekuwa chombo cha kuhifadhi, kulinda, kutunza na kuendeleza amali hizo ambazo zilikuwa msingi wa maisha ya wanajamii.

Amali hizi ni tamaduni, mila desturi, dini, siasa, uchumi na kadhalika. Amali hizi sharti zihifadhiwe katika uasili wake. Kujenga na kuhifadhi lilikuwa jukumu la taaluma ya Fasihi Simulizi. Dhima nyingine ya Fasihi simulizi ilikuwa ni kutafuta ukweli kwa kuvihakiki na kuchambua vipengele vyote vya maisha. Kutokana na dhima hiyo, fasihi simulizi iliweza kutumika kama chombo cha uhusiano bora na chombo chenye nguvu na misingi imara. Jamii haiwezi kukua na kuendelea bila fasihi, fasihi simulizi ikiwemo. Fasihi simulizi katika jamii hutumika kama chombo ambacho humchora na kumwonyesha mwanajamii vile alivyo na uwezo wa kushirikiana na wenzake pamoja na kushirikisha elimu na ujuzi alionao kwa manufaa ya jamii. Fasihi simulizi ilitumiwa kama chombo cha

Complete Documents
Expanded Features

kurekebisha na kuunda upya hadhi na utu wa wanajamii katika nyanja mbali mbali za maisha yao. Kutokana na hadhi hiyo twaweza kudokeza kwamba Fasihi simulizi ni sanaa madhubuti inayokua na kukomaa kufuatana na mabadiliko ya wakati, jamii na mazingira. Hekima na mantiki ipatikanayo katika tanzu mbali mbali za Fasihi Simulizi ni amali kubwa kwa mwanajamii aliyetalamikia kuweza kuitumia kwa kutatua matatizo mbali mbali kama vile ya ndoa, ujinga, maradhi, uchumi, siasa, na umaskini. Fasihi simulizi hutumika kama ghala ya rasilimali na amali za Uafrika na hivi leo yatumika kama chemichemi ya Fasihi Andishi, kama Sengo (1973: 77) anavyotuelezea.

Fasihi simulizi hutumika kama mtumishi wa maisha ya watu/wanajamii. Inatumika kama chombo cha pekee cha kujenga umoja katika jamii husika.
Kwa mujibu wa maoni ya Plekhanov (1957) Fasihi (fasihi simulizi ikiwemo) ni chombo mojawapo katika harakati dhidi ya mazingira. Mtazamo huu unashikilia kwamba sanaa haina budi kutumiwa kumsukasuka na kumzindua mwanajamii ili apambane na mazingira machafu. Ili Fasihi simulizi iwe na manufaa katika jamii, ni lazima iwe na jukumu la kuieleza jamii, kuichambua, kuikosoa na kuiongoza katika lengo lake la kupindua unyonge na uchafu uliosakini katika jamii.

Mbali na hayo, Fasihi simulizi hutumiwa kama chombo cha kutoa pongezi kwa watu binafsi ambao wametoa mchango wa kuiendeleza jamii. Kwa wembe huo huo, inatumiwa kushtumu wanajamii ambao nia yao ni kuipotosha jamii. Fasihi simulizi kwa karne nyingi katika janibu mbali mbali za ulimwengu, imetumika kama chombo cha wanyonge ambao ndio wengi katika jamii za kilimwengu. Fasihi hii hutumiwa kutoa hisi za wale ambao hawawezi kujieleza kwa njia ya maandishi. Kwa vile umma wa watu walio wengi hawajui kusoma na kuandika, wanajamii hawa hawana njia nyingine ya kutoa hisi za mawazo yao isipokuwa kwa kutumia chombo hiki cha sanaa.

**MAREJEO**

Hamad A. K. (1982) Fasihi simulizi ni nini? Misingi ya Nadharia ya Fasihi. Taasisi ya Kiswahili na Lugha Za Kigeni. Zanzibar

Complete Documents
Expanded Features

Kirumbi P. S (1975) Misingi ya Fasihi Simulizi. Nairobi: Shungwaya publishers Ltd.

Matteru M.L.B. (1983) Fasihi : Makala ya Semina ya Waandishi wa Kiswahili, Dar es Salaam: TUKI.

Mponda M.S.S. (1975) Fasihi Simulizi. Mulika Namba 7 Jarida la TUKI. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi M. M. (1989) Tanzu za Fasihi Simulizi. Mulika Namba 21. Jarida la TUKI. Dar es Salaam: TUKI.

Nkwera F. M. W. (1978) Sarufi na Fasihi. Sekondari na vyuo. Dar es Salaam: T. P. H.

Plekhanov , G. U. (1957) Art and social life. Moscow: Progress publishers.

Sengo, T.S.Y. na Kiango, S.D. (1977) Hisi zetu. Dar es Salaam: TUKI.

## MHADHARA WA PILI

## FASIHI SIMULIZI NA UANDISHI

### MADHUMUNI

Baada ya somo hili utaweza kueleza

(a) Tofauti kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi

(b) Uhusiano kati ya Fasihi hizi mbili

### UTANGULIZI

Tangu Fasihi Andishi itawale huko Ulaya na Asia kuwa ndiyo Fasihi , kwa kuwa ndiyo iliyotambuliwa na wenye nguvu za kisiasa na kiuchumi, Fasihi Simulizi ilidharauliwa, ikateswa, ikadunishwa na kurushwa wakati Fasihi Andishi ilitukuzwa na kuendelezwa.

Complete Documents Expanded Features

Nia yetu katika kushughulikia Fasihi Simulizi kitaalamu ni kuondoa na kuzika fikira duni ambazo tumezirithi kutokana na wataalamu wa kigeni kuwa sanaa ya Fasihi Simulizi ni ya kishenzi. Kinyume na kasumba ya aina hii, ni dhahiri kuwa makuzi na mabadiliko yake yameithibitisha kuwa nyenzo bora sana ya mawasiliano. Ufundishaji wa jamii zetu leo na kesho utategemea utumiaji wa sanaa hii kama ghala ya amali zetu.

Kutokana na utafiti unaoendelezwa, imetambulika kwamba tenzi za Kigiriki zinazosifiwa sana ambazo zaidiwa kuwa zilitungwa na manju kipofu kwa jina Homer, hazikuwa zimeandikwa bali kwa miaka kama mia tano zilikuwa katika umbo la masimulizi kabla ya kuhifadhiwa kimaandishi. Hali hii yatuonyesha kuwa kigezo cha ubora wa tungo za tenzi kwa mizani ya uandishi katika Ulaya hakina mashiko.

Vile vile, ni majuzi tu ambapo wanateknolojia wameanza kukubali kuwa sehemu kubwa ya Bibilia ni Fasihi Simulizi ya Wayahudi. Vile vile imedhihirika kutokana na utafiti kuwa fasihi hiyo haikutoka mbinguni bali ina mizizi yake katika jamii ya Wasumeri (Mesopotamia), Waajemi na Wagiriki. Msimamo huu umefikiwa kutokana na utafiti wa wataalamu mbali mbali katika Fasihi Simulizi ya jamii mbali mbali huko Ulaya kusini na Asia. Utafiti katika tanzu mbali mbali za Fasihi Simulizi umethibitisha kwamba karibu tanzu zote za Fasihi Andishi zina mizizi yake katika Fasihi Simulizi. Mulokozi (1983:19) anatueleza kuwa karibu kila utanzu wa Fasihi Andishi una mshabana wake katika Fasihi Simulizi.

| **FANI ZA FASIHI SIMULIZI** | **FANI ZA FASIHI ANDISHI** |
| --- | --- |
| Wimbo | wimbo |
| Ushairi | ushairi |
| Utenzi | utenzi |
| Ngano | ngano |
| Kisa | hadithi fupi |
| Utenzi | riwaya |
| Hadithi | riwaya |

PDF Complete
Expanded Features
Unlimited Pages

| | |
|---|---|
| Visaasili | riwaya ya kihistoria |
| Visakale | riwaya ya kihistoria<br>(pia riwaya ya kiwasifu) |
| kitendawili | tambo hasa katika ushairi<br>(mfumbo) |

Kimaudhui tunaona pia kuna ukuruba mkubwa kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Dhamira nyingi ambazo ndizo kiini cha maandishi mengi katika Fasihi Andishi ya kisasa zilikwishajadiliwa katika Fasihi Simulizi. Mifano ya dhamira hizi ni mapenzi, siasa, uhusiano wa watu wa jamii, harakati za kitabaka uhuru, ukombozi, usawa, unyonge wa mwanamke, uchawi, uzazi, ndoa na unyumba na migogoro ya kitabaka. Fasihi Andishi haijafumbua dhamira mpya kabisa ila inaongezea maudhui mapya katika dhamira hizo za kale (Mulokozi 1983 : 20 – 21).

Misemo mingi ya Fasihi Simulizi hasa methali haijapitwa na misemo ya Fasihi Andishi katika usanii wake. upeo wa kisanaa uliofikiwa katika sanaa ya Fasihi Simulizi haujakiukwa mpaka leo. Hali hii inatuangazia kuwa njia za uumbaji wa Fasihi Simulizi ambazo ni pamoja na ushirikishaji wa watu wengi na kwa kipindi kirefu ni bora zaidi kuliko njia zinazotumiwa katika uumbaji wa Fasihi Andishi. Hii huwezekana kwa vile mtunzi mwanzilishi wa utungo fulani ni fanani mmoja binafsi. Baadaye utunzi wake huwa ni mali ya jamii nzima na kila mwanajamii huwa na uhuru wa kutumia kipawa chake kuongezea usanii wake katika utungo huo. Kutokana na juhudi hizo, jamii hupata kitu kilicho bora na kamili zaidi kwa sababu ya kushirikisha akili, ujuzi na ufundi wa watu wengi kwa miaka mingi.

Kwa upande wa Fasihi Andishi, utunzi huwa ni kazi ya mtu binafsi na pengine watu wachache ambao mwandishi huamua kuwashirikisha katika utunzi wake. Fasihi Andishi haipati fursa ya kushirikisha umma moja kwa moja katika uumbaji wake na ikiisha andikwa mara nyingi huwa haibadilishwi tena.

Complete Documents
Expanded Features

Eleza tofauti kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi?

Kimsingi, Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi ni kitu kimoja ila tofauti baina yake ni zile njia tu zinazotumiwa na fanani za Fasihi hizo kuwasiliana na hadhira. Fanani wa Fasihi Simulizi hutumia mdomo, sauti, vitendo muziki n.k. kuwasiliana na hadhira yake wakati fanani wa Fasihi Andishi hutumia karatasi na wino.

Kuna uwezekano wa kutumia ala za Fasihi Simulizi kuwasilisha Fasihi Andishi. Kwa mfano, tenzi nyingi na mashairi ya Kiswahili yaliyoandikwa huimbwa hadharani. Vile vile Fasihi Simulizi yaweza kusambazwa kwa njia ya maandishi isipokuwa ikiandikwa huwa inapoteza ladha yake ya kimasimulizi. Kile tunataka kusisitiza ni kwamba hati za maandishi si ukuta ambao hutenganisha kabisa Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.

Michezo mingine tunayosikia na kutazama katika televisheni ambayo huvutia umma sana mara nyingi huwa ni Fasihi Simulizi ambayo haikuandikwa. Kwa mfano, kikundi ambacho chajulikana kama street comedian katika mji wa Nairobi huwa na wanaume ambao wanaigiza kama wahusika wanawake. Kikundi hiki bila shaka huwa hawatayarishi michezo yao na kuandika bali huigiza tu kulingana na hadhira yao na ujumbe ambao wanataka kuwasilisha. Mara nyingi, nia yao huwa ni kuchekesha pamoja na kutoa ujumbe fulani.

Taarabu na ngoma nyingine za kienyeji hutumia nyimbo na ushairi wa Fasihi Simulizi au mchanganyiko wa Fasihi Andishi. Kinachobainika basi ni kwamba Fasihi Simulizi bado yapendwa, yaigizwa na inatumiwa na kuhitajika na umma. Ukweli unaodhihirika ni kwamba Fasihi Simulizi ni muhimu na haiwezi kamwe kufa bali itabadilika na kuoana na uandishi wa teknolojia ya media ya umma.

| | |
|---|---|
| Sanaa ya maonyesho | drama/tamthilia |
| Hotuba | hotuba |
| Sifo (tungo za kusifu) | sifa |
| Wasifu | wasifu |
| Maombolezo | maombolezo |

Complete Documents
Expanded Features

| | |
|---|---|
| Methali | methali, misemo |
| Ibura, shani | kisa cha ajabu |

Pia tukitalii fani mbali mbali za Fasihi Andishi, tunaona kuwa karibu kila mwandishi wa fasihi ameathiriwa kwa njia moja au nyingine na Fasihi Simulizi. Baadhi yao wameathiriwa kifani wakati wengine wameathiriwa kmaudhui. Wengine hata wameathiriwa kwa njia zote mbili.

Kwa upande wa fani, tuna ithibati kuwa baadhi ya waandishi kama Ebrahim Hussein (Mashetani na Kinjeketile), Peninah Muhando (Pambo na Lina Ubani) wametumia wahusika ambao hupatikana katika Fasihi Simulizi. Wahusika kama wanyama, majini, mazimwi au usimuliaji wa hadithi wa moja kwa moja kwa kutumia wahusika bapa bila kujadili mandhari na nafasi za wahusika ni sifa ambayo hubainisha tanzu za Fasihi Simulizi. Tukigeukia upande wa maudhui tunaona kuwa waandishi wengi katika tanzu za Fasihi Andishi hulenga kuadili; lengo lililomo katika Fasihi Simulizi na mara nyingi hata kichwa cha hadithi huwa ni methali fulani kutoka Fasihi Simulizi. Mifano ya maandishi haya ni Mwerevu hajinyoi; Baada ya Dhiki Faraja, Afadhali mchawi, Lila na Fila Havitangamani na Umleavyo.

Fani mbali mbali za Fasihi Simulizi zilibuniwa na jamii tofauti ili kutimiza mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Baadhi ya fani hizi zimetoweka kwa vile matumizi yake pamoja na manufaa yake yalipungua. Kwa mfano, katika mataifa ya Ulaya, baada ya karne ya kumi na saba, tenzi simulizi zilipotea na pahali pake pakachukuliwa na riwaya, utanzu ambao ndio kilele cha Fasihi katika enzi za ubepari.

Fasihi simulizi, ikiwa ni sehemu ya Fasihi, hubadilika daima. Kimsingi, Fasihi Simulizi ndiyo iliyotawala katika mifumo yote ya jamii kabla ya mfumo wa ubepari kuchomoza miale yake. Fasihi simulizi ilifika kilele chake wakati wa mabadiliko kutoka katika jamii za ujima kuingia katika mfumo wa jamii za kitumwa na kimwinyi (ukabaila) na kuinukia mfumo wa ubepari. Kilele hiki kilienda sambamba na mwanzo wa kifo cha Fasihi Simulizi ya wakati huo.

Expanded Features
Complete Documents

Fasihi simulizi imesalia katika media ya umma, radio, runinga na sinema. Methali zinatumiwa katika vitabu, vitendawili vinachapishwa katika vitabu vya watoto na nyimbo za bendi za siasa zingali zinaendelea kuimbwa. Fasihi simulizi ambayo ilikuwa inatolewa watu wakizunguka moto au wakiwa vitandani jioni sasa imebadilika.

> Je hii inamaanisha kuwa Fasihi Simulizi haiwezi kujikita na kuendelea katika jamii za kisasa zenye ala za uandishi na ufundi wa kiteknolojia?

Kwa hivyo, katika kuhitimisha somo hili, kama Mbele (1982) anavyotueleza, twaweza kusema kuwa Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi zapaswa kuangaliwa kwa taswira ya mti. Mizizi na mti wenyewe ni Fasihi Simulizi nayo Fasihi Andishi ni matawi, majani na maua yake. Zimechangiana, zimeathiriana na kurutubishana.

**MAREJEO**


| | |
|---|---|
| Hussein, E.N. (1971) | 1969) Kinjeketile. Nairobi:Oxford University Press. |
| ___________(1976) | Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi. Nairobi: Oxford University Press. |
| Hyslop G. (1967) | Afadhali Mchawi. Nairobi:E.A.L.B. |
| Matteru M.L.B. (1983) | Fasihi Makala ya Semina ya Kimataifa. Dar es Salaam: TUKI. |
| Mbele J. (1983) | Oral literature and Writing Tradition. Kiswahili. Toleo la 50/2 Jarida la TUKi. Dar es Salaam:TUKI |
| Mhando P. (1975) | Pambo Nairobi; E.A.P.H. |
| __________(1984) | Lina ubani. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press. |
| Mlama, P. (1973) | The Role of Music in African Traditional Theatre. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Dar es Salaam. |
| Mnyampala M. (1968) | Ngonjera za Ukuta. Kitabu cha kwanza na cha pili. Nairobi: Oxford University Press. |

Complete Documents
Expanded Features

Mulokozi M. M. (1989) Tanzu za Fasihi Simulizi. Mulika Namba 21. Jarida la TUKI. Dar es Salaam : TUKI.

## MHADHARA WA TATU

# MAUDHUI NA FANI KATIKA FASIHI SIMULIZI

Msanii yeyote huwa na jambo ambalo amekusudia hadhira yake (wasomaji, watazamaji au wasikilizaji) wapate. Huwa na mafunzo, mawazo ambayo hudhamiria kuwasilisha kwa hadhira yake. Hayo mafunzo au mawazo yake ni malengo yake. Mawazo na mafunzo hayo hayaibuki kutokana na ombwe tupu. Kwa hivyo ni muhimu wakati wa kuchambua maudhui ya msanii kuyahusisha na hali halisi ya kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi zilizopo katika jamii. Mazingira hayo ndiyo humzaa, humlea na humkuza msanii na kwa hivyo hayawezi kupuuzwa wakati wa kuchambua maudhui ya msanii kwa sababu kwa njia moja au nyingine humwathiri katika utunzi wake.

Tukichuguza mawazo na mafunzo ya msanii tutaweza kubainisha falsafa ambazo msanii hudhamiria kuwasilisha kwa hadhira yake. Tunapozungumzia falsafa katika kazi ya Fasihi, tunamaanisha.

> Mchujo wa weleko wa mawazo muhimu yajitokezayo
> kila mara katika kazi mbali mbali za msanii.
>
> (Senkoro 1982:2)

Mawazo, mafunzo, lengo na falsafa hubainisha msimamo ama mtazamo wa msanii kuhusu masuala mbali mbali ya kijamii. Kwa kuchunguza msimamo twaweza kutofautisha kati ya msanii mmoja na mwingine ambao washughulikia suala moja. Kwa mfano, nyimbo zilizoimbwa na wapigania uhuru wa Mau Mau zilihitilafiana kutokana na wasanii. Kuna wale waliozitunga kwa lengo la kiukombozi na kuna wale waliozitunga kudhalilisha na kushtumu juhudi hizo.

Complete Documents
Expanded Features

## MAREJEO

Mulokozi M. M. (1989) Tanzu za Fasihi Simulizi Mulika Namba 21. Jarida la TUKI. Dar es Salaam: TUKI

Senkoro F. E. M. K. (1982). Fasihi Nairobi.Dar es Salaam: Nairobi.

Taasisi ya ukuzaji wa Mitala (1992) Tanzania.

## FANI

| | |
|---|---|
| (i) | Nini maana ya fani? |
| (ii) | Ainisha baadhi ya vipengele vya Fani katika kazi za fasihi simulizi; |
| (iii) | Umuhimu wa Fani katika tanzu za fasihi simulizi. |

Suala la msingi katika somo hili ni:

Fani ni nini katika tanzu za fasihi simulizi?

Wataalamu mbali mbali wamejaribu kufafanua dhana ya fani katika fasihi. Baadhi ya maoni ambayo yametolewa na Senkoro (1982:8) ni kuwa: Fani katika Fasihi ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kazi yake . Kutokana na maelezo ya Senkoro inaeleweka kwamba fani ni ustadi au ubingwa au mbinu ambazo msanii wa kazi ya fasihi hutumia katika kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake. Katika kuchangia mjadala huu kuhusu maana ya fani Mulokozi na Kahigi (1979:53) wamesema: Fani ni sanaa,ni jumla ya vipengele vya lugha vilivyowekwa katika mpangilio mahsusi ili kutoa kwetu maana fulani .

Complete Documents
Expanded Features

Kwa mujibu wa maelezo yao tunaona kuwa fani ni jumla ya vipengele vya lugha ambavyo msanii hutumia katika kutoa maana fulani kwa hadhira. Maelezo haya yana utata kwa vile yatubidi kuelewa maana ya lugha na zaidi ya hayo vipengele vyake. Isitoshe, katika fani hasa katika fasihi simulizi kuna baadhi ya vipengele ambavyo hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe ambavyo si vya lugha lakini ni vya ishara nyinginezo za kisanaa. Lugha huwa ni mojawapo tu ya vipengele vya fani.

Taasisi ya ukuzaji mitaala (1988:168) nayo inaeleza kuwa: Fani ni umbo lililosarifiwa ili kuelezea hisia za fanani . Maelezo haya yanatuelekeza kwa dhana kuwa fani ni jinsi msanii anavyofinyanga umbo fulani na umbo linamaanisha utanzu au aina ya sanaa. Kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu tuliowanukuu tunaona kuwa fani ni jumla ya vipengele vyote vya fasihi ambavyo msanii hutumia katika juhudi za kuelezea hisia au maoni yake kwa njia ya ufasaha.

Miongoni mwa vipengele hivi ni:

(1) Tukio

Katika tanzu za Fasihi Simulizi, mara nyingi ni lazima pawe na jambo au tukio ambalo huchukuliwa kama kiini na chanzo cha utanzu utakaohusishwa. Fani au utanzu unaotumiwa na msanii hauibuki tu vivi hivi. Tukio huwa ndilo kishawishi cha fanani wa Fasihi Simulizi. Kwa mfano nyimbo za unyago huibuka katika mazingara yake. Hadithi za sifa za ushujaa zaweza kuibuka katika mazingara ya vita. Methali za kutuliza zaweza kutumiwa pale ambapo pana majonzi ya aina fulani. Kwa hivyo kile tunasisitiza ni kwamba ni lazima pawe na tukio ambalo litakuwa chem. Chem. Ya utanzu utakaotumiwa na fanani kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira yake.

(2) Mazingira

Mazingira au muktadha ni kipengele kingine cha fani ya Fasihi Simulizi.

| |
|---|
| Jukumu la mazingira ni lipi katika tanzu za Fasihi Simulizi? |

Complete Documents
Expanded Features

Kwanza ni muhimu kuelewa kuwa mazingira ni pale mahali ambapo matukio ya Fasihi Simulizi huibuka ama hutokea. Ufundi wa kuchora mazingira unajitokeza pale ambapo fanani huchora picha halisi, picha inayoonekana wazi wazi juu ya mazingira husika.

Fasihi Simulizi hutegemea sana muktadha na mazingira maalum. Kutokana na hali hiyo tungo za Fasihi Simulizi huwa zimejikita katika utamaduni wa jamii zinamoibukia. Vifaa ambavyo vinatumika katika Fasihi Simulizi hutegemea mazingira yanayohusika. Kwa mfano msanii anapodhamiria kutoa picha ya kuogofya anatuchorea mazingira ambayo yanaogofya. Aweza kutumia mazingira ya misitu na wahusika kama majitu ili kuleta dhana ya hofu katika mazingira yake.

(3) Umbo

Kipengele kingine cha fani katika tanzu za Fasihi Simulizi ni kipengele cha umbo ambacho kinaashiria muundo na mtindo wa utanzu unaohusika. Kama tutakavyoona baadaye kigezo kimoja ambacho kinatumika katika kuzianisha tanzu za Fasihi Simulizi katika makundi mbali mbali ni kile cha umbo. Tanzu za Fasihi Simulizi zimeanishwa kimaumbo katika matapo kama

(1) Mazungumzo

(2) Masimulizi

(3) Maigizo (drama)

(4) Ushairi – (a) Nyimbo
(b) Maghani

(5) Semi

(6) Ngomezi (Tungo za ngoma) (Mulokozi 1989:3)

Complete Documents
Expanded Features

Kila mojawapo wa maumbo haya huwa na sifa zake kimuundo na kimtindo kama tutakavyoona katika sehemu ya pili ya kozi hii.

| |
|---|
| Suala linalotujia ni je, Muundo ni nini kama sehemu ya fani katika Fasihi Simulizi? |

Muundo katika Fasihi Simulizi ni mtiririko wa visa na matukio. Katika muundo tunazingatia jinsi fanani alivyofuma na kuunda na hata jinsi ameungaisha tukio moja na lingine, kitendo kimoja na kingine, wazo na wazo, ubeti na ubeti na hata mstari wa ubeti na mwingine. Kwa hivyo tunachunguza jinsi kazi imefumwa kimpangilio, kisura, kimaonyesho, kiubeti na kadhalika.

Kuna miundo mbali mbali katika tanzu mbali mbali za Fasihi Simulizi. Kuna muundo ya moja kwa moja na kuna miundo changamano. Baadhi ya miundo ni kama vile ya kiutelezi. Katika miundo ya aina hii, hadhira huweza kufuata matukio mbali mbali kutoka mwanzo hadi mwisho kwa mbinu ya utelezi.

Katika mashairi ipo miundo mbali mbali ambayo hutumiwa kuainisha mashairi kwa mujibu wa idadi ya mistari katika kila ubeti. Miundo hii ndio hutupa mashairi ya tarbia, tathlitha, takhmisa na kadhalika.

Katika hadithi na hata katika tamthilia waweza kuwa na muundo ambao fanani ameanza kutoka mwanzo akaenda katikati na baadaye kumalizia kisa chake. Aina hii ya muundo imeitwa mtiririko shanga. Mtiririko wa aina hii hujengwa kwa kutumia visa au vitukio mbali mbali na vinaweza kuongezwa na kupunguzwa bila kupoteza maana ya hadithi au tamthilia. Kipengele kingine cha fani ambacho huenda sambamba na muundo ni mtindo.

| |
|---|
| Mtindo ni nini katika Fasihi Simulizi? |

Expanded Features
Complete Documents

Watu wengi sana huchanganyikiwa kuhusu dhana ya muundo na mtindo.

Mtindo katika kazi ya Fasihi ni ile namna ambayo msanii hutunga kazi hiyo na kuipa sura ambayo kifani na kimaudhui huainisha kanuni za kaida zilizofuatwa kama ni zilizopo (za kimapokeo) au ni za kipekee. Kwa mkururo wa maelezo hayo, twaweza kusema kuwa mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya Fasihi kwa njia ambayo hatimaye hubainisha au huonyesha nafsi na labda upekee wa mtunzi wa kazi hiyo:

Mtindo huwa na sehemu mbili kuu:-

(a) Maudhui na Fani

(b) Nafsi ya msanii ambayo hujitokeza katika ndoa kati ya fani na maudhui. Hapa tunatumia nafsi kwa maana ya uafikiano baina ya wazo linaloelezwa na mwelezaji wa wazo hilo.

Kutokana na mtindo wa kazi ya Fasihi inakuwa ni vigumu kubadili sentensi hata neno katika kazi hiyo bila kubadili mtindo wenyewe. Kwa hivyo, twaweza kusema kuwa mtindo ni ile namna ambayo mtunzi huipa kazi yake ya kifasihi sura kifani na kimaudhui kwa njia ambayo mtunzi mwingine asingeweza kuipa.

| |
|---|
| Tunamaanisha nini tunaposema haya? |

Kile tunachosisitiza ni kuwa hata ikiwa watunzi wawili watashughulikia mada moja mitindo yao itakuwa tofauti na hapa ndipo tunaafiki kauli kuwa: Mtindo ni mtu Mtindo ndio unawawezesha watazamaji, wasikilizaji na hata wasomaji kung amua mtunzi wa kazi hiyo hata bila kumwona ama kusoma jina lake.

Complete Documents
Expanded Features

(4) Lugha

Pengine hiki ndicho kipengee muhimu zaidi katika fani ya Fasihi. Kama Khatib (1981: 16) anavyodokeza, lugha katika fasihi iwe simulizi au andishi: Lazima iwe na utanashati na ulimbwende wa kipekee wenye mvuto na mnato wa kuteka na kusisimua hisi za wasikilizaji wasomaji au watazamaji .

Lugha ndio malighafi ya Fasihi. Lugha inayotumika katika Fasihi ni lugha ya kisanaa inayopamba na inayokusudia kuibua hisia fulani kwa hadhira yake. Yaweza kuathiri nyoyo za hadhira kulingana na jinsi inavyotumiwa kwa lengo la kuchekesha, kukejeli, kubeza, kuchokoza, kutia hamasa au kushawishi.

Matumizi ya lugha fasaha, uteuzi wa msamiati na matumizi ya misemo na methali zinazosadifu mazingira ya jamii husika hufanya fasihi simulizi kuwa na sumaku za kuvuta msomaji, msikilizaji au mtazamaji. Zaidi ya hayo, tamathali mbali mbali za usemi huongeza uhai katika fasihi na kuifanya itimize lengo lililokusudiwa. Kwa hivyo, lugha huwa na mguso, mvuto na mnato wa aina ya ajabu kwa hadhira iliyokusudiwa. Hii ndio sifa ya lugha ya kisanaa ambayo inasadifu dhamira. Kila mazingira hupatiwa lugha yake kutegemea dhamira na muktadha. Hapa ndipo tunapata lugha za aina kama lugha ya kisheria, lugha ya kidini, lugha ya kijando na kadhalika.

Tamathali za usemi hutumika kujenga picha. Mifano ya tamathali hizi ni kama sitiari, tashihisi, kejeli, kijembe, ishara, tauria, simo na kadhalika.

Taswira ni mojawapo wa mbinu ambazo hutumiwa na msanii wa fasihi simulizi ili kuwasilisha ujumbe wake.

| |
|---|
| Taswira ni nini? |

Complete Documents
Expanded Features

Taswira ni mkusanyiko wa picha mbali mbali ambazo huundwa kwa njia ya maelezo na wasanii katika kazi ya fasihi.

Mara nyingi taswira huambatana na matumizi ya tamathali za usemi hasa za stiari na tashbihi. Katika taswira twaweza kubainisha matumizi ya ishara mbali mbali zinazowakilisha mawazo, dhana, vitu au watu.

Taswira huwa ni lugha ambayo inachora picha ya watu, vitu au mahali kwa kutumia ishara. Katika taswira twaweza kubainisha maelezo ambayo jinsi yanavyopangwa na msanii huweza kufanya hadhira zipate aina mbali mbali za hisi kama za kusikia, kuona, kuonja na kunusa. Taswira hutumiwa na wasanii ili kunasa hisia za hadhira zao. Wasanii hutumia maneno ambayo huumba picha kamili ya kitu, hali, wazo, dhana au uzoefu fulani wa jamii inayohusika.

Matumizi ya picha mara nyingi huenda sambamba na yale ya ishara. Ishara ni dhana au mawazo mbalimbali yanayotumiwa na wasanii katika kazi zao za Fasihi kuwakilisha vitu, dhana au mawazo mengine. Kwa mfano radi na ngurumo zaweza kuashiria vita na hangaiko. Matumizi mema ya taswira na ishara hutegemea ubingwa wa msanii wa kuchota mambo mbalimbali katika mazingira ya jamii anayohusisha katika sanaa yake.

Lengo kuu la kutumia taswira ni kusisitiza maudhui yanayotolewa. Kwa hivyo kufaulu au kutofaulu kwa matumizi ya taswira, kutatathminiwa kwa mizani na jinsi taswira hizo zimesaidia kuwakilisha au kuzuia maudhui yaliyokusudiwa.

Toa mifano ya tamathali zingine za usemi
ambazo hutumiwa katika fasihi simulizi na
ueleze dhima yake katika Fani ya Fasihi

Complete Documents
Expanded Features

simulizi.

Fasihi simulizi haitegemea maneno pekee ili iweze kukamilika. Tungo za Fasihi Simulizi hutegemea sana visaidizi vya kuonekana na kusikika (Finnegan 1970, Matteru 1981)

Masimulizi mengi hutegemea visaidizi kama sauti, miguno, ngurumo, misogeo katika kueleza dhana ambazo haziko katika maneno. Masimulizi mengi pia hutegemea miondoko, na vitabia mbali mbali kueleza dhana fulani (Matteru 1979). Haya yaweza kusemwa pia kuhusiana na nyimbo na misemo. Kulingana na ufundi uliotumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe wake kazi za Fasihi Simulizi huwa na upeo.

Upeo ni nini?

Upeo katika Fasihi simulizi ni kilele cha kazi yenyewe. Kuna upeo wa aina mbili

(a) Upeo wa juu

(b) Upeo wa chini.

**UPEO WA JUU**

Upeo wa juu ni sehemu za kazi hiyo ambazo hutosheleza haja za wasikilizaji au watazamaji. Katika sehemu hii hadhira hupata ujumbe muhimu ambao kazi ya sanaa ilikuwa imechelewesha kuwasilisha kwa kutumia mbinu kama za taharuki, mbinu rejeshi, na mtindo wa kuitelezi. Mara nyingi watunzi wa kazi za Fasihi huweka kipeo cha juu mwishoni mwa kazi zao hata ingawa si lazima kuwa na kipeo kimoja tu. Wakati mwingine waweza kupata kazi ya Fasihi simulizi ambayo haina kipeo kabisa.

Complete Documents
Expanded Features

Katika Fasihi wasanii hujenga mgogoro ambao hujitokeza na kukua kadiri kazi hizo zinavyokwea kuelekea kwenye upeo wa juu. Kipeo cha juu hutokea pale ambapo msanii hujaribu kutoa suluhisho kwa mgogoro alioujengea kazi yake.

## UPEO WA CHINI

| |
|---|
| Navyo vipeo vya chini ni nini? |

Upeo wa chini ni pale ambapo haja na matarajio ya hadhira hayakukidhiwa. Katika baadhi ya kazi za Fasihi vipeo vya chini huwa dhihirisho la udhaifu wa kazi hiyo. Lakini katika kazi zingine upeo wa chini huwa umekusudiwa hivyo na mtunzi.

## UCHESHI KATIKA KAZI YA FASIHI SIMULIZI

Ucheshi ni kipengee muhimu cha kifani katika kazi za Fasihi Simulizi. Ucheshi ni mbinu ya kifani ambayo watunzi hutumia katika kazi zao za Fasihi kwa lengo la kuchekesha na kuburudisha hadhira zao. Vichekesho hutumiwa kwa nia ya kuburudisha hadhira na kuiondolea uchovu.

Wasanii mbali mbali hutumia mbinu tofauti tofauti kuleta vichekesho katika kazi zao. Baadhi yao hutumia vitendawili ili kujenga kejeli, dhihaka n.k. vichekesho pia huweza kutumiwa ili kujenga maudhui.

## WAHUSIKA

| |
|---|
| Wahusika huwa na dhima gani kifani<br>Katika kazi za Fasihi Simulizi? |

Expanded Features
Complete Documents

Njia muafaka ya kujibu swali hili ni kufafanua maana ya wahusika na jukumu lao katika kazi za Fasihi Simulizi. Wahusika ni viumbe ambavyo hutumiwa na msanii katika mtiririko wa vitukio kueleza kisa chake. Wahusika hawa waweza kuwa watu, miti, wadudu, mizimu, misitu na wanyama. Wahusika huwa viumbe ambavyo hutenda na kutendewa. Wanatumiwa na msanii kusimamia hali mbali mbali za binadamu katika jamii wanamoishi. Wanazungumza na huzungumziwa. Hawa ndio uti wa mgongo wa fani ya Fasihi Simulizi. Bila wahusika mtiririko wa vitukio hukosa pahali pa kujishikilia. Wahusika ni viumbe maalum wa watunzi kwa vile ndio wanaotumia kutoa picha au kuwasilisha mawazo na fikira zao kwa jamii inayowakilishwa na wahusika hao.

Wahusika hutumiwa kwa njia nyingi na wasanii wa Fasihi. Jukumu la wahusika hutegemea sana lengo ama madhumuni ya fanani. Mifano ya matumizi ya wahusika ni wale ambao watumiwa kibapa. Hawa hutumiwa kama sanamu ama mapicha ambayo yanaonyesha tabia fulani katika kazi ya Fasihi Simulizi. Wahusika wenyewe huumbwa ili wajenge mori katika hisia za hadhira. Kwa mfano wahusika kama mazimwi hutumiwa kuogofya hadhira. Wengine kama fisi hutumiwa kuchekesha hadhira kwa tabia zao za uzembe na ujinga. Hata hivyo katika tanzu za Fasihi Simulizi si lazima wahusika wakamilike kama viumbe halisi.

Wahusika wengine hujengwa kuwa vielelezo au wawakilishi wa makundi fulani ya watu. Aghalabu wahusika hawa kwa haiba na silka yao huwa ni watu binafsi lakini huwakilisha sehemu maalum ya jamii. Waweza kuwakilisha wazee, vijana, wanawake, mapadri, wahuni, wasomi na kadhalika. Kuna wahusika ambao hujengwa ili watumiwe kikweli katika tanzu za Fasihi Simulizi. Wanaumbwa ili waweze kuaminika katika matendo, maneno na mawazo yao kama watu wanaoishi kweli. Kutokana na ujenzi huo mtazamo wa wahusika juu ya maisha hukua na kubadilika pamoja nao. Hawa waweza kupimwa na kuchunguzwa kwa vigezo vya binadamu halisi wakiwa katika ulimwengu wa fani

Complete Documents
Expanded Features

wanayotumika. Wahusika kama hawa huwa ni rahisi kuwatambua kama wawakilishi wa watu fulani katika jamii. Ujenzi wa wahusika hupimwa kwa mizani ya mtunzi. Je mtunzi amefaulu kuwaumba wahusika ambao wamemsaidia kuwasilisha ujumbe wake? Mara nyingine watunzi wa tanzu za Fasihi Simulizi hutumia hadhira zao kama wahusika. Kuna hadhira za aina nyingi katika tanzu za Fasihi Simulizi. Hadhira ni wasikilizaji ama watazamaji. Mara nyingi hadhira huchukuliwa kuwa mkusanyiko wa watu au vitu ukiwa na lengo la kuathirika kutokana na jambo linalotendeka au linalotendwa (Msokile 1981: 44).

Katika utanzu wa nyimbo ambao una viitikio (choruses) msanii hutumia hadhira kama waitikiaji. Waitikiaji huwa na jukumu la kuidaka sehemu ya wimbo kila baada ya mwimbaji kumaliza kuimba ubeti mmoja wa wimbo. Jukumu kubwa la waitikiaji ni kupumzisha fanani hasa mwimbaji. Mbali na hayo wanaleta mabadiliko ili watazamaji na wasikilizaji wasichoshwe na sauti moja ya mwimbaji. Aghalabu waitikiaji huwa wake na waume pamoja lakini kuna uwezekano wa kuwa na wanawake pekee kama katika mazingira ya unyago au waume pekee katika jando. Hata hivyo ni muhimu kuelewa kuwa si kila wimbo huwa na kiitikio na kwa hivyo ikiwa wimbo hauna kiitikio hata waitikiaji hawapo. Hatimaye, Fasihi Simulizi huwa na hadhira tendaji au yenye kushiriki katika utendaji wa kazi yenyewe. Kwa mfano katika ngoma waweza kucheza na kama tulivyoona katika nyimbo waweza kuitikia. Vile vile waweza kupiga makofi, vigelegele na kushangilia. Hata katika usimuliaji wa hadithi, hadhira haikai tu kimya na kusikiliza fanani bali huitika kwa maneno. Kama ehe, tena ikawaje. Mara nyingine ikiwa hadithi ina wimbo wanashiriki katika kuimba wimbo huo.

**MAREJEO**


Finnegan R. (1970) Oral literature in Africa. London: Oxford University Press.

Khatib A. H. (1981) Misingi ya Nadharia ya Fasihi Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Zanzibar

Matteru M. L. B. (1981) Fasihi Simulizi na Uandishi Fasihi Makala ya semina ya kimataifa ya waandishi wa kiswahili III Dar es Salaam: TUKI.

Expanded Features
Complete Documents

Msokile M (1992)__ Misingi ya hadithi fupi fupi. Dar es Salaam: TPH.

## MHADHARA WA NNE

## NJIA ZA KUZIANISHA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI

Baada ya mhadhara huu utaweza:

(a) Kubainisha baadhi ya sababu zinazowafanya binadamu kushughulikia taaluma mbalimbali kwa mpango maalum.

(b) Kufahamu njia zinazotumiwa kuzigawa tanzu za fasihi simulizi katika makundi tofauti tofauti

(c) Kuonyesha manufaa na upungufu wa njia hizo.

Kila taaluma ina njia zinazotumiwa kuzungumzia dhana zake na matawi yake mbali mbali. Ukiangaza katika ujirani wako kwa makini, utagundua kwamba imani walizo nazo watu na ujuzi wao juu ya nyanja tofauti tofauti za maisha ya binadamu zitakupa fununu kuhusu njia walizozitumia kupata ama imani hizo au ujuzi huo. Baadhi ya watu watadai kwamba ujuzi wao umetokana na ujarabati. Maadamu kuna ujuzi wa aina nyingi, njia ya kupata ujuzi huo pia ni nyingi. Hivyo ndivyo ilivyo na fasihi simulizi vile vile. Mitaala ambayo imefanywa juu ya fasihi hii imeonyesha kwamba kuna njia mbili zilizotumiwa kuzianisha tanzu zake.

Kwa nini wanadamu hutaka kuugawa ujuzi wao katika makundi makundi?

Kwa nini wanadamu hutaka kuugawa ujuzi wao katika makundi makundi?

Kwa nini wanadamu hutaka kuugawa ujuzi wao katika makundi makundi?

Sababu ya kwanza na ya wazi inayowafanya wanadamu kuubainisha ujuzi wao ni kurahisisha ufahamu wa ujuzi huo. Kama mambo mbali mbali hayakupangwa kwa namna inayoelezeka na kufuatika kwa urahisi, basi mambo

Complete Documents
Expanded Features

hayo yangekuwa mchanganyiko usiofahamika kwa mpango, mchanganyiko usiokuwa na mbele wala nyuma.

Fasihi simulizi iko vivyo hivyo. Tunashughulikia njia za kuzigawa tanzu zake katika matawi mbali mbali kwa kuwa tunataka kufahamu mielekeo na sababu zilizowafanya wataalamu wa fasihi hiyo kuizungumzia vile walivyoizungumzia. Kwa ujumla, njia mbili zimekuwa zikitumiwa kutalii fasihi simulizi. Kwa mujibu wa maelezo ya G. Kubik katika makala yanayoitwa Recording and Classification of Oral literature in Tanzania (1977), kuna njia za kupachikwa kutokana na wageni na zile zitokanazo na wenyeji wenyewe.

## NJIA ZA KIGENI

Tunaposema kwamba baadhi ya wataalamu hutumia njia za kigeni, tuna maana kwamba katika kuichambua fasihi simulizi ya jamii fulani, kategoria zisizotokana na fasihi hiyo hutumiwa. Kwa mfano, wageni walipoingia katika bara la Afrika, walikuja na utamaduni wao. Fasihi yao andishi kwa simulizi ilikuwa sehemu ya utamaduni huu. Hawa wageni walikuwa na tanzu zao za fasihi simulizi. Walipofika huku, baadhi yao hawakushughulikia tanzu za fasihi za wenyeji waliokurubiana nao. Baada ya kujifunza lugha za wenyeji, kile walichofanya ni kupachika kwa majina ya kikwao juu ya tanzu za fasihi simulizi zisizokuwa za kwao. Walifanya hivi pasi kuzingatia tofauti za tanzu zinazotokana na mazingira tofauti. Tanzu za fasihi za wenyeji zilizoelekea kushabihiana na za wageni zilianishwa kwa kanuni na kaida za kigeni. Na zile ambazo hazikulingana na za kigeni zilipuuzwa.

G. Kibuk, Mtaalamu tuliyemrejelea kitambo anasema kwamba katika kuelezea na kufasili fasihi ya wenyeji kwa kufuata njia za kigeni, mambo mengi yanayohusu fasihi simulizi ya wenyeji hayatiliwi maanani. Njia za kigeni aghalabu huwa na msingi. Mara nyingi, huwa zimeongozwa na imani kwamba bara la Afrika halina mapokeo yoyote ya usanii. Ruth Finnegan (1987:27) ameonyesha uketo wa mapendeleo haya kwa kumrejelea Mzungu anayeitwa Burton:

Expanded Features
Complete Documents

> Mila za washenzi za kutembea uchi zimeupofusha ubongo na kuangamiza kaida zote za lugha. Hakuna ushairi huko ushenzini. Hakuna mizani hakuna vina, hakuna chochote kinachozindua hisi au kuteka fikra za msikilizaji.

Mawazo kama haya hayawezi kumpa Mwafrika uhuru wa kujielezea fasihi. Pia, hayampi Mzungu fursa ya kuangalia tanzu za fasihi simulizi kwa mtazamo na mwelekeo wa Kiafrika. Sababu ni kwamba, kitambo imeishadaiwa kwamba Mwafrika hana fasihi.

Mapendeleo mengine yamekita katika kile kinachoelezwa na watafiti wa Kizungu kuwa uajabu wa Mwafrika. Kuna madai kwamba lugha ya mshenzi imekolewa na uchawi na kwamba washenzi huzalisha sanaa yao kujumuia. Anasema kwamba Mzungu anayetarajia kupata aina zote za vileo vya humu barani ataambulia patupu. Sababu ni kwamba kuna aina nyingi za vileo visivyopatikana Ulaya humu barani. Mfano huu wa vileo unaonyesha kwamba kuna tanzu nyingi za fasihi simulizi barani zisizopatikana Ulaya. Pendekezo la Kubik ni kwamba ingefaa kama watafiti wangejizatiti kujua mapya kutokana na utafiti badala ya kwenda nyanjani kuthibitisha imani zao na mapendekezo yao.

| |
|---|
| Je njia hizi za kigeni hazina manufaa yoyote? |

Upungufu wa njia za kigeni unaoonyeshwa na Kubik ni kweli. Hata hivyo, kuna manufaa kadhaa yanayotokana na njia za kigeni za kugawanya tanzu katika makundi. Njia hizi zikitumiwa kwa uangalifu, zinaweza kusaidia katika ulinganishaji wa fasihi za tamaduni mbali mbali. Sababu ni kwamba licha ya upungufu uliobainishwa, njia hizi zinaweza kutumiwa kuainisha sifa zinazofanana na zisizofanana katika fasihi simulizi zinazotoka katika tamaduni tofauti tofauti.

Complete Documents
Expanded Features

**NJIA ZA WENYEJI**

Tumekuwa tukizungumzia faida na upungufu wa kutumia njia za kigeni za kutafiti. Njia za kienyeji nazo pia zina manufaa yake na matatizo yake. Katika kuzitumia njia hizi, mtafiti hujilowa katika utamaduni wa watu ambao jamii yao inatafitiwa. Kutokana na hojaji anazofanya, mtafiti huweza kuibuka na majina ya tanzu kulingana na jinsi zinavyoitwa na wenyeji wake.

Manufaa yanayotakana na njia hizi ni kwamba fasihi ya watu haina maelekeo ya kupotoshwa. Mtafiti hujaribu juu chini kuona kwamba kile kinachowasilishwa kinasadifu hali halisi ya wenyeji. Lakini mtafiti akijiingiza sana katika jamii anayotafiti bila kupanua mtazamo wake kwa kulinganisha yale anayopata na yanayopatikana katika sehemu nyingine za ulimwengu, atakuwa na msimamo finyu kuhusu fasihi simulizi kwa ujumla. Katika kiwango cha kinadharia mtafiti atafaidika kwa ujumla. Katika kiwango cha kinadharia, mtafiti atafaidika zaidi iwapo atakurubiana na tajriba nyingi za fasihi simulizi.

Kwa hivyo, inapendekezwa kwamba njia hizi zinaweza kusaidiana na kuchangiana. Maana fasihi yoyote ile ina utaifa wake na umataifa wake. Sifa zinazopatikana katika fasihi nyingi za mataifa mbali mbali zinadhihirisha kwamba kijumla fasihi zote zinalingana kwa njia fulani. Hata hivyo, kila mazingira yaweza pia kuibusha fasihi kivyake na kipekee kutangamana na mahitaji ya wale wanaoizalisha.

| |
|---|
| Jadili faida na upungufu wa njia za kienyeji katika kuigawa fasihi simulizi katika makundi tofauti tofauti. |

**MAREJELEO**

PDF Complete Expanded Features Unlimited Pages

Finnegan R. (1987) The perception of African Oral literature Oral Literature in Africa. Nairobi. Oxford University Press.

Kubik G. (1977) Recording and Classification of Oral Literature in TanzaniaDar es Salaam. Geothe Institute.

Mulokozi M. M. (1983) Utafiti wa Fasihi Simulizi katika Makala za Semina ya kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi . Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

## MHADHARA WA SITA

## VIGEZO VYA KUGAWA FASIHI SIMULIZI KATIKA TANZU

### MADHUMUNI

Baada ya mhadhara huu, utaweza:

(a) Kutoa kielezi cha kigezo

(b) Kuorodhesha baadhi ya vigezo vinavyotumiwa kubainisha tanzu za fasihi simulizi.

(c) Kuonyesha iwapo kuna utata wowote katika vigezo hivi

Neno vigezo ni wingi wa kigezo . Kigezo ni kipimio au kuchujio. Katika muktadha huu, vigezo ni mizani zinazotumiwa kuzigawa tanzu za fasihi simulizi katika makundi tofauti tofauti.

> Tutajuaje kama utanzu unaozungumziwa ama ni kitendawili au ni methali au ni ngano?

Jambo la kwanza linaloweza kumsaidia mtafiti kujua na kuzianisha tanzu za fasihi simulizi ni kutambua majina yake. Kuna majina kama vile ngano, tarihi, vitendawili tauria, tenzi na methali. Tanzu hizi zimepewa majina tofauti tofauti kwa sababu majina hayo yanaashiria tofauti zao kidhahania na za kunasibisha.

Complete Documents
Expanded Features

Tanzu zinaweza kutambulika kwa kuilinganisha miundo yake na kanuni zinazofuatwa katika kuzitamba au kuziigiza. Kadhia kama masimulizi na maigizo huweza kutumiwa kuutambua utanzu fulani. Kusimulia, kunaufanya utanzu usiitwe wimbo. Sababu ni kwamba masimulizi hutambwa nao wimbo huimbwa.

Pamoja na kulinganisha miundo na kaida za maumbo aina aina ya fasihi simulizi, tanzu zinaweza kujulikana kwa kuichunguza mianzo na miisho yake. Angalia mifano ifuatayo:

(a) (i) Kitendawili

(ii) Tega

(b) (i) Hadithi, hadithi?

(ii) Hadithi njoo.

(c) (i) Paukwa

(ii) Pakawa

(iii) Kaondoka chanjagaa
Kajenga mji kakaa
na mwanangu mwansiti
Vijino kama yakuti
Kinywani kama ukuta na
vilango vya kupita. Hapo
zamani za kale

(d) Huyo mtoto alifanya haraka,
Akajikuta ya taabani
Mnakumbuka

(e) Bismillahi naikadimu
Hali ya kutunga hino nudhumu
Na ar – Rahimu nyuma ikae.

(f) .. wakakaa raha mustarehe.

Kutokana na mianzo na miisho ya aina hii, utanzu waweza kujulika. Ni wazi kwamba:

(a) Ni kitendawili
(b) Ni ngano

Expanded Features
Complete Documents

(c) Pia ngano
(d) Inatumia methali na
(e) Ni mwisho wa ngano.
(f) Kumbuka kwamba huu ni ubeti wa kwanza wa Al – Inkishafi.

Tumeweka hapa kuonyesha kwamba jambo hili ni kweli pia katika muktadha wa fasihi andishi. Unaweza kutaja mianzo na miisho mingine inayotambulisha tanzu za fasihi simulizi?

Kigezo kingine cha kuujua utanzu wa fasihi simulizi ni kuutizama mtindo wake. Mtindo unashirikisha mambo kama matumizi ya lugha, sajili, na hata kidatu (pitch). Ukariri unaweza kuonyesha iwapo utanzu fulani ni wimbo au si wimbo. Utendi unatofautiana na kharafa kwa upande wa vitushi. Utendi una matukio mengi unavyovifanya vitushi vyake kuwa vigumu na ilhali kharafa ina matukio machache yanayowasilishwa moja kwa moja.

Tumeyazungumzia mambo ya kimtindo kama kwamba mambo haya yanajisimamia peke yake; ukweli ni kwamba mtindo hutegemea maudhui na dhamira. Maudhui mbali mbali huweza kuwasilisha katika tanzu tofauti tofauti. Mara nyingi, maudhui mateule huwasilishwa katika tanzu zinazoafiki uteule. Kwa mfano, katika jamii nyingi, matukio mengi kuhusu mashujaa husimuliwa katika utendi. Nazo nyimbo za dhihaka huweza kuimbwa katika mazingira ya kufanyia tohara ambapo watu watakubaliwa kiada kutoleana matusi bila hofu, aibu wala adhabu. Watu huwa na leseni ya kuwashambulia wanajamii wenye mienendo mibaya.

Jamii nyingi za kijadi na hata za wakati wetu ni za kitabaka. Baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hudhihirika kulingana na namna zinavyoipambanua jamii kitabaka. Kuna nyimbo katika jamii zetu zinazopaswa kuimbwa na watoto. Jinsia ni namna nyingine ya kuziangalia tanzu za fasihi simulizi na kuzigawa katika makundi tofauti tofauti. Kuna tanzu ambazo hutambwa na wanawake, na zingine zinazotambwa na wanaume. Utanzu kama khuswala kumuse[1] unatambwa na wanaume peke yake.

Complete Documents
Expanded Features

Wahusika wanaosawiriwa katika tanzu mbali mbali wanaweza kutumiwa kama kigezo cha kuzianisha tanzu hizo. Kharafa na hekaya huainishwa kwa kuwa wahusika wa kharafa ni wanyama na ilhali wahusika wa hekaya ni binadamu. Ngano zinaweza kuitwa ngano za majitu kwa sababu wahusika wake wengi ni majitu. Nyingine zaweza kuitwa ngano za ujanja kwa vile mhusika wake mkuu ni mjanja kama vile sungura mjanja au mzee kobe.

Kigezo cha mwisho muhimu kinachoweza kutumika kuufahamu utagaa wa fasihi simulizi ni mahali na wakati pa kutambia. Kuna tanzu zinazotambwa usiku na nyingine zinazoshughulikiwa mchana. Wakati na mahali ni mambo yanayotegemea mila za jamii zinazohusika.

| |
|---|
| Je, kuna utata wowote katika vigezo vilivyo elezwa? |

Hivi ndivyo baadhi ya vigezo ambavyo vinaweza kumsaidia mtafiti kuzigawa tanzu za fasihi simulizi katika matawi yake. Vigezo hivi ni vingi. Kuna vile vinavyoingiliana na vingine vinavyochangiana. Baadhi ya vigezo vinatekeleza majukumu haya kwa pamoja. Hii ina maana kwamba utanzu mmoja wa fasihi simulizi waweza kupatikana katika makundi ama mawili au zaidi. Mazingira yanaweza kutokea ambapo mipaka inaweza kukiukwa. Tarihi ni masimulizi. Lakini ikirutubishwa na tanzu nyingine kisha ikawasilishwa katika mahadhi ya ushairi, itakuwa utendi. Jambo hili halimaanishi kwamba tarihi imepoteza utarihi wake wote inapobadilika na kuwa utendi.

Pia baadhi ya nyimbo haziwezi kutofautishwa hasa zile zilizoimbwa katika mazingira ya starehe. Wimbo unaomkejeli bwana arusi katika arusi waweza kutokea katika sherehe za tohara. Kwa hivyo, ikiwa vigezo hivi vitakuwa na msaada wowote katika kurahisisha ufahamu wa tanzu za fasihi simulizi, itabidi kuziorodhesha sifa nyingi zinazoubanisha utanzu fulani. Isifikiriwe kwamba kazi hii ni rahisi. Inahitaji utafiti mpana kufanywa ili majawabu yanayosadifu ukweli wa maisha ya watu fulani yapatikane.

---

[1]Utanzu unaotambwa katika baadhi ya jamii za Baluhya baada ya kifo cha mtu hususa mzee aliyeheshimika. Hujaribu kuwaliwaza na vile vile kumweka marehemu katika mkabala wa kihistoria ya jamii yake.

**MAREJELEO**

PDF Complete
Expanded Features
Unlimited Pages

Ben – Amos, Dan (1977) Folkrole in Africa in Bernth Lindfor s Forms of Folkrole in Africa. Austin: University of Texas Press.

Lusweti, B. M. (1984) The hyena and The Rock Nairobi: Macmillan.

Mulika 19 (1987)

Mulika 20 (1988)

## MHADHARA WA SABA
## UTUNZI NA UHAKIKI KATIKA FASIHI SIMULIZI

**Katika sehemu hii, mshiriki anapaswa :**

Wadhifa wa mtunzi katika fasihi simulizi

(a) Mazingira yanayofadhilisha utungaji katika fasihi simulizi.

(b) Njia zinazotumiwa na wana sanaa katika kutunga fasihi simulizi.

Kama tulivyoonyesha katika sehemu ya madhumuni, mhadhara huu una lengo la kuonyesha dhima ya msanii na jinsi anavyoitekeleza dhima hiyo katika fasihi simulizi. Tunapozungumza juu ya utunzi, tuna maana ya jinsi ya kuisana kazi ya sanaa. Muktadha tunaozungumzia hapa ni wa tungo zinazofinyangwa kwa minajili ya kupokewa kwa mdomo.

Kwanza kabisa, inapasa kueleweka kwamba mtunzi ni sehemu ya jamii iliyomzaa na kumlea. Licha ya kwamba anaweza kuwa ametunukiwa na kipawa cha kipekee cha kutunga, malighafi yote anayotumia kutunga yanatokana na jamii yake. Maudhui yake yanachotwa kutoka kwa jamii. Aidha nahau zake, stiari zake na hata tashbihi zake hutoka katika mazingira yake. Ni kweli kwamba mwanasanaa mwenye kipawa cha juu cha kubuni aweza kuifinyangia jamii picha ngeni ambayo si rahisi kuitambua moja kwa moja. Lakini hatimaye jambo atakaloitungia jamii linatokana na jamii yenyewe. Mikarara na vikale atakavyotumia kutunga pia vinatokana na jamii ile.

| |
|---|
| Kuna uhusiano gani baina ya msanii na jamii yake? |

Expanded Features
Complete Documents

Wanjiku Mukabi Kabira anasema katika kitabu chake The Oral Artist (1983) kwamba wasanii walikuwa na nyadhifa tofauti tofauti katika jamii za kijadi. Kazi ya mtunzi katika mfumo wa ujamaa mkongwe iliegemea upande wa kutetea maslahi ya walio wengi katika jamii. Baadhi ya wasanii walitukuza historia ya jamii walimoishi. Wengine waliwasifu watawala wao. Wengine walivisifu vipawa vyao vya kuhifadhi mapokeo ya jamii zao.

Msikilize Kouyate anavyojisifu katika utangulizi wa Utendi wa Sundiata: An Epic of Old Mali (1960).

> Mimi ni shaha au manju. Mimi ndimi
> Djeli Mamoud Kouyate mwana
> wa Bintou Kouyate na Djeli Kedian
> Kouyate, hodari katika sanaa
> ya kuzungusha ulimi. Tangu
> zamani za kale sisi wana mbari
> wa Kouyate tumekuwa tukiutumikia
> ufalme wa Keita na Mali. Sisi
> ni vyombo vya uzungumzi, ndiswi
> maghala yanayohifadhi siri za
> karne nyingi. Sanaa ya
> kuzungumza haina siri kwetu;
> bila sisi majina ya wafalme
> yangepotelea katika usahaulifu;
> sisi ni kumbukumbu ya wanadamu;
> kutokana na maneno yetu, sisi
> hupulizia uhai matukio na mafanikio
> yaliyopita mbele ya macho ya
> vizazi vichanga.
> Ujuzi wangu niliupata kutoka
> Kwa babangu Djeli Kedian, ambaye
> pia aliupata kutoka kwa babake,
> historia haina miujiza kwetu;
> tunawafundisha na hata makabwela
> kulingana na utashi wetu, kwa
> kuwa sisi ndisi tunaoweka
> funguo kumi na mbili za
> milango ya Mali. Najua majina
> ya wafalme wote waliorithi
> kiti cha enzi cha Mali.
> Najua jinsi watu weusi
> walivyogawika katika makabila
> mbalimbali kwa sababu

Complete Documents
Expanded Features

babangu alinirithisha ujuzi
wake wote. Neno langu ni
safi na halina doa la urongo,
ni neno la baba, ni neno
la baba wa baba. Nitakupa
neno la baba kama nilivyolipokea.
Wanahistoria wa kifalme hawa __
fahamu nini maana ya kusema
urongo .. Sikilizeni neno langu,
enyi nyote mnaotaka kujua
kwa kuwa kutokana na mdomo
wangu mtafahamu historia ya
Mali. (Tafsiri yetu, uk wa 24 dondoo
Kutoka Nandwa, J. & Bukenya).

Tumeinukuu sehemu hii ya Utendi wa Sundiata kwa mapana kwa sababu inachangia kwa kiasi kikubwa mjadala tunaouendeleza sasa. Kwanza, inatufahamisha baadhi ya majukumu ya wanasanaa wa kijadi. Pili, inatueleza njia moja miongoni mwa nyingine, zilizotumiwa kuwatayarisha wanasanaa hawa kutunga tungo zao. Kutokana na dondoo hili, tunagundua ya kwamba Djeli Kouyate ni mwaguzi, mwanahistoria, mwanasheria, mwanasiasa, mwalimu na mburudishaji (angalia Nandwa na Bukenya, 1983:24). Juu ya haya, kutokana na kujigamba kishairi kwa Djeli Kouyate, tunajulishwa kwamba alipata ujuzi wake kupitia katika mapokeo.

| |
|---|
| Fafanua dhima ya msanii katika jamii za kijadi. |

Basi hii ni moja kati ya njia zilizotumiwa kuwaandaa wanasanaa wa jadi katika wajibu mgumu wa kutunga tungo zao. Mfano wa Djeli Kouyate unathibitisha kuwa utunzi katika fasihi simulizi ulifanywa katika mipaka iliyokubalika na iliyozozewa na wengi. Hii haina maana kwamba msanii hangeweza kuusawiri umbuji wake wa kibinafsi. Linalosemwa hapa ni kwamba msanii hakutazamiwa kukiuka kaida zilizoabudiwa na sehemu kubwa ya jamii yake. Tuna maana gani tunaposema hivi?

Complete Documents
Expanded Features

Jambo hili linaelezwa kwa kindani na Jan Vansina (1985) anaposema kwamba kila maigizo yaonyeshwayo ni mapya na kila utambaji wa hadithi ni mpya kwa vile ambavyo katika hali halisi hakuna mtambaji wala mwigizaji anayeweza kukirudia kitendo kile kile alichokifanya hapo awali. Hata hivyo, Vansina, (1985), anasisitiza kwamba kila hadithi inayosimuliwa, kila wimbo unaoimbwa na kila maigizo yanayoigizwa ni thibitisho la kuwepo mapokeo maalum yaliyo hai na yanayorejelewa kila kukicha yaani usanii katika fasihi simulizi huelea baina ya mapokeo yaliyozozewa na ubinafsi wa mwanasanaa fulani.

Hii ndio sababu inayofanya ngano zenye mianzo, mitiririko ya vitushi na hata miisho ile ile kupewa sura tofauti tofauti na wanasanaa mbalimbali. Kuna wasimulizi wazuri waiozidhibiti njia za kuzipulizia hadithi uhai – njia kama kidatu, uigaji na ushirikishaji wa hadhira katika masimulizi yao. Kuna wengine ambao masimulizi yao hayana mwanzo wala mwisho na huichosha hadhira wakati wote wa kusimulia hadithi zao. Jambo hili laweza kutokea miongoni mwa wasimulizi ijapokuwa wanahadithia ngano moja tu.

## MWANASANAA WA KUIMBA

Tumeonyesha jinsi tanzu za fasihi simulizi zinazosimuliwa zinavyofundishwa na kuwasilishwa. Mwanasanaa wa wimbo naye huendelezaje kipawa chake? Kulingana na maoni ya Albert Lord (1960), mwana sanaa huyu hufuata vidokezo vifuatavyo kuutunga na kuimba wimbo wake.

(I) Kwanza mwanasanaa hutafuta tukio ambalo anataka kutunga wimbo juu yake. Mara nyingine mwimbaji hutafutwa na tukio la kuimbwa, akawa analazimika na muktadha anamopatikana kuanza kuimba. Anaweza kuwa katika sherehe za arusi au mazishi ambapo atachota malighafi ya utungo wake hapo hapo. Hivyo mwimbaji huweza kuimba mara tu mazingira yanayopalilia hali ya kuimba yanapotokea.

(II) Ikiwa mwimbaji atalazimika kutafuta tukio

Complete Documents
Expanded Features

ambalo ataka kutunga wimbo juu yake, jambo litakalofuata ni kujitafutia mikarara. Mikarara huujenga wimbo kimuundo na vilevile hulikuza tukio kwa upande wa dhamira. Hatimaye, mikarara huuweka wimbo katika mahadhi ya kuweza kuimbwa.

(III) Lord anasema kwamba mwimbaji hasitisiti wala kurudi nyuma pindi tu anapoanza kuimba. Hufululiza mbele hadi wimbo wake unapokwisha. Mfululizo huu unatokana na mazoea yake ya kuyahusisha mambo mbalimbali kwa haraka na kwa mdundo maalumu. Na ni mdundo huu, ngoma na vituo ndivyo humsaidia kupumua na kutafuta maneno mengine wakati wimbo unaendelea kuimbwa. Kumbuka kwamba hata nyimbo zinazoimbwa katika rekodi za santuri na kanda za kunasia sauti zina midundo ya aina hii.

> Jadili namna nyinginezo wanazotumia Wanasanaa kutunga tungo mbalimbali.

**UTUNGAJI WA FASIHI SIMULIZI NA USASA**

> Je, sasa una athari zozote juu ya fasihi simulizi?

Complete Documents
Expanded Features

Bado kuna watunzi wanaotumia mitindo mathalan ile tuliyokuwa tukijadili hapo juu kuwasilisha tungo zao. Hata hivyo, kwa sababu ya uvumbuzi wa kisayansi ambao umetokea katika jamii, kuna baadhi ya wasanii ambao hutunga tungo zao, halafu wanaziandika au wanazinasa katika kanda za kunasia sauti na kuziwasilisha baadaye.

## Je tutaiita aina hii ya utunzi fasihi simulizi?

Kila mwanafunzi wa fasihi simulizi ana maoni yake juu ya swali hili. Kuna wale watakaokubaliana na hoja hii na wengine ambao hawatakubaliana nayo asilani. Maoni ya kila mmoja yatalingana na ushahidi atakaorejelea. Kwa wakati huu tutatoa maoni yetu na kisha tuendelee na somo hili.

Fasihi simulizi hutungwa kwa ajili ya kushirikishwa kwa dhati kwa hadhira fulani. Ikiwa mambo fulani yataandikwa, lakini yatambwe katika hali halisi inayofungamana na udhati wa maisha, basi hayo yatakuwa sehemu ya fasihi simulizi. Uandishi na unasaji wa sauti zitakuwa nyenzo za kurahisisha ukumbusho. Hivyo, uandishi na unasaji wa sauti utashabihi vikale na mikarara iliyorahisisha ukumbusho zamani za kale, kabla ya uandishi na unasaji wa sauti kuvumbuliwa.

Tuseme kwa mfano, kikundi cha wanamziki cha Les Wanyika kinaonyesha Pamela . Bila shaka maonyesho yao yatabadilika kutegemea hadhira zao mbalimbali. Sababu ni kuwa hawatatoa na hawawezi kutoa maonyesho yao yote sarafu kwa nyingine. Lakini hii haimaanishi kwamba hawajaandika muziki wao angalau kwa ajili ya kujikumbusha mikarara yake tu. Kwa upande mwingine ikiwa kinasa sauti kitatumiwa kuunasa muziki halafu kiwe ndicho chombo cha kutoa huo muziki, basi muziki huo hautakuwa sehemu ya fasihi simulizi. Utakuwa umekengeuka kutokana na uhalisi na hautazungumzia hadhira maalum kwa zamu. Utakuwa kama neno lililoandikwa ambalo halijisemei wala kujitetea kila linapoulizwa swali na msomaji. Fasihi simulizi ina uhai zaidi ya hivi (angalia Plato The Phaedrus , 1952)

PDF Complete
Expanded Features
Unlimited Pages

**MAREJELEO**

Kabira M. W. (1983) The Oral Artist Nairobi: Heinneman. Kenya

Kirumbi P. S. (1975) Misingi ya Fasihi Simulizi Nairobi: Shungwaya

Lord Albert (1960) The singer of Tales Cambridge: Havard University Press

Nandwa J & Bukenya A. (1983) African Oral literature for schools Nairobi: Longman, Kenya

Niane D. T. (1979) Sundiata: An Epic of Old Mali. London: Longman Drumbeat

Plato (1952) The Phaedrus (Trans. With Introduction and Commentary by H. Hackforth) Cambridge: Cambridge University Press.

Vansina , Jan (1985) Oral Tradition as History Nairobi: Heinneman Kenya

## UHAKIKI KATIKA FASIHI SIMULIZI

Baada ya sehemu hii ya mshiriki anatarajiwa:

(a) Kufafanua maana ya uhakiki kwa ujumla

(b) Kueleza jinsi uhakiki hufanywa na ulivyokuwa ukifanywa katika muktadha wa fasihi simulizi.

Neno uhakiki lina maana mbili katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Maana ya kwanza ni:

(i) Upataji wa hakika au ukweli wa jambo. Nayo maana ya pili inasema:

(ii) Maelezo yanayochambua maandishi kwa kufafanua mambo mbali mbali yaliyomo. Kwa mujibu wa mahitaji mhadhara huu, maana ya pili inakaribiana zaidi na jambo tunalotaka kuzungumzia. Ikiwa tutaihusisha maana hii ya pili na fasihi, basi uhakiki wa fasihi utakuwa maelezo yanayochambua maandishi kwa kufafanua mambo mbali mbali yaliyomo. Kielezi hiki kina upungufu kwa kuwa hakitilii maanani nafasi ya fasihi simulizi. Kinachukulia kuwa kuna fasihi andishi peke yake; fasihi simulizi inapuuzwa. Ili kuihusisha fasihi simulizi moja kwa moja na kielezi hiki, tutaelezea uhakiki wa fasihi hivi:

Uhakiki wa fasihi ni maelezo

yaliyoandikwa au yaliyozungumzwa
yanayo chambua tanzu mbali mbali

Complete Documents
Expanded Features

za fasihi – fasihi andishi au
fasihi simulizi.

Uhakiki hudhamiria kuieleza, kupima, kuifafanua na kuichunguza kazi ya fasihi. Uhakiki unapaswa kuifanya matini inayosomwa na inayotambwa kusisimua. Pia uhakiki unatarajiwa na kuhimiza ufahamu wa kazi ya fasihi ili kumfanya mshiriki kutilia maanani baadhi ya mambo ambayo pengine hayangetiliwa maanani.

Nini maana ya neno Uhakiki na
uhakiki wa fasihi ?
Jadili shabaha za uhakiki wa fasihi

## UHAKIKI KATIKA FASIHI SIMULIZI

Uhakiki katika fasihi simulizi si jambo jipya, ni mkongwe. Katika desturi za waswahili, uhakiki ulifanywa wakati washairi walipokuwa wakipingana na kuchokozana huku wakichambuliana mashairi. Haya ni maoni ya Shihabuddin Chiragdin (Nassir, 1970).

Chiragdin anazianisha namna tatu za kufanya uhakiki katika jamii ya Waswahli. Anasema kwamba huko Pemba, wangoi waliingia kwa kufuatishana na kutongoa tungo zao. Kazi ya wasikilizaji ilikuwa ni kumteua mngoi aliyemakinika zaidi katika matumizi ya lugha. Hii ina maana kwamba wanasanaa hodari wangeweza kujulikana kutokana na wanagenzi.

Kisha Chiragdin anaitalii pwani ya Kenya. Utafiti wake unaonyesha kwamba Wamvita wana desturi ya kufunga nyama . Desturi hii huwashirikisha wahusika wawili wakuu ambao hawaonani na pengine hawajuani. Malenga wa kwanza atafunga nyama . Kwa mujibu wa maelezo ya Chiragdin kufunga nyama kuna maana ya kufumba fumbo. Malenga wa pili akiuliza kwa ushairi mpaka amfungue nyama yaani alifumbue hilo fumbo na pengine amtambue huyo mfumbaji pia.

Complete Documents
Expanded Features

Hatimaye, Shihabuddin Chiragdin anasema kwamba huko Tanzania kuna ngonjera ambapo watu wawili husailiana na kujibizana kwa ushairi katika magoma mbalimbali. Baadhi ya magoma haya ni:

(i) Diriji – Hii ni ngoma inayochezwa na wanaume kwa bakora au/ na panga.

(ii) Lelemama – ni ngoma ya wanawake inayochezwa juu ya mabao na kwa kutumia mbiu.

(iii) Tari – aina mojawapo ya ngoma inayopigwa kwa kutumia matari.[1]

Kutokana na mitaala ya Shihabuddin Chiragdin, tunaona kwamba katika jamii ya Waswahili, uhakiki ulifanywa hapo hapo katika hali ya kutunga na kuwasilisha tungo za kisanaa.

Mawazo ya Shihabuddin Chiragdin yanafanana na yale ya Abiola Irele (1981). Katika jamii za Kiafrika na zisizokuwa na mapokeo ya uandishi, jinsi ya kuzitathmini kazi za sanaa kulihitamidiwa kutokana na njia za kuzitunga kazi hizo, katika hali ya kuziwasilisha. Mafanikio ya msanii yalitegemea ridhaa ya hadhira yake. Ikiwa washiriki wataisifu kazi ya fasihi basi kazi hiyo itakuwa imefaulu. Kwa upande mwingine kama washiriki hawataridhishwa na tungo za sanaa fulani, basi tungo hizo hazijafaulu. Vigezo vya kuchuja sanaa vilijulikana kimapokeo na wanajamii walivitambua mara moja pasi kuambiwa. Hivyo ndivyo uhakiki ulivyofanywa katika jamii zisizokuwa na mapokeo ya uandishi.

## DHIMA YA MHAKIKI KATIKA FASIHI SIMULIZI

Katika Mulika Namba 12 (1978: 2 – 6), A. G. Gibbe anajadili kuhusu dhima ya mhakiki wa fasihi. Maoni yake kumhusu mhakiki ni yafuatayo:

> Mhakiki hujishughulisha na maandishi ya waandishi
> asilia, yeye husoma kwa undani maandishi yao
> na kuyatafakari na kuandika makala au vitabu kuhusu

[1] Angalia utangulizi wa Malenga wa Mvita, uk. Wa 7-9 kwa ufafanuzi zaidi.

Complete Documents
Expanded Features

maandishi .. makala ya mwandishi mwenye uelekeo
wa kimapinduzi huwa ni chombo madhubuti cha mapinduzi
(uk. 2).

Anamaliza kwa kusema kwamba lengo kuu la mhakiki ni kuonyesha akina nani maandishi yanayowahusu na maadishi hayo ni ya kiwango kipi katika maendeleo ya jamii.

Maelezo ya Gibbe yana matatizo mawili:

(i) Gibbe mwenyewe amekolewa kabisa na mtazamo wa kijamaa juu ya maisha. Anatoa mawazo yake kwa mwelekeo wa itikadi ya kijamaa. Hakuna ubaya katika mwandishi kuonyesha msimamo wake juu ya mambo tofauti tofauti yanayopatikana katika mazingira yaliyomzunguka. Hata hivyo, Gibbe anapuuza dhima za wahakiki wengine wasiokuwa wanajamaa . Anawagusia lakini hawasawiri kwa mapana ya kutosha. Dhamira yake ni kuwaonyesha kama watu wanaopuuza wajibu wao ilhali wanafahamu kwamba kitendo hiki ni usaliti dhidi ya jamii zao. Ukweli ni kwamba unyonyaji na unyanyasaji wa umma hurutubishwa pia na wahakiki hususa wale wasiokuwa wa kimapinduzi. Yafaa na wao pia wazungumziwe kwa marefu. Kile anachoishilia kukifanya Gibbe si kutueleza dhima ya mhakiki bali kuorodhesha baadhi ya maelekezo anayopaswa kuyafuata mhakiki wa kimapinduzi.

(ii) Tatizo la pili linalotokana na tahakiki ya A. G. Gibbe ni kwamba anapozungumzia dhima ya mhakiki, hashughulikii fasihi simulizi asilani.

Kwake, fasihi simulizi haipo na kama ipo, inaendelea kudidimia na kusahaulika.

| |
|---|
| Nini dhima ya mhakiki wa fasihi kwa ujumla? |

Complete Documents
Expanded Features

Dhima ya mhakiki kwa ujumla inaweza kuhitamidiwa kutokana na dhima ya uhakiki. Jukumu la mhakiki ni kuhakiki. Mhakiki ndiye mtendaji katika kazi uhakiki. Kazi anayofanyia matini ya fasihi, fasihi simulizi kwa andishi ni dhima yake.

| |
|---|
| Utunzi na uhakiki ni mambo yanayofanana katika fasihi simulizi . Jadili |

Wajibu wa mhakiki wa fasihi simulizi ulikuwa kusambaza itikadi ama ya watawala au itikadi iliyoonelewa na wengi kuwa ndiyo iliyowafaa. Majisifu ya Kouyate (mhadhara wa saba yatakuzindulia ukweli kwamba yeye kama mtunzi na mhakiki alikuwa na wajibu kwa wote, wafalme na makabwela. Ni kejeli kwamba Kouyate anajaribu sana kujinasibisha na nasaba ya kifalme ijapokuwa yeye anatokana na nasaba ya mafelahi. Huku kuunganishwa kwa sifa mbili zisizotangamana kunamfanya Kouyate kuwasemea wanajamii wote.

Kutokana na wajibu wa mhakiki mwenyewe, ama alisifiwa ama kukemewa kijumla kufungamana na imani ya mafunzo waliyopata wanajamii kupitia katika mapokeo yao. Jambo la pili linalojitokeza katika mazungumzo yetu kuhusu fasihi simulizi ni kwamba mtunzi alijifunza vigezo vya kuzitathmini kazi zake katika harakati zake za kutunga. Lengo lake muhimu lilikuwa kutunga tungo zilizoafikiana na kaida za jamii yake. Kwa kiwango hiki mtunzi alikuwa mhakiki wakati huo huo alipokuwa akitunga. Mwandishi hakujitungia; aliwatungia wengine na nia yake ilikuwa kufikia ukamilifu ulioabudiwa na jamii. Hata hivyo, alibadilisha mikakati ya kuwasilisha tungo zake kila ilipohitaji (Kabira, 1983: 1 – 4).

Expanded Features
Complete Documents

## MAREJELEO

Gibbe G. A. (1978) Dhima ya Mhakiki katika Mulika Namba 12 Dar es Salaam: Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Hough Graham (1966) An Essay on Criticism. London. Duckworth.

Kabira W. M. (1983) The oral Artist. Nairobi: Heinemann Kenya Limited.

Nazareth, Peter (1972) Literature and Society in Modern Africa. Nairobi: East African Literature Bureau.

(1978) The Third World Writer: His Social Responsibility. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Irele, Abiola (1981) The African Experience in Literature and Ideology. London: Heinneman Educational Books.

(2006) Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Nassir Ahmad (1970) Malenga wa Mvita Nairobi: Oxford University Press.

## MHADHARA WA NANE

## UTAFITI KATIKA FASIHI SIMULIZI

Baada ya mhadhara huu utaweza:

(a) Kufafanua maana ya neno utafiti .
(b) Kueleza historia fupi ya utafiti katika bara la Afrika.
(c) Kuorodhesha vifaa vinavyopaswa kuwepo ili utafiti muafaka utimizwe.
(d) Kueleza manufaa ya utafiti.

Kulingana na ufafanuzi wa A Standard English – Kiswahili Dictionary, maana ya neno utafiti ni uchunguzi, ni upelelezi au ni utafutaji wenye nia ya kuvumbua habari ngeni. Nayo Kamusi ya Kiswahili Sanifu inaueleza utafiti kuwa udadisi wa hali ya juu . Maana inayoelezwa na Kamusi ya Kiswahili Sanifu inafaa zaidi. Sababu ni kuwa inafungamana na neno utafiti kitaalamu. M. M. Mulokozi ametoa historia fupi juu ya utafiti wa fasihi simulizi. Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kiswahili (1983), mhakiki huyu

Complete Documents
Expanded Features

anaonyesha kwamba lengo la utafiti huathiriwa na itikadi ya mdhamini wa mtafiti fulani. Aghalabu, mdhamini hutaka utafiti unaofanywa kuridhisha mapendekezo na mapendeleo yake.

| |
|---|
| Jadili maoni ya watafiti weupe juu ya bara la Afrika katika karne ya kumi na tisa |

Jambo hili laelekea kuwa kweli hususa tukizingatia kipindi cha ukoloni. Kwa miaka mingi, utafiti wa nyanja mbalimbali za maisha ya Mwafrika ulielekezwa kwa nia na kwa sababu zisizokuwa na mantiki. Unaweza kukumbuka visa asili vyovyote vinavyochukiza juu ya utu wa Mwafrika?

Mulokozi anadondoa ithibati nyingi kudhihirisha kwamba utu wa Mwafrika haukuthaminiwa kwa lolote lile. Chambilecho mwandishi Frantz Fanon, Mwafrika alichukuliwa kuwa kinyume cha ubinadamu na utubora. Maoni makali sana yanayothibitisha madai haya yamedondolewa na Mulokozi (1983) kutoka kwa maandishi ya G. F. Hegel alipokuwa akiandika historia ya ulimwengu. Ijapokuwa Mulokozi ameitoa tafsiri yake ya Hegel, nasi pia tumewajibika kuitoa yetu. Hegel anasema:

> Afrika halisi, yaani Afrika
> Kusini ya jangwa la Sahara
> Haijaingiliana wala kuhusiana
> historia kwa lolote lile na
> sehemu nyingine za ulimwengu.
> Afrika ni kama nyumba iliyojifunga
> kwa ndani na kujisahaulisha
> kusijulikane chochote kilichomo.
> Afrika ni eneo lililozaliwa
> juzi inayobarizi nje ya
> mipaka ya historia inayofahamiwa na
> kujulikana.
> Ni eneo ambalo limefunikwa
> gubigubi kwa giza totoro,
> giza la usiku. Na ijapokuwa
> Mwafrika bado anaishi porini
> na hawezi kamwe kufugwa,
> anawasiri kwa mbali ishara

Expanded Features
Complete Documents

za kibinadamu kama tunavyozifahamu.
Hata hivyo, huwezi kutarajia ustaarabu
wa aina yoyote kutokana na
kiumbe cha aina hii.

Kwa hayo, tunaliacha bara
la Afrika na hatutalitaja tena
daima dawamu. Afrika si sehemu ya
ulimwengu kihistoria. Kile tunachofahamu
kuwa Afrika ni roho ambayo
ni mtovu wa historia, iliyokwama
katika tope la uasili na ambayo
haijabadilika wala kukua tangu
hapo na uumbaji.

Tumegusia Afrika hapa
kusawiri angalau kwa
kifupi sura ya ulimwengu
ulivyokuwa kabla athari zozote za
kihistoria kutokea. Historia ya
ulimwengu husonga – ikitokea
Mashariki ikielekea Magharibi.
Uropa ni mwisho wa kihistoria;
Asia chanzo chake.
(Tafsiri yetu, uk. 178 Kamenju
katika Zirimu & Andrew Gurr).

Utafiti wa mwanzo kumhusu Mwafrika katika vipengele vyake vyote ulielekezwa na maoni kama haya. Fasihi simulizi ya Kiafrika ilianza kushughulikiwa tangu mwaka wa 1850. Hapo ndipo watumishi wa kwanza wa serikali za kikoloni walipoanza kuzungumzia utamaduni wa Mwafrika. Hii ina maana kwamba fasihi simulizi ya Waafrika ilitajwa bila kutarajia. Iliangaliwa kama sehemu ya utamaduni wa Mwafrika. Tokea miaka ya 1930, Waafrika wengi walianza kuzungumzia mambo yaliyohusu utamaduni wao. Walipewa motisha wa kuzungumzia utamaduni wao kutokana na uzindishi wa Uafrika, na pia kutokana na mwamko wa utaifa. Baada ya uhuru kupatikana, somo la fasihi simulizi lilianza kushughulikiwa kwa mapana zaidi. Waandishi kama Ruth Finnegan, Rose Mwangi, Taban Lo Liyong, Okot p Bitek, J. Nandwa, A. Bukenya, B.M. Lusweti, N. Kipury na Wanjiku Kabira walijitokeza. Huko Tanzania Marehemu Bi. Matteru amaeishughulikia fasihi hii sana. Afrika ya Magharibi nayo imezaa vigogo kama

Complete Documents Expanded Features

Ben Dan Amos, Bascom na Isidore Okpewho. Kwa wakati huu kuna watafiti wengi wa fasihi simulizi wageni kwa wenyeji. Mara nyingi watafiti hawa hutumia njia za kimseto kutafitia fasihi simulizi. Na wageni si lazima wawe watu weupe. Wanaweza kuwa Waafrika wanaotoka maeneo tofauti na yale yanayotafitiwa.

Licha ya kwamba mtafiti anaweza kwenda uwanjani na kutumia ama njia za wenyeji au njia za kigeni au mchangamano wa zote kutafiti, mtafiti huyo anatazamiwa kuingiliana na wanajamii wa fasihi anayotalii. Nao utafiti si ukusanyaji wa data tu; utafiti unapaswa kuchochewa na udadisi fulani kwa upande wa mtafiti. Kutokana na udadisi huu, mtafiti anaweza kuwahoji wanajamii wa jamii inayohusika. Mtafiti anaweza kutumia hojaji. Hojaji ni orodha ya maswali yanayoulizwa na mtafiti.

Eleza hatua za maendeleo zilizopigwa katika utafiti wa fasihi simulizi tangu kupatikane uhuru katika jamii za Afrika Mashariki?

Aghalabu, hojaji hutumiwa kukusanya maoni ya watu waliosoma. Maswali ya hojaji yana nafasi ya kuandikia majibu kwenye karatasi. Lakini mtafiti anaweza vilevile kutumia hojaji bila kuandika na kusambaza maswali kwenye karatasi.

Inapasa mtafiti awafahamishe wahojiwa mapema kwamba atawahoji. Kama hafanyi hivyo, huenda akashukiwa kuwa ama mdakuzi au mpelelezi wa siri. Njia nyingine ya kutafitia ni kukutana na watu wanaolifahamu jambo analolitafuta mtafiti na kuzungumza nao. Katika kule kuzungumza mtafiti anaweza kupata jambo litakalomsaidia.

Jadili manufaa na upungufu wa njia mbalimbali za kukusanya data katika fasihi simulizi.

Expanded Features
Complete Documents

Pia, mtafiti anaweza kupata data kwa kushiriki katika sherehe mbalimbali na kujionea yale yanayotendeka. Hatimaye, mtafiti anaweza kuzungumzia jambo lolote kuhusu sherehe hizo kutokana na msimamo wake. Namna ya kukusanya data kutategemea lengo la utafiti na jinsi utafiti ule unavyopaswa kutumiwa. Lakini kutumia njia hizi zote au baadhi ya njia hizi kukusanya data hakuufanyi utafiti kuwa yakini. Ili ujuzi wa fasihi simulizi ukubalike kuwa kweli, unapaswa kuthibitiwa kisayansi.

| |
|---|
| Orodhesha na ujadili hatua zinazofuatwa katika kuthibitisha ujuzi wa kisayansi. |

K. S. Goldstein katika kitabu cha A Guide For Fieldworkers in Folklore (1964) anasema kwamba utafiti wa kisayansi hufuata hatua zifuatazo:

(i) Lazima kuwa na tatizo analotaka kulitatua mtafiti. Tatizo hili huitwa kisio,haipothesia au nadharia tete. Haipothesia ni jambo linalokubaliwa ijapokuwa halikuthibitishwa. Lengo la utafiti huwa ni kuyakinisha ukweli wa hypothesia. Hypothesia humwongoza mtafiti katika kuvibainisha vifaa vinavyohitajika na data zinazopaswa kuwepo ili utafiti wake ukamilike.

(ii) Hatua ya pili inahusiana na ya kwanza, nayo ni kutafuta data muafaka na vifaa vinavyosaidia kuziwasilisha data hizo kutegemea aina ya utafiti unaofanywa. Mtafiti anaweza kuhitaji kalamu, karatasi, kinasa – sauti, tepu video, kamera, kamera za sinema, mkalimani na kadhalika (angalia Mulokozi, 1983 katika marejeleo).

(iii) Sehemu ya tatu ni ya ukusanyaji wa data. Data zinaweza kukusanywa kwa kutumia baadhi ya njia tulizozungumzia.

(iv) Hatua ya nne inahusu uwasilishaji data. Data hizo zinaweza kuwasilisha kwa njia mbili kulingana na jinsi utafiti ulivyofanywa.

(a) Pengine matini itatafsiriwa neno kwa neno na baadaye kutafsiriwa kufungamana na maana iliyokusudiwa katika lugha asilia.

(b) Data zinaweza kuwasilishwa moja kwa moja kulingana na lugha asilia ya mtafiti.

Expanded Features
Complete Documents

(v) Baada ya uwasilishaji wa data kufanywa, uchambuzi wa hiyo data hufuata. Katika fasihi simulizi, yaliyomo na jinsi yanavyowasilishwa ni baadhi ya mambo yanayozingatiwa. Mambo mengine kama vile mandhari na sherehe pia yanahitaji kutiliwa maanani.

(vi) Ulinganishaji wa makisio ya mwanzo na matokeo ya uchambuzi wa data ni hatua ya mwisho ya kudhihirisha ujuzi wa kisayansi. Kutokana na ulinganishaji, huenda makisio ya mwanzo yayakinishwe kuwa sahihi. Inawezekana pia kwa makisio au kurebishwa au kufutiliwa mbali. Ikitokea kwamba makisio ya awali yamefutiliwa mbali, tasnifu mpya zitaibuka kutokana na haipothesia zilizothibitishwa na uchunguzi wa kweli.

Onyo: Mtafiti anapaswa kukumbuka kwamba ili utafiti wake uzalishe matokeo yanayotegemewa, anapaswa kufahamu mazingira yote yanayozunguka mahali anapopafanyia utafiti wake na majaribio yake. Jambo hili litamwezesha kuainisha na kuzuia kadhia zinazoweza kuuingilia utafiti na kusababisha matokeo yasiyokuwa ya kweli kupatikana.

> Tofauti kuu iliyopo baina ya methali na kitendawili ni kwamba kitendawili ni fumbo ilhali methali si fumbo. Tafiti tahadhania hii na uonyeshe kama inasheheni ukweli wowote.

## MATATIZO YANAYOWEZA KUMKABILI MTAFITI

Kuna matatizo mengi yanayoweza kumkabili mtafiti ya fasihi simulizi G. Kubik (1977) anaainisha matano:

(i) Inawezekana kwamba mtafiti haelewi lugha inayosheheni tatizo analotafiti juu yake. Hivyo basi, atategemea mambo ya kuambiwa, mengine ambayo yatakuwa yamepotoshwa.

(ii) Ni vigumu kupata miktadha inayochukuana vizuri na tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Kwa mfano, nyimbo za matanga huimbwa vizuri zaidi wakati mtu ameaga dunia. Haziwezi kuimbwa ovyo ovyo. Na muktadha wa matanga huenda usimsaidie mtafiti vizuri. Fikiria jinsi utakavyochukuliwa na watu wengine ikiwa wakati wakiomboleza,

Expanded Features
Complete Documents

wewe utakuwa ukitembea huku na huko na kinasa – sauti chako .
Ama sijui . Kamera ya sinema yako. Utachukuliwa kuwa mchawi.

(iii) Ushirikina ni tatizo jingine. Mtafiti anaweza kufikiria kwamba atalogwa na watu ambao jamii inatafitiwa. Na jamii ambayo fasihi yake inatafitiwa inaweza kumshuku mtafiti hasa iwapo huyo mtafiti ni mgeni. Mgeni anaweza kufikiriwa anataka kujua siri zetu ili atuloge .

(iv) Tatizo lingine linaloweza kumkumba mtafiti ni mapendeleo. Mapendeleo yanaweza kuzuka pale ambapo mtafiti atadanganywa kuhusu asiyojua juu ya fasihi simulizi ya jamii fulani.

| |
|---|
| Kwa kutoa mifano inayofaa, jadili matatizo yanayoweza kumkabili mtafiti katika fasihi simulizi, anapotafiti hapa uwanjani. |

Pia ikiwa mtafiti anatafiti juu ya jamii yake mwenyewe, kuna mambo atakayoyapuuza kwa kuwa hayaathiri matokeo ya utafiti wake. Mengine yatapuuzwa kwa sababu yanaeleweka . Haya ni mapendeleo.

(v) Tafsiri za matini ndilo tatizo la mwisho tatakalozungumzia hapa. Iwapo hata data zinazowasilishwa zitatafsiriwa, mtafiti atakuwa na shida ya kupata msamiati utakaowasilisha dhana zote kwa usawa kutoka lugha changizi hadi lugha pokezi.

## MANUFAA YA KUFANYA UTAFITI KATIKA FASIHI SIMULIZI

(i) Kusahihisha mielekeo mibaya kuhusu fasihi simulizi ya Kiafrika na utamaduni wa Mwafrika kwa jumla.
(ii) Kufahamu mambo yanayopatikana katika fasihi simulizi ya Mwafrika kwa njia ya utaalamu.
(iii) Kuchanganua data tunazopata na kuhitamidi ukweli unaohusu maisha yetu kutokana nazo.
(iv) Kuelewa matatizo ya nyanjani yanayowakabili watafiti.

## MAREJELEO

Fanon, Frantz (1963) The Wretched of the Earth (Transconstance Farrington) New York: Grove Press Inc.

Goldstein, S. K. (1964) A Guide for Fieldworkers in Folklore Hatboro: Folklore Associates Inc.

PDF Complete
Expanded Features
Unlimited Pages

Kubik, G. (1977) Recording and classification of Oral Literature in TanzaniaDar es Salaam: Goethe Institute.

Mulokozi M. M. (1983) Utafiti wa Fasihi Simulizi katika Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili. 111: Fasihi Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu Dar es salaam.

Nandwa J. & Austin Bukenya (1983) African Oral Literature For Schools. Nairobi: Longman Kenya Limited.

Zirimu & Andrew Gurr (1971) Black Aesthetics: Papers from a Colloquim held at the University of Nairobi: Nairobi: East African Literature Bureau.

## SEHEMU YA PILI

Hii ni sehemu ya pili ya mfululizo wa mihadhara inayoshughulikia fasihi simulizi. Katika sehemu ya kwanza, tulizungumza kuhusu fasihi simulizi kinadharia. Sehemu hii inalenga kuelezea na kuchanganua tanzu mbalimbali za fasihi simulizi.

Mihadhara saba ya kwanza inatalii tanzu za kinathari au za kihadithi. Nayo mihadhara ya mwisho inahusu tanzu za kishairi na kidrama.

.

## MHADHARA WA KWANZA

## Tanzu za Fasihi Simulizi za Kihadithi

Baada ya mhadhara huu, utaweza:

(a) Kuainisha majina ya baadhi ya tanzu za Fasihi simulizi za kihadithi.

(b) Kuonyesha tofauti kuu zilizopo baina ya tanzu za kishairi na tanzu za kihadithi za fasihi simulizi.

Complete Documents
Expanded Features

Kuna makundi mawili muhimu ya tanzu za fasihi simulizi. Kundi moja linahusu tanzu zenye mwelekeo wa kishairi na ilhali lingine linashughulikia tanzu za kinathari au zenye sifa za kihadithi.

Jadili tofauti kuu zilizopo baina ya tanzu za kishairi na tanzu za kihadithi za fasihi simulizi.

Tanzu za kishairi zina sifa nyingi za ushairi kuliko tanzu zenye lugha ya kinathari. Ushairi aghalabu hutumia lugha ya kitamathali na mkato. Pia, ushairi una mizani, ulinganifu wa sauti na mipigo.

Matteru (1987) amesema kwamba katika muktadha wa fasihi simulizi, ushairi ni fungu linalojumlisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia mapigo kwa utaratibu maalumu. Mapigo haya yanaweza kuwa ya kimuziki au yoyote yale yaliyopangwa kwa muwala wa uwazi. Tanzu kama nyimbo, maghani, methali, vitendawili, misimu hupatikana katika kundi hili la "ushairi".

Kwa upande mwingine, Matteru (1987) anasema kwamba tanzu za kinathari zinajumlisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia lugha ya kawaida ya maongezi, lugha ya mjazo. Kwa kawaida, mipigo ni huru na huambatana na mipigo iliyotumiwa katika lugha ya kawaida. Matteru anamalizia kwa kusema kwamba 'nathari' hujumlisha tanzu kama hadithi, ngano, tarihi, visaasili, vigano na masimulizi.

Pengine mifano michache ya tanzu za kishairi na tanzu za kihadithi za fasihi simulizi zitaonyesha ukweli wa tofauti hizi. E. Kezilahabi amedondoa wimbo ufuatao wa kumbembeleza mtoto wa Bibi Hafsa M. Ali ( Omari, et. Al 1980: 126-127):

1. Mama na baba katenda kunioza dume kongwe,
   Halisafiri halendi kazi kupiga matonge, Lakikaa
   mvunguni hunguruma kama ng'ombe.

2. Ukilea mwana mwema na mwana mui mlee,
   Mwema ukimpa chenga mui umpe chelele,

Complete Documents
Expanded Features

Hujui akufaaye akupaye maji mbele.

3. Msikiti wa Jibondo kandili mbili zawaka,
   Wamo wasomaji vyuo na waandikao nyaraka,
   Nyamba zote nimekula kasoro kia la paka.

4. Mwana nikatie kanga nimechoka msagunda,
   Kanga robo ya thamani si kitu cha kukushinda,
   Makubwa siyatamani suruali za marinda.

5. Mama aliponizaa hakuniona mbaya,
   Kanipa chakula chema na nguo njema kuvaa,
   Kasoro kitu kimoja kunita mwana hizaya.

6. Kua mwanangu kua kua nikupe wasia,
   Nikupe kundi la ng'ombe la mbuzi unywe
   maziwa, Asiyeweza kuniumba hawezi kuniumbua

7. Karatasi nakupelekea kwa mfalme Hassani,
   Mwenyewe kanzu ya malota na fimbo ya henzerani,
   Makosa niliyokosa sina mwombezi kwani,
   Mwombezi wangu nyota, na baraka ya Ramadhani.

Katika wimbo huu mambo kadhaa yanajitokeza. Kuna mkarara na mapigo. Sifa hizi zimeukabidhi wimbo huu mdundo maalumu unaounasibisha zaidi na tanzu za ushairi kuliko tanzu za kinathari za fasihi simulizi.

Nao mfano unaofuata ( Mpungu, 1979: 25-29) ni wa utanzu wa kinathari.

## Kuchakulo na Nyani

Hapo kale, kuchakulo alikuwa akiishi mahali palipokuwa na nyani wengi. Nao hao nyani walikuwa wamezoea kumcheka kuchakulo kila alipopita karibu nao. Tabia hii ilimwudhi sana kuchakulo. Kwa muda, alikaa akifikiri njia ya kuwaadhibu nyani hawa.

Siku moja jawabu likamjia. Akaenda mpaka mwituni ambako alipata zabibu tamu sana; akazitia katika mfuko mmoja. Katika mfuko ule ule akatia changarawe. Akaenda moja kwa moja mpaka mahali nyani walipokuwa wamekaa kwa furaha. Akaingiza mkono wake mfukoni na kuzitoa zabibu. Akazitafuna na huku akisema: "Haa! Meno ya wavulana huzisaga hizi changarawe mpaka zikawa unga! Angalieni!"

Akazitoa zabibu na kuzitafuna.
Wale nyani kuona vile wakamwendea wakisema:
"Hebu tupe na sisi tuzisage kwa meno."

Expanded Features
Complete Documents

Kuchakulo akaingiza mkono mfukoni na badala ya kuzitoa zabibu akatoa changarawe na kuwapa. Nyani kujaribu kutafuna wakaumwa na meno na kuzitema chini. Kuchakulo akaendelea kuzitoa zabibu kwa akili na kuzitafuna. Hao nyani waliiona hiyo ajabu, wakamwuliza kile kinachomfanya yeye aweze kutafuna kwa urahisi bila kuyaharibu meno na wakati wao hawawezi.

Kuchakulo kwanza alicheka kisha akayatema mate chini na kuwaambia: "Msinichezee, mimi nimetahiri na ninyi bado. Meno ya mtu aliyetahiri ni magumu, na anaweza kutafuna hata mawe".

Akatoa zabibu tena, akizitafuna. Baru! Baru! Baru! Huku akiwaangalia nyani kwa dharau. Lo! Wale nyani wakashangaa sana. Wakaanza kuangaliana kisha wakamwuliza kuchakulo: "Sasa twambie tutafanyaje ili tuweze kutafuna zabibu kama wewe?"

Kuchakulo akawaambia: "Hakuna dawa nyingine ila kutahiri tu!"

Nyani wakamwambia awaletee ngariba wa kuwatahiri wawe kama yeye. Wakapanga siku ya kumleta huyo ngariba. Kuchakulo alimwendea chui na kumwambia: "Bwana chui, kila wakati nasikia wanitafuta uniue. Nikikupatia nyani uwafanye kitoweo chako utanifaa namna gani?"
Chui akamwambia: "Mimi hupenda sana nyama ya nyani na ukinipatia hata mmoja urafiki wetu utadumu."

Kuchakulo na Chui wakapanga mahali watakapokutana akiwa na wale nyani. Kuchakulo akawaendea nyani na kuwaambia: "Nimempata mtu hodari sana wa kutahiri na amekubali kufanya kazi hiyo bure ili awasaidie."

Nyani kusikia hawatalipa kitu wakafurahi sana wakawaendea wengine na kuwapasha habari. Siku ile iliyopangwa na Kuchakulo na Chui ikaonekana inawafaa vile vile.

Siku ilipofika Kuchakulo alimwendea Chui na kumwambia: "Nifuate".

Chui alimfuata mpaka mahali palipokuwa na pango lenye giza akaachwa ndani. Halafu, Kuchakulo aliwaendea Nyani na kuwaleta kwenye uwanja uliokuwa karibu na pango lile. Walipokwisha kujipanga, Kuchakulo akwaambia: "Mtakuwa mkija mmoja mmoja mpaka yule wa mwisho."

Kuchakulo akaenda tena ndani ya pango na kumwambia Chui ajiweke tayari. Ikawa kazi ya Kuchakulo ni kumpelekea mmoja mmoja akiimba wimbo huu:-

> "Vumilia, vumilia
> Huwezi kufa,
> Vumilia, vumilia
> Uondolewe utoto,
> Hakuna kulia au kufanya kelele
> Vumilia tu ufanywe mtu mzima."

Expanded Features
Complete Documents

Kufika pangoni nyani aliingia peke yake na Kuchakulo akaachwa mlangoni. Nyani alipofika ndani alimkuta Chui amejiweka tayari kumvunja shingo na kumtupa ndani kabisa mvunguni.

Mtindo huu uliendelea mpaka karibu kumfikia nyani wa mwisho. Kila wakati alipompeleka mmoja alikuwa akiimba wimbo ule wake. Walipokuwa wamebaki wawili tu wakamshuku Kuchakulo.

Mmoja akamwambia mwingine: “Wewe ukifika mlangoni uangalie vile wale wenzetu wanavyofanywa ili tujue yanayofanyika”.

Kuchakulo akaja tena na kumwambia: “Twende, unasitasita nini? Je, unaogopa?”

Yule nyani hakutaka kumwonyesha anashuku kitu. Kuchakulo akaanza: “Vumilia, vumilia, Huwezi kufa ……Heeeeeeeeeeeeeee! Huuuuuuuuuuu! Haraka twende!”

Yule Nyani kufika mlangoni akasimama, akainama na kuangalia ndani. Kwa mwangaza kidogo akamwona Chui mkubwa mwenye madoadoa ya manjano na meusi anamkodolea macho.

Kuangalia uvunguni akawaona wale wenzake wote wamelala wamekufa fo!fo!fo! Akaondoka mbio mpaka alimpomwacha mwenzake na wote wakatimua mbio wakatokomea msituni. Kuchakulo alijaribu kuwafukuza asiwapate. Akarudi kwa Chui. Chui akamshukuru sana akimpigapiga mgongoni na kumhakikishia kuwa urafiki wao utadumu.

Kuchakulo akamwacha Chui na mizoga ya Nyani na kurudi zake nyumbani.

Wale Nyani wawili ndio waliowazaa nyani tunaowaona siku hizi, na tangu siku ile hawajadhubutu kumcheka tena Kuchakulo.

Hapo kale, Kuchakulo alikuwa akiishi mahali palipokuwa na nyani wengi……….

Kutokana na mfano huu, tunaona kwamba hakuna mipigo inayojitokeza kwa utaratibu. Lakini mipigo ikibainika hapa na pale ni huru, isipokuwa kama wimbo umetumiwa kama ulivyo tumika katika hadithi ya “Kuchakulo na Nyani.”

## MAREJELEO

Kezilahabi, E. (1980) “Ushairi na Nyimbo katika Utamaduni Wetu” Katika Urithi wa Utamaduni Wetu ( Kilichohaririwa na C.K. Omari na M. Mvungi). Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Matteru, M.L.B ( 1987) “Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi” katika Mulika Namba 19. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Complete Documents
Expanded Features

Mpungu, E.B (1979) Mjinga na Mwerevu. Nairobi: Trans Africa
Senkoro, F.E.M. (1982) Fasihi. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

## MHADHARA WA PILI

### Ngano

Baada ya mhadhara huu, utaweza:

(a) Kubainisha aina mbalimbali za ngano na kuonyesha sifa zake muhimu.

(b) Kutathmini namna mbalimbali za kuziweka ngano katika makundi tofauti tofauti.

Kulingana na maelezo ya M.L.B Matteru, ngano ni "hadithi za paukwa pakawa----wakaishi raha mustarehe" ( Mulika 19, 1987). Maelezo haya yanakumbusha kwamba Matteru ametumia kigezo cha mianzo na miisho kuanisha ngano kutokana na tanzu zingine za fasihi simulizi.

Mara nyingi ngano zina nyimbo. Nyimbo hizo zina nyadhifa kadhaa. Zinaweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu wa ngano inayosimuliwa. Zinaweza kutumiwa kubadilili nadhari ya wahusika kutoka kwa shughuli wanayofanya hadi kwa nyingine.

| Eleza sifa muhimu za ngano |
|---|

Juu ya kazi hizi mbili, nyimbo huweza kutumiwa kama kiliwazo. Tunaposema hivi, tuna maana kwamba zinaweza kulegeza mtiririko na upeo wa matukio yanayotambwa katika ngano.

Kwa ujumla, kuna aina mbili za ngano. Aina ya kwanza ni hekaya. Katika hekaya, wahusika wakuu na muhimu huwa wanadamu. Aina ya pili ya ngano ni kharafa. Katika kharafa, wanyama na viumbe vingine visivyokuwa na uhai (kama miti, mawe, majitu) ndivyo hutumiwa kuwasilisha ujumbe. Haya ni makundi makubwa ya ngano yaliyoainishwa kwa mizani ya wahusika.

Complete Documents
Expanded Features

Wataalamu kama Grimms (Thomson,1946) wamependekeza kuwa aina za ngano zinaweza kutambulika kwa mujibu wa matukio muhimu yanayofanyika katika ngano hizo au kwa kufungamana na mitiririko ya ngano hizo. Ngano zinazotokana na jamii mbili tofauti au zaidi zitaainishwa kwa kundi moja maadamu matukio muhimu yanayosimuliwa nazo yanashabihiana kimsingi.

Kuna hadithi moja inayojulikana sana katika mkusanyiko wa ngano za Rose Mwangi (1970:86) ambayo inaelezea unyama Majitu juu ya mja mzito ambaye bwanake, mhunzi, alikuwa ameenda ughaibuni kusana. Jitu lilimnyanyasa mwanamke huyo hata akachoka. Kwa hiyo, aliamua kumtuma ndege mdogo kwenda kumwitia bwanake.

Ngano kama hii inapatikana katika jamii ya Waluhya pia. Katika ngango hii, ndege vile ndiye anatumwa kumwita bwana aliyeenda nchi za mbali kusana. Imani ya Grimms ni kwamba hizi ni ngano za aina moja kwa vile ambavyo zinaelezea juu ya matukio yanayofanana kimsingi. Mitiririko inayotumika kung’amua kama ngano zinafanana au hapana inaweza kuwa mirefu, kama ule uliorejelewa hivi karibuni. Pia, inaweza kuwa mifupi ikaonyesha mwelekeo wa ngano peke yake.

Tatizo linaloweza kutokana na matumizi ya tukio na mtiririko kama mizani ya kutambua ngano ni kwamba ijapokuwa ngano zinaweza kufanana katika vitengo vingi kimatukio na kimtiririko, utathmini wa ngano hizo huenda ukaathiriwa na miisho yake. Ikiwa matokeo yanayotarajiwa kutokana na mtawalio wa matukio ya ngano hayatimizwi na pengine mwishoni tukapata kinyume na matarajio yetu, bila shaka tutawajibika kusaili mizani ya matukio na mtiririko kama njia inayofaa ya kufafanua ngano.

Kwa mfano, kuna hadithi moja inayohusu jitu lililomdanganya msichana mrembo na kumwoa. Katika hali ya kawaida, baada ya msichana kama huyu kufunuliwa ukweli kuhusu ‘mchumba’ wake, hujaribu kukimbilia usalamani. Lakini katika hadithi inayorejelewa hivi sasa, jitu linamfuata msichana, linampata na kumla. Jambo hili linakanusha matarajio ya msomaji aliyezoea hadithi zenye mitiririko kama hii. Na jambo

Complete Documents
Expanded Features

hili lina maana kwamba hatuwezi kutegemea matukio na mitiririko kuielewa ngano hii moja kwa moja.

Tathmini njia mbalimbali za kuzianisha ngano katika makundi tofauti tofauti

Njia nyingine ambayo imetumiwa na baadhi ya wataalamu kuzifafanua ngano ni vikale vinavyopatikana katika ngano zile. Kikale ni nini? Kwa mujibu wa Mulika Namba 16 (1984: 49-50).

> Kikale ni aina ya mtiririko, wahusika au picha kongwe ambayo inajitokeza mara nyingi- labda kwa sura tofauti kidogo-katika kazi ya sanaa. Kwa mfano, mama wa kambo ni aina ya mhusika kikale katika hadithi za fasihi simulizi. Aina ya mtiririko kikale ni ile inayohusu mtu anayenyanyaswa ( kitinda mimba, kwa mfano) anayefaulu baadaye.

Kutokana na maelezo haya , taja baadhi ya taswira vikale vinavyojitokeza katika hadithi za kikwetu? Kuna maelezo ya kuwasawiri wanyama wadogo wadogo kuwa wajanja. Licha ya kutokuwa na nguvu za kiwiliwili, wao ni werevu na hutegemea werevu wao ( na wakati mwingine udogo wao kushinda katika ulimwengu wenye hatari nyingi). Ngano mashuhuri za kaka sungura na hadithi za Abunuwasi zinapatikana katika kundi hili.

Ukweli ni kwamba wahusika vikale waliosifika zaidi ni Kuchakulo na Sungura. Aghalabu hawa huchorwa kuwa na maarifa na ujanja wa kiwango cha juu. Hivyo, vikale vinaweza kutumiwa kuzifafanua ngano zikaitwa za ujanja, za majitu au za ukatili wa mama wa kambo kutegemea na wahusika wanaosawiriwa.

Upungufu wa vikale ni kwamba wajanja si washindi katika utekelezi wa miradi yao kila mara. Kuna ngano mbili katika kitabu cha Hare and Hornbill, ( Okot p'Bitek, uk.38-39) juu ya 'Sungura na Popo', na juu ya 'Sungura na Jogoo' ( Uk. 48-49). Katika ngano hizi, pwagu anapata pwaguzi, yaani, wajanja wanashindwa kuutumia ujanja wao kwa mafanikio hali ikawa ya 'mjinga akierevuka, mwerevu yu mashakani'.

Expanded Features
Complete Documents

Okot p' Bitek (uk.48-49) anatueleza kwamba Sungura na Jogoo walikuwa marafiki wakubwa. Siku moja Jogoo alimwalika Sungura nyumbani kwao. Sungura alifunga safari siku iliyofuata. Alipofika kwa akina Jogoo, Jogoo alimweleza hivi;

Rafiki yangu, unajua siku hizi nyama ni adimu kupatikana. Kwa hivyo ngoja kidogo niende jikoni nimwambie mamangu aukate mguu wangu mmoja kwa ajili ya kitoweo chako .

Sungura alishtuka na kusikitika kusikia hivyo. Alimsihi Jogoo asijifanye hivyo. Lakini Jogoo hakuambilika wala kushawishika. Alidai kwamba alikuwa na upendo mwingi juu ya rafiki yake na angemfanyia chochote kumfurahisha. Bila kupoteza wakati, Jogoo alitokomea akielekea jikoni.

Baada ya muda mfupi, alirudi huku akitembea kwa mruko wa mguu mmoja. Yaani mguu wake mwingine (kama alivyodai) ulikuwa umekatwa ili uwe kitoweo. Sungura alilalamika kwa mara nyingine. Lakini ilikuwa kama mtu aliyekuwa akilia juu ya maji yaliyomwaika ; hayazoleki.

Sungura alipenda sana kitoweo alichopikiwa. Kwa sababu hii, yeye pia alimwalika Jogoo. Tena mara moja! Jogoo alitarajiwa kufika kwa akina Sungura siku iliyofuata;

> "Najua kwamba mguu wako utakuwa haujapona. Lakini fika kwetu nami pia nikuonyeshe mapenzi yangu juu yako", Alisisitiza Sungura.

Jogoo alienda kwa akina Sungura kama alivyoahidiwa. Alikuwa bado akitembea kwa mruko wa mguu mmoja. Sungura alimkaribisha chumbani kwake. Mara, akamwendea mamake na kumwamrisha akinoe kisu.

"Kwa nini?", Mama aliuliza huku akionyesha wasiwasi.

"Wewe kinoe tu", Sungura alijibu bila kutarajia maswali zaidi.

Complete Documents
Expanded Features

Mamake Sungura alidhani kwamba pengine mwanawe alikuwa ameweka nyama mahali fulani. Lakini alishtuka alipomwona Sungura akikaa chini, kuunyosha mguu wake na kuamrisha "ukate!"

Mamake Sungura alisitasita, lakini alilazimishwa kutii amri huku akisimangwa na mtoto wake. Mguu ulikatwa. Huku akihisi uchungu chungu nzima na kuchirikwa kwa damu nyingi, alitoka kwa mamake akielekea alikokuwa Jogoo.

Jogoo alipomwona hakuamini. Alishikwa na huruma, akaanza kukimbia kumwelekea Sungura. Katika zile shamrashamra za kite na hangaiko, alisahau na kutumia miguu yake yote kukimbia. Sungura alikasirika sana kuona hivyo. Muda mfupi baadaye, alikufa kwa kutokwa na damu nyingi.

Ngano hii inadhirisha kwamba mnyama ambaye kwa kawaida hufikiriwa kuwa mjanja huweza kudanganyika. Katika jamii nyingi huko Afrika Magharibi, Mzee Kobe ndiye kiwakilisho cha ujanja na hekima. Lakini katika ngano ya C. Achebe inayopatikana katika Shujaa Okonkwo ( Sura ya 11 ), Mzee Kobe anavuna 'matunda' ya ulaghai wake. Ushahidi huu unaonyesha kuwa matumizi ya vikale hayana mantiki yanayothibitika katika hali zote.

## MHADHARA WA TATU

### Ngano

Baada ya mhadhara huu, utaweza:

(a) Kueleza wazi njia aliyotumia V. Propp kuifafanua ngano.

(b) Kuitathmini njia hiyo.

Kama tulivyoona katika mhadhara uliopita, kuna upungufu wa matukio na wahusika vikale kama njia za kuifahamu ngano. Kwa kuwa njia hizi hazikujitosheleza, watafiti waliendelea kuishughulikia ngano na kuonyesha jinsi inavyoweza kufahamika vizuri zaidi. Mmojawapo wa watafiti hawa alikuwa Vladimir Propp. Madhumuni ya Propp

Complete Documents
Expanded Features

yalikuwa kuieleza ngano kwa kuzingatia muundo wake. Ithibati za majaribio yake na matokeo ya majaribio haya yanapatikana katika kitabu chake cha Morphology of the Folktale. Tasnifu kuu ya Morphology ni kwamba ufafanuzi wa ngano kimuundo, ni wa kisayansi na wa hakika zaidi kuliko matumizi mizani zilizotangulia.

Eleza maana ya muundo katika muktadha wa kiisimu

Muundo ni umbo la kitu kutokana na jinsi kilivyoundwa na kutengezwa ( Hawkes, T. 1977). Propp anazungumzia muundo wa ngano kiisimu. Isimu ni taaluma inayotalii lugha ya mwanadamu kisayansi. Wanaisimu wanaoieleza lugha kuwa mahusiano ya miundo mbalimbali wanakubaliana kwamba lugha ina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ya lugha dhahania, nayo sehemu ya pili ni ya lugha tumikizi.

Lugha dhahania inahusu uwezo wa binadamu wa kuunda maneno na sentensi nyingi kadiri anavyotaka. Kwa upande mwingine, lugha tumikizi ni uwanja unaoshughulika na lugha halisi anayotumia mwanadamu katika mawasiliano ya kila siku. Lugha dhahania haiwezi kufafanuliwa bayana, lakini kutokana na lugha tumikizi, miundo na kanuni zake ( lugha dhahania zaweza kuhitamidiwa na kujulikana).

Mfano ufuatao umenuiwa kutusaidia kufahamu dhana hizi. Maana ya neno ‘pata’ katika lugha ya Kiswahili inatokana na uhusiano na mfuatano uliopo baina ya fonimu /p/, /a/, /t/, /a/. Ikiwa fonimu hizi hazitafuatana kwa mpangilio huu, neno, ‘pata’ halitakuwa na maana ya ‘pata’ tuifahamuyo. Pia, neno ‘pata likitamkwa, litapata maana kwa kuwa neno hili si “kata”, “bata, “tapa” wala “tata”. Kwa hivyo, mzungumzaji akisema “pata”, pata hiyo itakuwa na maana kufungamana na mfumo wa lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

Propp aliiazima dhana ya lugha kama mfumo wenye vipashio vinavyotegemeana na ambavyo maana zake hutokana na matumizi yake kufafanua ngano. Aliegemea zaidi katika ufafanuzi wa hekaya za Kirusi hasa zile zilizosimulia juu ya matukio ya ushujaa. Alitoa mifano ifuatayo kuthibitisha madai yake:

(i) Mfalme anampa shujaa furukombe.

Expanded Features
Complete Documents

Furukombe anambeba shujaa mpaka nchi nyingine

(ii) Mzee anampa surenko farasi.
Farasi anambeba Surenko hadi nchi nyingine

(iii) Mchawi anampa Ivan Jahazi
Jahazi inambeba Ivan hadi milki nyingine

Katika mifano hii mitatu, kazi ya wahusika wakuu ni sawa. Ni imani ya Propp kwamba ngano hizi zinaweza kuwekwa katika kijopo kimoja. Kutokana na majaribio mengi ya aina hii, Propp aliibuka na mbinu ya aina yake ya kuzianisha ngano. Kwa ujumla aliona kwamba kuna nyadhifa thelathini na moja katika hekaya za Kirusi. Wadhifa wa mhusika ni tendo linalofanywa na mhusika na umuhimu wa tendo hilo katika utekelezaji wa kadhia kuu ya ngano. Matendo hutegemeana ili yakue na huwepo kwa sababu ya ulazimifu wa mtiririko ya masimulizi.

Nyadhifa thelathini na moja zilizobainishwa na Propp ni zifuatazo:

(i) Jamaa wa aila fulani hutokomea.

(ii) Mhusika mkuu anaonywa kuhusu uvunjaji wa mwiko fulani

(iii) Mwiko unavunjwa

(iv) Mkinzani wa mhusika mkuu anatokea. Anajaribu kufanya udaku na upelelezi dhidi ya mhusika mkuu kwa lengo la kumwangamiza

(v) Mkinzani anapata habari juu ya windo lake

(vi) Mkinzani anajaribu kumghilibu nguli ili amtawale au aichukue bahati yake

(vii) Nguli anakubali vitimbi vya mkinzani bila kujua. Katika kufanya hivyo anamsaidia adui yake.

(viii) Mkinzani anamwumiza au kumjeruhi jamaa wa nguli.

(ix) Jamaa wa nguli anakosa kitu ambacho bila kwacho maisha yake hayatamridhisha. Pengine kitu hicho kilichukuliwa kwa ghilba za mkinzani.

(x) Kutokana na huu ukosefu, bahati mbaya inabainika. Nguli anatafadhalishwa au kuamrishwa kukitafuta hicho kitu.

(xi) Msasi anaamua kuanza muradi wake.

Complete Documents
Expanded Features

(xii) Nguli anakutwa na majaribu, pengine hata kushambuliwa. Jambo hili linamtayarisha kupata usaidizi mkubwa zaidi ama kutokana na uramali au kutokana na mhusika mwingine.

(xiii) Nguli anajaribu kuepukana na matendo ambayo yanaweza kumwangamiza baadaye.

(xiv) Nguli anapata nguvu za uramali

(xv) Anaenda au anapelekwa mahali pa utafutaji wake

(xvi) Nguli na mkinzani wake wanakutana na kupigana

(xvii) Mwanzoni, nguli anaabishwa

(xviii) Lakini baadaye mkinzani anashindwa

(xix) Bahati mbaya iliyokuwepo hapa awali inafutiliwa mbali

(xx) Nguli anatoka vitani na kuanza kurudi nyumbani au kwenda mahali pengine pasipojulikana.

(xxi) Anafuatwa na wasaidizi wa mkinzani.

(xxii) Nguli anaokolewa kutokana na wawindaji wake

(xxiii) Anafika nyumbani au nchi nyingine bila kujulikana

(xxiv) Mlaghai anajitokeza na kujijulisha kuwa yeye ni nguli

(xxv) Kazi ngumu kufanywa inapewa kwa nguli

(xxvi) Kazi hiyo inatekelezwa

(xxvii) Nguli anatambuliwa

(xxviii) Mkinzani pia anabainika

(xxix) Nguli anapewa taadhima na ‘sura’ mpya

(xxx) Mkinzani anaadhibiwa

(xxxi) Nguli anaozwa na kupewa kiti cha enzi

Nyadhifa za mhusika mkuu kama zilivyomdhihirikia Propp zimeorodheshwa. Si lazima nyadhifa hizi zote zionekane katika kila hekaya au kharafa inayosomwa au inayotambwa, au inayohusu ushujaa ama isiyohusu ushujaa. Kasoro inayotokana na “nyadhifa” za Propp ni kwamba ni nyingi sana na huenda zikadhoofusha uwezo wa kutofautisha ngano moja kutokana na nyingine.

Expanded Features
Complete Documents

## MAREJELEO

Hawkes, T. (1977) Structuralism and Semiotics. London: Mathuen.

Masoko, D.W et. Al (1984) Mulika Namba 16. Dar es Salaam: TUKI

Matteru , M.L.B (1987) "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi katika Mulika Namba 19. Dar es Salaam: TUKI

Mwangi, Rose (1970) Kikuyu Folktales. Nairobi: Kenya Literature Bureau

P'Bitek, Okot (1978). Hare and Hornbill. Nairobi: Heinemann.

Propp, Vladimir (1968). Morphology of the Folktale. Austin and London: University of Texas.

Thomson Stith (1946) The Folktale. New York: Holt, Rinehart and Winston.

## MHADHARA WA NNE

### Visakale

Baada ya mhadhara huu, utaweza:

(a) Kubainisha sifa muhimu za visakale

(b) Kulinganisha visakale na tendi

Kama jina hili linavyoonyesha visakale ni visa vya kale au ni hadithi zinazohusu matukio yaliyotendeka zamani. Kulingana na maoni ya M.M. Mulokozi, "Visakale ni masimulizi ya kimpapokeo juu ya wahenga na mashujaa wa kabila au taifa yenye kuchanganya chuku na historia" ( Mulika 21, 1989:5).

Visakale huwasilisha ukweli fulani kihistoria juu ya kikundi cha watu. Lakini vinatofautiana na mapisi. Mapisi hueleza historia bila kutia mambo ya kubuni. Visakale kwa upande wake hufumwa katika sanaa yenye ubunifu ndani yake kadiri ya kuupeleka ukweli masafa kadhaa kutoka kwenye sanaa.

Aghalabu, kadhia zinazosimuliwa katika visakale ni njaa, kiangazi, magonjwa maambukizi, uhamaji, vita na mengineyo. Wahusika wengi katika visakale ni wanadamu. Ni wanadamu wenye uwezo mkubwa au mdogo kutegemea mantiki wanayowekewa. Kwa kuwa kisakale kinaweza kurudiwarudiwa kwa njia mbalimbali, kisakale kimoja kinaweza kuwa na matoleo tofauti tofauti kutegemea malengo na mielekeo ya watambaji. Kumbuka kwamba hii ni mojawapo ya sifa za fasihi simulizi. Miundo yake hubadilika kulingana na imani za wasimulizi na vilevile kufungamana na

Complete Documents
Expanded Features

mageuzi ya mandhari inamotambiwa. Tumesema kwamba baadhi ya wahusika wa visakale wana uwezo mkubwa. Hawa wahusika wanasadifu maelezo J.S Madumulla juu ya usawiri wa wahusika wakuu wa mwanzo tunaokumbana nao katika fasihi andishi ya Kiswahili:

> Mhusika huyo alikuwa na nguvu
> za ajabu na ujasiri usio wa
> kawaida, na alitambuliwa kwa
> urahisi kutokana na sifa za
> uadilifu, nguvu na akili ambazo
> hazikuwa na mpaka; mhusika
> ambaye alikuwa na hali ya ajabu,
> nguvu za kiungu, majaribu
> magumu na aghalabu hamu
> isiyovia ya kutimiza lengo lake
> (Kiswahili, 1987:60)

Sifa hizi zimetokana hapo awali na wahusika wa tanzu za fasihi simulizi kama visakale na tendi. Visakale na tendi ni tanzu za fasihi simulizi zinazoshughulika na masimulizi ya ushujaa. Kwa kuwa wahusika hawa hupewa sifa na hulka za kuajabisha, mianzo ya visakale aghalabu hushabihiana na mianzo ya masimulizi mengine ya kimapokeo kama ngano.

Huanza kutambwa kwa, "Hapo zamani za kale……..." Lugha inayotumiwa kutamba visakale inaleta hisi kwamba matukio na mizimu inayorejewa havina uhusiano bayana na mambo yanayopitika katika jamii husika. Ukweli ni kwamba baadhi ya kadhia zinazozungumzwa ni ithibati ya matukio halisi yaliyotendeka katika jamii inayohusika. Mifano ya visaakale ni "Fumo Liyongo" na "Lwanda Magere". Wahusika hawa wana sifa ambazo bila kwazo kujulikana hawawezi kuuawa.

| |
|---|
| Linganisha sifa muhimu za Fumo Liyongo na Lwanda Magere (baada ya kuufanya utafiti wako mwenyewe. |

Jambo muhimu linalopaswa kutiliwa maanani vilevile ni kwamba kuna mfanano baina ya baadhi ya visakale na tendi hasa katika usawiri wa wahusika wake wakuu. Kisakale cha Liyongo ( Mhina, 1970) na Utenzi wa Liyongo (1913) ni tanzu zinazofanana kwa kuwa

Complete Documents
Expanded Features

zote zinarejelea sifa za kati za Liyongo. Hata hivyo Utenzi wa Liyongo ni utanzu wa kishairi, nacho kisakale cha Liyongo ni utanzu wa kinathari.

| Jadili Utenzi wa Liyongo na kisakale cha Liyongo kwa upande wa dhamira na fani. |
|---|

Kama tulivyogusia hapo mwanzoni, utanzu wa fasihi simulizi unaokaribiana pia na visakale ni mapisi. Haya ni maelezo ya kihistoria ambayo hayajapigiwa chuku yoyote. Yanaweza kuwa juu ya matukio yanayopatikana katika kumbukumbu ya jamii kama ushindi wa vita. Au yanaweza kuwa maelezo kuhusu koo mbalimbali na jinsi zile koo zilivyojumuika kuunda taifa moja. Maelezo ya Mwakilongomutwa Mwakiyombwe mwanzoni mwa tamthilia ya Mukwava wa Uhehe (1979) ni mfano mzuri wa mapisi. Mapisi mengine yanaweza kumhusu mtu aliyeishi hivi karibuni au ambaye bado anaishi ambaye kadhia alizofanya zinastahili kuhadithiwa juu yake.

## MAREJELEO

Kijumwa, M. (1913) Utenzi wa Liyongo.
Lo Liyong, Taban (1972) Popular Culture of East Africa. Nairobi: Longman
Lusweti, B.M. (1984) "Legends" katika The Hyena and the Rock. Nairobi: Macmillan
Massamba et. Al (1987) Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.

## MHADHARA WA TANO

Baada ya mhadhara huu, utaweza:

(a) Kueleza maana ya kisaasili

(b) Kufafanua njia mbalimbali za kueleza kisaasili kwa njia ya kitaalamu

Visaasali vimeelezwa kwa njia mbalimbali kimapokeo. Baadhi ya maelezo yanasema kwamba ni hadithi ambazo pamoja na kuwa na wahusika wa aina tofauti tofauti hasa miungu na binadamu, husimulia juu ya matukio ya kiada ( Matteru 1987). Kama jina la utanzu huu lilivyo visaasili ni visa vya mianzo. Hushughulikia mianzo ya matendo yaliyozowewa kama unyago, ndoa, tohara na imani mbalimbali. Mbali na kufafanua mianzo ya desturi, hutoa utaratibu unaofuatwa katika utekelezaji wa desturi hizo. Wakati

Expanded Features
Complete Documents

mwingine matukio yanayotambwa katika visaasili hufumwa katika lugha ya kimafumbo. Kwa ujumla, visaasili ni:

> Hadithi za kale zenye kuwakilisha
> imani na mtazamo wa jamii inayohusika
> kuhusu asili ya ulimwengu na mwenendo
> wake, kuhusu asili yao wenyewe, na
> maana na shabaha ya maisha yao.
> Mara nyingi hadithi hizi huaminiwa
> kuwa kweli tupu na hutumika kuelezea
> au kuhalalisha baadhi ya mila na madhehebu ya jamii
> inayohusika ( Mulokozi 1989:6).

Maoni ya J.G Frazer katika The Golden Bough ni kwamba visaasili ni uigizaji wa matukio kitamathali, matukio ambayo hapo awali yalihusishwa na sherehe kama uganga, uchawi na uramali. Maigizo haya ni aina ya hadithi iliyobuniwa ili ieleze jinsi ada fulani ilivyoanza. Hivyo basi, kisaasili huliwekea mantiki tukio la kiada, chanzo chake na jinsi ililivyopokewa na vizazi mbalimbali vya jamii inayohusika.

Katika ujirani wetu ( bara la Afrika), mtaalamu aliyefanya utafiti mpana juu ya visaasili ni Isidore Okpewho. Ameandika kitabu cha Myth in Africa (1983). Licha ya kuvipitia baadhi ya vielezi tulivyovipitia kuhusu maana na dhima ya visaasili, anaonyesha kutoridhika kwake na vielezi hivyo. Katika kitabu cha Myth in Africa, Okpewho anatoa madai mapya ambayo yalikuwa hayajatiliwa maanani na wataalamu waliomtangulia. Madai yake ni kwamba vielezi vinavyoviona visaasili kama kitengo cha anathropolojia ya kidini haviridhishi – kwa kuwa ukweli wote kuhusu visasili hauwezi kujulika kupitia kwavyo.

Miongoni mwa mengine, uamuzi wa Okpewho unatokana na uchambuzi anaofanya juu ya kisaasili cha kabila la Lo Dagaa wanaoishi katika sehemu za kaskazini za nchi ya Ghana. Kisaasili cha Wa Lo'Dagaa kimehifadhiwa kimaandishi katika kitabu kilichohaririwa na Jack Goody kinachoitwa The Myth of the Bagre. Okpewho aliona kwamba kisaasili hakiliwekei tukio mantiki; maoni yake ni kwmba kuna maingiliano mengi kati ya ukweli na uzushi, hasa ikiwa sherehe inayoadhimishwa haijakufilia mbali. Imani yake ni kwamba umbo asili la kisaasili hubadilika katika mapito ya wakati kwa sababu ya usahaulifu wa watu wanaopaswa kukikumbuka, na vile vile, kwa sababu ya

Complete Documents
Expanded Features

mageuzi yanayoweza kutokea katika mazingira yao. Okpewho anadai kwamba lazima mabadiliko haya yatatanishe toleo la kisaasili chasili.

Pengine madai ya Okpewho yatafahamika zaidi tukikipitia kisaasili cha Lo Dagaa. Kabila hili lina kisaasili kinachoigiza namna ya kuwaingiza watu katika jando ya kuvumilia ili hatimaye wafanikiwe maishani. Jando yenyewe huitwa "Bagre"- na ndiyo sababu iliyokifanya kitabu kilichohaririwa na Jack Goody kuitwa The Myth of Bagre.

Kisaasili cha Bagre ni hadithi ya ndugu wawili waliokuwa wakiishi kwa taabu na uhitaji mwingi. Baada ya Ndugu hawa kuamua kupitia mistuni na poroni ambamo walikutana na viumbe vya ajabu ajabu, waligundua ufunuo wa kunga mbalimbali za kukabiliana na kuepukana na majanga ambayo yalikuwa yamewalemea hapo awali. Tajriba walizopitia ndugu hawa zilizua utaratibu wa matukio. Kama utaratibu huu ungefuatwa katika mviga ya baadaye, ungeweza kuvipa vizazi vilivyofuatia ufanifu usiokwisha.

Okpewho anaainisha jambo moja ambalo kwa maoni yake litamshangaza msomaji au msikilizaji wa kisaasili cha Bagre. Kuna uhamishaji, ubadilishanaji na upokezanaji wa ishara na maana baina ya ndugu wa asili waliopitia sherehe hiyo hapo mwanzoni na wale wanaoipitia wakati uliopo. Mtambaji wa kisa hiki huwaona jamaa wanaoingizwa jandoni sasa kana kwamba ni mababu wa mwanzo walioipitia sherehe zamani.

Maoni ya Okpewho ni kwamba ikiwa kisaasili hiki kimepokewa mdomo kwa mdomo, basi kimsingi kilitambwa na ndugu wawili kama kinavyosimuliwa wakati uliopo juu ya jamaa wanaoingizwa jandoni. Hii ina maana kwamba hata na wale mababu wa mwanzo walipokuwa wakijiingiza jandoni, waliwarejelea mababu wengine. Kutokana na uchunguzi huu, Okpewho anahitimisha kwamba hakuna uhakika ikiwa kisaasili hutangulia sherehe kinachoadhimisha au shere hutangulia kisaasili. Yaani, haijulikana kwa hakika iwapo kisaasili huingia mwanzo kisha kikifuatwa na tukio la kiada au kinyume na haya hufanyika.

Katika kutoa kauli hizi, Okpewho anakanusha vielezi vya kimapokeo vilivyokita katika anthropolojia ya dini.

Linganisha maoni ya Okpewho kuhusu maana ya kisaasili na dhana zilizokita katika

Expanded Features
Complete Documents

anthropolojia ya kidini kuhusu kisaasili.

Maoni ya Okpewho ni kwamba maana ya kisaasili inapatikana katika ufahamu wa maingiliano ya ukweli na uzushi katika kisa hicho. Kadiri tendo linaloadhimishwa na kisaasili fulani linavyozidi kusahaulika ndivyo uzushi mwingi unavyolikolea tendo hilo. Anavyodhamiria kusema Okpewho ni kwamba kila tunaposonga nyuma katika mapito ya wakati, uhakika wa kisaasili hubainika zaidi. Kisa cha mwanzo kina ukweli zaidi kikilinganishwa na kisa cha hivi karibuni zaidi. Ikiwa tendo linalosimuliwa katika kisaasili fulani lilifanyika juzijuzi, halina budi kuripotiwa kwa uaminifu zaidi. Sababu ni kwamba baadhi ya washiriki katika tendo hilo watashadidia ushuhuda wa kweli kuhusu tendo hilo.

Hata hivyo, Okpewho anakubali kwamba umbuji wa mtambaji huchangia ukweli au uzushi unaopatikana katika kisaasili fulani. Hatimaye, kulingana na maoni ya Okpewho, kisaasili ni malighafi ambayo wanajamii hutumia kuelezea utamaduni wao toka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Katika kufanya hivyo kisaasili husawiri uzushi mwingi kuliko ukweli na ubunifu mwingi kuliko uhakika katika mapito ya wakati.

Uamuzi huu haukubaliwi na P.O Anyumba ambaye katika mihadhara yake alishikilia kwamba viwango vya uzushi na ukweli, ubunifu na uhakika huenda bega kwa bega kila kisaasili kinapotamwa. Kwake, kisaasili ni ukweli uliokolewa na uzushi. Kama hamna uzushi katika kisaasili, hakitakuwa kisaasili tena.

## MAREJELEO


Frazer, J.G (1957). The Golden Bough. London: Macmillan

Goody, Jack (1972) The Myth of the Bagre. Oxford; Clarendon

Matteru, M.L.B. (1987) “Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi” Katika Mulika 19. Dar es Salaam: TUKI

Mulokozi, M.M. (1989) “Tanzu za Fasihi Simulizi” Katika Mulika 21. Dar es Salaam: TUKI

Okpewho, Isidore (1983) Myth in Africa. London: Cambridge University Press.


## MHADHARA WA SITA

Expanded Features
Complete Documents

**Istiara (b) Mbazi (c) Kisa.**

(a) Baada ya mhadhara huu, utaweza kueleza maana ya (i) (a) Istiara ( b) Mbazi (c) Kisa
(b) Kutoa mifano ya kila mojawapo ya tanzu hizi.

(a) Istiara ni hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine isiyokuwa ya wazi. Ni masimulizi ambayo hutumia ishara zenye maana ambazo hujitokeza katika masimulizi mengine. Mifano ya hadithi za aina hii ni ngano zozote zinazozungumzia kadhia mbalimbali kuhusu maisha ya mwanadamu huku zikitumia wanyama au taashira za aina nyingine kama viwakilisho vya wanyama hao. Hadithi za sungura, majitu, kobe na dubu kwa hakika zimekusudiwa watu. Isifikiriwe zinazungumzia wanyama. Wanadamu wanapaswa kukusanya mafunzo kutokana na matendo na uhusiano wa wanyama hao. Ikiwezekana, majina ya wanyama yanaweza kubadilishwa kwa majina ya wanadamu halisi.

Jadili sifa muhimu za istiara. Kuna maingiliano gani kati ya istiara na kharafa?

Pengine mwanasanaa wa fasihi ya Kiswahili aliyetumia Istiara nyingi sana katika maandishi yake ni Shaaban Robert. Masimulizi yake ya mwanzo ya Adili na Nduguze, (1952), Kufikirika (1967) na Kusadikika (1952) yametumia Istiara. Katika masimulizi haya, vitu, watu na wahusika vinasimamia mawazo na dalili fulani maalumu- (Mulika 16, 1984: 49). Jambo hili linazusha utata mwingine juu ya vigezo vinavyotumiwa kuziainisha ngano. Katika mihadhara iliyotangulia tulizingatia matukio, vikale na dhima za wahusika. Sasa, tumeona kwamba vigezo vya kifani pia vyaweza kutumika kubainisha tanzu.

(b) Mbazi: Hii ni hadithi fupi yenye mafunzo itolewayo kama mfano wakati wa maongezi au wa kumwonya mtu. Hadithi hii inaweza kuwa mrando mfupi kutokana na mkondo au mwelekeo wa hotuba au mafunzo maalumu yanyowasilishwa. Pengine mwalimu aliyemakinika zaidi katika matumizi ya aina

Expanded Features
Complete Documents

hii ya hadithi alikuwa Yesu Kristo. Aliwaelekeza wanafunzi wake na walimwengu kupitia katika mbazi.

Pamoja na mbazi kuzungumzia hali halisi inayopatikana katika maisha ya watu, hutoa ujumbe wake kwa muhtasari na kwa uyakinifu zaidi kuliko fundisho lenyewe, ambalo huenda likawa limefumwa katika lugha dhahania. Mbazi huliweka wazo dhahania katika muktadha maalum unaofahamika. Kutokana na haya, maswali mengi kuhusu fundisho au wazo hili hujibiwa kwa urahisi. Katika wakati wa Yesu Kristo, mbazi zilifaa kwa wasikizaji ambao pengine hawakukuwa na muda mrefu wa kuketi mahali pamoja ili wafundishwe.

| Huku ukitoa mifano inayofaa onyesha tofauti kuu zilizopo kati ya istiara na mbazi |
|---|

( c) Kisa: Wakati mwingine huitwa kidahizo. Kwa mujibu wa maelezo ya Mulika 16 (1984:48):

> Ni masimulizi mafupi yanayohadithia tukio moja bila ya kujifafanua. Kwa mfano, kidahizo cha nyani na mtotowe. Nyani na mtoto wake walikwenda kula mahindi katika shamba. Wakala, wakala, wakala. Halafu mtoto aliuliza, Mama, tunakula tu, je mpaka uko wapi? Mamaye alimjibu, Wewe kula tu mpaka wataweka wenyewe.

Kidahizo pia huweza kutoa funzo ijapokuwa hakilifafanui vizuri kama mbazi. Mfano mzuri unapatikana katika riwaya ya Kisima cha Giningi (1991:88) ambapo Muhammed Saidi Abdullah anasema:

> Kuna hadithi moja katika hadithi za Esopo ambayo
> tunaweza kutueleza hali ya mambo yalivyokuwa hivi sasa.
> Hadithi hiyo inatueleza namna msasi mmoja na mbwa wake
> walivyokuwa wakimfukuza Sungura aliyekimbilia baharani.
> Msasi alipomlaumu mbwa wake kwa nini hakumpata yule Sungura,
> mbwa alijibu, “Pana ajabu gani mimi kumkosa Sungura.
> Sungura anakimbia kuokoa roho yake; lazima awe na
> nguvu ya kukimbia. Mimi nikwanda mbio kwa sababu ya
> kutaka sifa tu.

Expanded Features
Complete Documents

Mwandishi ametumia kidahizo hiki kuthibitisha kwa nini Msa na Sajin Paolo hawakufaulu kuwashika Ali Makame na Hamadi Mshenga.

Kidahizo pia kinaweza kutokana na tukio la kweli, ambalo laweza kuchekesha. Kuna vidahizo vingi vilivyotokana na uhusiano ambao ulikuwepo baina ya Waafrika na Wazungu. Tumewahi kuelezwa kidahizo kifuatacho toka Utaitani. Mzungu alimwona mwanamke aliyekuwa akiuza machungwa. Kwa vile alitaka kuyanunua alimwendea mwanamke, akatwaa chungwa moja mkononi kisha akauliza, "How much?" Mwanamke alidhani Mzungu anauliza juu ya "Maji". Kwa hivyo alijibu, "Maji yanapatikana mahali popote".

## MAREJELEO


Abdulla, M.S (1991) Kisima cha Giningi. Nairobi, Evans Brothers.
Masoko, D.L.W. et. A. (1986) Mulika namba 16. Dar es Salaam: TUKI
Mulokozi, M.M. (1989) "Tanzu za Fasihi Simulizi" katika Mulika 21 ( Wahariri: A.M. Khamisi and J.S. Madumulla), Dar es Salaam: TUKI
Robert, Shaaban (1952) Adili na Nduguze.
------------------ London and Basingstoke: Macmillan
------------------=(1967) Kufikirika Nairobi: Oxford University Press
--------------------(1951) Kusadikika. Nairobi: Evans Brothers.


### MHADHARA WA SABA

**Ngano za kwa Nini?**

Baada ya mhadhara huu, utaweza kueleza:

(a) Sifa muhimu za masimulizi ya kwa nini?

(b) Kutofautisha visaasili kutokana na masimulizi ya kwa nini?

Masimulizi ya kwa nini ni ngano zinazoeleza na kufafanua mianzo ya kaida za kitamaduni na zinazopatikana katika mazingira anamoishi mwanadamu. Tofauti kii iliyopo baina masimulizi ya kwa nini? Na visaasili ni kwamba hayashirikishwi na imani za kichini kama visaasili vilivyo.

Ngano za kwa nini zinazojulikana zaidi ni zile zinazojaribu kueleza sababu zinawafanya baadhi ya wanyama kuwa na sifa fulani. Kuna ngano zinazoelea kwa nini koo huchakura

Complete Documents
Expanded Features

mchanga, na nyingine zinazoonyesha kwa nini mbuni ana shingo ndefu. Aghalabu ngano hizi zimekusudiwa watoto kwa kuwapa maelezo rahisi ya kusuluhisha udadisi wao. Mfano wa ngano za kwa nini ni huu unaofuata.

Asili ya Fisi kuwa na Manyoya Meupe.

( C.K. Omari, 1972: 43-46)

## MAREJELEO

Nandwa, J. & Bukenya, A. (1984) African Oral Literature for Schools. Nairobi: Longman Kenya.

Omari, C.K. (1972) Hadithi za Bibi Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

## MHADHARA WA NANE

**Tanzu za Fasihi Simulizi**

**Semi**

**Vitendawili**

Baada ya mhadhara huu utaweza kueleza

1. Semi ni nini
2. Vipera vya semi
3. Maana ya vitendawili
4. Dhima ya vitendawili
5. Jinsi ya kuchambua vitendawili

Katika kuendeleza mhadhara huu twapaswa kukumbuka kwamba lengo letu ni kueleza fani ya semi pamoja na kuviainisha vipera vyake. Zaidi ya hayo mhadhara huu utajikita katika kushughulikia kipera kimoja nacho ni vitendawili.

### Semi ni nini?

Semi ni fungu la tungo za kisanaa ambazo ni fupi fupi zenye kutumia picha, tamathali na ishara. Semi hizi hubeba maana na mafunzo muhimu ya kijamii. Semi zaweza kugawanywa katika vipera kadha navyo ni:-

(i) Vitendawili
(ii) Methali
(iii) Misimu
(iv) Mafumbo
(v) Lakabu

Expanded Features
Complete Documents

Tutaanza na vitendawili.

## Vitendawili

Mwansoko (1988.1) aeleza kuwa vitendawili ni sehemu ya fani ya fasihi simulizi na fasihi simulizi ni sanaa ambayo inatokana na ubunifu wa uwezo wa mwanadamu. Ni uzungumziaji wa kitu au jambo fulani ambao unafanywa kwa kusanii ( sio kwa mazungumzo ya kawaida) ukiwa kwa swali au kwa fumbo linalotaka kufumbuliwa .

Katika kuchangia maelezo ya maana ya vitendawili Mulokozi (1989:15) anasema

> "Kitendawili ni usemi uliofumbwa ambao hutolewa kwa hadhira ili ufumbuliwe".

Kutokana na maelezo ya wataalam hao wawili kile kinachobainika ni kuwa vitendawili ni mojawapo wa tanzu za fasihi simulizi. Zaidi ya hayo imebainika kuwa vitendawili ni semi fupi fupi za mafumbo ambazo hudai ufumbuzi. Fumbo lenyewe huwa ni kauli ambayo huwa na maelezo ya kutega na kwa hivyo hudai uteguzi.

Fumbo hilo kwa kawaida huwa linafahamika katika jamii husika na mara nyingi huwa na mafunzo muhimu kwa washiriki mbali na kuchemsha bongo zao. Kwa vile vitendawili ni mafumbo, ufumbuzi wake hutegemea uwezo wa mtu wa kutambua, kuhusisha na kulinganisha vitu vya sampuli mbalimbali vilivyomo kwenye mazingira yake. Vitendawili huhitaji akili pevu na tambuzi, akili yenye busara na hekima. Jibu na maelezo yanayotolewa kwa kitendawili sharti yasadifu na kulingana na hali na tabia na mazingira ya jamii inayohusika. Vitendawili ni sanaa inayotendwa na huwa imejisimamia yenyewe kinyume na methali ambazo ni sanaa tegemezi (Mulokozi ( 1989: 15). Vitendawili hutumia picha, tamathali na ishara kueleza wazo lililofichika ambalo ndilo jawabu la fumbo. Vitendawili hupewa jibu lake kwa maneno au maelezo. Hata kama kitendawili kinatolewa kwa sauti, badala ya maelezo. Jibu lake huwa linafahamika katika jamii husika. Kwa mfano katika jamii ya Wagikuyu kitendawili chaweza kutolewa kwa sauti kama:

Hu! Jibu lake huwa ni mwanamke mjamzito wakati anapopanda mlima.

Complete Documents
Expanded Features

Au

'Si na si' – jibu lake huwa ni uzi na sindano

## Muundo wa Kitendawili

Vitendawili vingi huwa na muundo mmoja tu, muundo wa kimapokeo yaani wa kiasili. Kitendawili huwa kimegawanywa katika sehemu nne:-

(a) Kiingizo/kitangulizi
Fanani katika fani ya vitendawili huanza kwa kusema 'kitendawili'. Washiriki ambao mara nyingi huwa ndio hadhira hujibu 'tega'.

(b) Sehemu ya pili ya kitendawili huwa ni kitendawili au fumbo lenyewe.

(c) Sehemu ya tatu huwa ni swali la msaada ikiwa hadhira haikuelewa kitendawili. Mara nyingi hadhira huuliza maswali ya msaada katika juhudi za kutafuta jibu la fumbo. Iwapo jibu linafahamika mara moja, mara nyingi huwa hakuna haja ya swali la msaada.

(d) Sehemu ya mwisho ni jibu la kitendawili. Washiriki wakishindwa kutoa jibu la kitendawili waweza kutoa kichocheo kwa fanani ili awafumbulie fumbo lake au atoe jibu kwa kitendawili chake mwenyewe.

Kichocheo mara nyingi huwa mji. Fanani husema:
'Toa mji'
Hadhira hutoa mji ambao utamshawishi fanani kutoa jibu la fumbo lake. Utoaji wa miji ulitokana na jadi za kivita za kuteka miji baada ya jamii fulani kushinda katika vita.

Kichocheo kingine ambacho huweza kutolewa ni:
Hadhira! Oa mke
Fanani ; Lipa mbuzi

Baada ya fanani kuridhishwa na kichocheo anachopewa na hadhira yake anatoa jibu kwa fumbo lake. Kutokana na muundo huu inabainika kuwa katika fani ya vitendawili ni lazima kuwe na washiriki wa aina mbili:

Expanded Features
Complete Documents

(i) Mfumbi – yule anayetoa fumbo

(ii) Mfumbuzi- yule atakayetoa jibu. Kwa hivyo katika kukamilisha fani hii panapaswa kuwa na mtegaji na mteguzi.

Muundo wa vitendawili ni wa majibizano. Mtambaji hutoa kitangulizi na kitendawili naye mtambiwa hujibu ‘tega’. Mtambaji hutoa kitendawili au fumbo lenyewe. Mtambiwa hutarajiwa atoe jibu na akishindwa anamshawishi mtambaji atoe jibu la kitendawili chake kwa kumpa kichocheo. Aina ya kichocheo hutegemea jamii inayohusika. Katika jamii za kivita tumeona kichocheo chaweza kuwa mfugo kama ng’ombe, mbuzi na kadhalika. Fanani wengine katika jamii za wakulima hudai mashamba.

## Dhima ya Vitendawili

Vitendawili hutegwa kwa lengo maalum. Mara kwa mara vitendawili huwa na dhima kubwa katika kukomaza fikira na falsafa pamoja na kuburudisha na kuliwaza. Vitendawili hutumiwa kama chombo cha kufunza vijana ili bongo zao ziwe stadi, wawe na busara, wawe na mahiri na wapate urazini katika kupambana na harakati za maisha wakati watakapokuwa watu wazima. Vijana hupewa mbinu za kupambanua mambo ya maisha halisi vilivyo. Zaidi ya hayo wanapewa nyenzo za kujenga moyo wa kiushujaa na ari ya kujivunia itikadi za jamii.

Kwa vile vitendawili huhusishwa na maumbile ya jamii, vijana huandaliwa katika kuelewa mazingira yao kwa matumizi ya fani ya vitendawili. Vijana wanajulishwa aina ya mimea, miti, wanyama vifaa vya matumizi ya nyumba na mambo ambayo kwa jamii huwa ni maajabu au miujiza kama mwezi, jua na nyota.

Pia vitendawili hutumiwa kutoa mafunzo kuwaandaa vijana waume kwa wake watakapopata umri wa kuwa na nyumba zao na watoto wao. Isitoshe vitendawili vyaweza kutumika kujenga ari ya kushindana na kuzoesha vijana wawe wepesi wa kufikiri, kuamua, kutoa jawabu maridhawa. Vitendawili vingine hujikita katika kutoa mafunzo ya dini, itikadi na mielekeo ya jamii husika. Pia vitendawili vyaweza kutumiwa

Expanded Features
Complete Documents

kukebehi na kutoa vitisho kwa vijana ambao waweza kutoa siri za jamii. Kwa mfano katika kitendawili cha;-

'Yeye anatuona sisi hatumuoni'.

Jibu lake ni Mungu. Kitendawili kama hiki hutoa mafunzo ya kidini kwamba kila wakati Mungu huwa anatuona hata ikiwa sisi hatumuoni. Kwa hivyo wakati mtu anapofanya jambo, jambo hilo liwe zuri au baya hata ikiwa hakuna mtu anayemuona apaswa kukumbuka kuwa Mungu anamuona. Kitendawili kama hiki chaweza kutumiwa kuzuia watu kutenda mambo maovu wakidhani hawatajulikana kwa vile hata wasipoonwa na mtu. Mungu huwa amewaona.

Ingawa vitendawili hutegewa watoto, si vya kitoto. Vitendawili ni vito vya thamani. Thamani yake huwa ni maana au ujumbe utolewao na kitendawili hicho katika kuiekeleza jamii.

Dhima ya vitendawili nyingine ni kutajirisha na kupamba mazungumzo. Pia vinatumiwa kuanzisha, kukatisha au kukamilisha hadithi au kisa kinachoelezwa. Kwa hivyo vitendawili kama fani zingine za fasihi huwa na umuhimu wa kufufua, kuhifadhi, na kukuza au kuendeleza utamaduni wa jamii.

Vinatumiwa kama vyombo vya kuburudisha. Vitendawili katika jamii nyingi hutumiwa kama vyombo vya kustarehesha, kufurahisha na kuchekesha wanajamii. Vitendawili hupigwa wakati wa jioni baada ya watu kufanya kazi mchana kwa lengo la kuburudisha na kujipumzisha. Kwa hivyo utegaji wa vitendawili ni mbinu moja ya kustarehesha au kupunguza na kusahaulisha uchovu. Katika muktadha huo vitendawili hutumiwa kama vichekesho. Kitendawili ni fumbo zito linalodai jawabu yenye maana. Fumbo lo lote liwalo hufikirisha. Vitendawili hufanya mtamba na mtambiwa kutumia akili na busara. Ndivyo maana vitendawili hujulikana kwa jina la chemsha bongo. Kama tulivyodokeza hapo awali vitendawili ni vito vya hekima. Hekima ya kitendawili hupatikana katika

Complete Documents
Expanded Features

kitendawili chenyewe na katika jibu lake. Vitendawili hufunza, huonya, huelekeza na hushauri. Vitendawili huadilisha na huadibu.

Dhima nyingine ya vitendawili ni kuelimisha jamii. Elimu hii hutanda nyanja mbalimbali za maisha ya binadamu. Vyaweza kutoa elimu ya kisasa, kiuchumi na kijamii, kisayansi n.k. Elimu huenda na wakati kadhalika na vitendawili. Kwa kadri jamii inavyojiendeleza kisiasa na kisayansi ndivyo pia vitendawili vinavyozidi kuchukua mfumo mpya.

## Usanifu katika Vitendawili

Vitendawili ni sanaa pevu sana. Vina usanii wa hali ya juu sana. Usanii huu hujibainisha tokea katika sanaa hadi maudhui yenyewe. Usanii ni ule ujuzi na uwezo wa kueleza au kutoa jambo kwa ufundi wa kuvutia. Hali hii hutokana na ujuzi mkubwa wa lugha. Usanii pia upo katika maudhui ambayo mara nyingi hujificha. Kitendawili chaweza kuwa na undani ambao si rahisi kuupata. Humo, huweza kuwa falsafa kubwa sana iliojizika katika kina kirefu cha maudhui. Fasihi simulizi hutumia picha mbalimbali katika kupamba lugha yake ili iteke hamu na shauku ya msikilizaji au mtazamaji ili ujumbe unaohusika ufanikishwe katika kufikia yule aliyekusudiwa.

Je usanifu wa vitendawili hudhihirika vipi?

Vitendawili kwa kawaida vina hulka ya kipekee ambayo hujipambanua na lugha ya kawaida . Yote yaliyomo katika vitendawili hujihusisha zaidi katika silka, itikadi, utamaduni, uchumi siasa na uhusiano wa matabaka ya jamii. Usanifu wa vitendawili unategemea zaidi sanaa ya watu wa jamii ambayo vitendawili hivyo vimetungiwa kwa ajili ya watu wa jamii hiyo tu.

Vitendawili vya Kiswahili vina utanashati mkubwa wa lugha. Vina utajiri wa tamathali za usemi. Vitendawili vingi vya Kiswahili hutumia picha. Picha hizi hujitokeza ama

Complete Documents
Expanded Features

katika kitendawili ( fumbo) chenyewe au katika jawabu. Picha hizi aghalabu huwa ni za vitu.

Mbinu ambazo hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa vitendawili ni nyingi kama Khatibu (1978:26) anavyoonyesha. Baadhi ya mbinu hizi ni:

(i) Mliolio. Kuna vitendawili ambavyo hutumia mbinu ya mliolio au Tanakali za sauti katika kuwasilisha ujumbe wake. Tanakali za sauti ni maneno ambayo huundwa katika sentensi kutokana na sauti zinazofanana. Wakati mwingine mfanano huu huelezwa kutokana na kurudiwarudiwa kwa neno au maneno yanayofanana.

Kwa mfano vitendawili vifuatavyo vimetumia mbinu hii ya mliolio au tanakali sauti.

(i) Pakacha tii ( ugonjwa wa matende)
(ii) Ba funua ba funua ( unyayo wakati wa kwenda).
(iii) Dii! Halina mshindo ( Difu)
(iv) Parr! Mpaka Marka ( utelezi)

Ushairi ni mbinu nyingine ambayo hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe wa vitendawili. Katika matumizi ya ushairi, kuna utumiaji wa mapigo ya kimuziki kwa utaratibu maalum. Vile vile katika matumizi haya lugha hutumiwa kwa mkato na hupangwa kwa mpangilio mahsusi. Sarufi ambayo hutumiwa huwa imekiuka kaida za mpangilio wa lugha iliyozowewa. Kwa mfano katika vitendawili hivi mbinu ya ushairi inadhihirika.

> Mchana “uu” usiku “uu” ( macho).
> Futi kafutika futi, futi kafutika
> Futi ( nazi- kumbi, fuu nazi maji)
> Huku ‘ngo’ na kule “Ngo” (giza)

**Tashihisi:** Katika mbinu hii vitu ambavyo havina uhai wala tabia za binadamu hupewa sifa za binadamu hupewa sifa za binadamu. Kwa mfano kitu ambacho kwa kawaida hakiwezi kutembea , kusema, kuzaa wala kufa kinaweza kupewa uwezo wa kutenda hivyo.

Complete Documents
Expanded Features

Popo mbili zavuka mto ( macho)
Popote niendapo ananifuata ( kivuli)
Maiti anasema bali waliomchukua wamenyamaa kimya ( chungu na mafiga)

**Dhihaka:** Hii ni mbinu nyingine ambayo hutumiwa katika fani kuwasilisha vitendawili. Katika mbinu hii maneno yanayotumiwa huwa na lengo la kumhujumu na kumdhihaki mtu. Nia huwa ni kumdharau au kumtweza, mtu hasa kwa maneno. Hii ni mbinu ambayo hutumiwa sana katika vitendawili. Kwa mfano:

Kitu kidogo kimemtoa mfalme kitini ( maja ndogo)

Mama mtu mweusi, watoto wekundu ( pilipili)

Bwana mkubwa ameanguka na makobamakoba yake ( mbuyu)

**Stiari**

Vitu vyenye hulka mbalimbali hulinganishwa.

Mifano:

Samaki wangu anaelea kimgongomgongo (merikebu)

Kuku mweupe hufanya harusi (chumvi na umuhimu wake)

**Usanii**

Katika kuchambua vitendawili usanii uliotumika ni kipengele ambacho hakiwezi kupuuzwa. Kitendawili hakiwi kitendawili iwapo lugha iliyotumika haikupangwa kwa mpangilio maalum wa kisanii. Usanii hapa unamaanisha ujuzi na uwezo wa kueleza au kutoa jambo kwa ufundi kwa kuvutia. Vipengele vya lugha vinavyotumiwa katika vitendawili kama tulivyodokeza hapo awali ni kama tamathali za semi, matumizi ya picha, lugha ya mkato na ushairi.

Baada ya kuchambua maana na matumizi ya lugha katika vitendawili, ni muhimu pia kuzingatia dhima ya vitendawili. Lengo la kila kitendawili ni kutoa maudhui au mafundisho fulani. Kwa mfano katika kitendawili kama:-

Complete Documents
Expanded Features

Tumekwenda wawili, nimerudi mmoja ( mgeni).

Kitendawili hiki kinatueleza kuwa katika jamii hii ni muhimu kusindikiza wageni.

Mfano mwingine ni;-

Chaka langu halina ubaridi

(nywele)

Kitendawili hiki kinasisitiza umuhimu wa usafi wa mwili. Dhima nyingine ya vitendawili ni kufunza wanajamii wake adabu njema. Kwa mfano;-

Rudi nyuma nikuonyeshe ( mavi ya mlevi)

Hapa tunaona kuwa wanajamii wanakanywa dhidi ya kuwa walevi wasije wakafanya vitendo vya aibu. Mfano mwingine ni ukichukua mama chukua na mtoto ( fagio). Katika kitendawili hiki uhusiano wa mtoto na mama unasisitizwa. Kwa kutumia kitendawili hiki wanaume wanahimizwa kuwa iwapo wataoa wanawake ambao wana watoto tayari, itawabidi wachukue watoto na mama yao kwa sababu hawawezi kutenganishwa.

## Hitimisho

Katika mhadhara huu tumejaribu kuangalia maana ya semi, vipera vyake, na tukajikita katika kuangalia kipera kimoja tu cha vitendawili. Katika kuangalia vitendawili, tumeangalia maana yake, muundo wake, usanii wake pamoja na maudhui yake. Katika kuangalia maudhui tumejikita katika kuangalia dhima yake kwa maisha ya wanajamii. Zaidi ya hayo tumeonyesha vipengele ambavyo vyapaswa kuzingatiwa wakati wa kuchambua vitendawili.

Kwa kurejelea vitendawili katika jamii yako jadili;-

(i) Maana yake
(ii) Usanii wake
(iii) Dhima yake kwa maisha ya wanajamii

Expanded Features
Complete Documents

## MAREJELEO

Farsi S.S (1958) Swahili Sayings Kenya. Nairobi: Kenya Literature Bureau

Finnegan R. (1979) Oral Literature in Africa
Nairobi: Oxford University Press

Hamad, A.K (1981) "Tanzu za Fasihi Simulizi." Misingi Ya Nadharia ya Fasihi. Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni. Zanzibar

Khatibu, M.S (1978) "Vitendawili- Fani ya Fasihi Simulizi". Mulika Na. 13. Jarida la Tuki. Dar- es-Salaam.

Kirumbi, P.S (1976) Misingi ya Fasihi Simulizi. Nairobi: Shungwaya Publishers

Kuhenga, C. (1977) Tamathali za Usemi. Dar-es-Salaam: East Africa Literature Bureau.

Mbughuni, P. (1983) "Riddles, food for thought". Kiswahili Tol. 50/1 Jarida la Tuki Dar-es-Salaam

Mulokozi, M.M. (1989) "Tanzu za Fasihi Simulizi" Mulika Na. 21. Jarida la Tuki Dar-es-Salaam

Mwansoko, H.J.M (1988) "Mbinu za uchambuzi wa vitendawili". Mulika No. 20. Jarida la Tuki. Dar-es-Salaam

Nkwera F.M.V (1978) Sarufi na Fasihi. Sekondari na Vyuo. Tanzania Publishing House Dar-es-Salaam.

Senkoro F.E.M. (1988) "Vitendawili katika jamii. Maana, maudhui na matumizi yake" Mulika No. 17 Jarida la Tuki Dar-es-Salaam

Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala (1988). Kiswahili Sekondari Dar-es-Salaam.

## MHADHARA WA TISA

**Tanzu za Fasihi Simulizi**

**Methali**

Baada ya somo hili utaweza kueleza:

1. Maana ya methali
2. Muundo/usanii wa methali
3. Dhima ya methali
4. Uchambuzi wa methali

Dhana ya methali ni dhana ambayo imeshughulikiwa na wataalamu wengi na kwa hivyo fafanuzi za dhana hii ni nyingi.

Katika kuelezea dhana hii Omari (19) anasema:

> Methali ni sehemu ya lugha ambayo
> inaweza kufananishwa na kiungo cha

Expanded Features
Complete Documents

> lugha na kitoweo cha lugha pia……
> hutumiwa kwa kutafakari na kuyapima
> maisha kufunzia jumuiya na kutawalia
> jamii na mazingira ya binadamu. Methali
> hufunua falfasa ya jamii, hekima ya wale
> wanaoitumia katika mazungumzo yao.

Maelezo ya Omari yamejikita zaidi katika kufafanua dhima ya methali kuliko kutueleza maana yake. Ametueleza kuwa methali huwa na dhima ya kupima maisha na kufunza wanajamii kuhusu falsafa ya jamii husika. Mlacha (1981) naye katika kuchangia mjadala wa maana ya methali amesema:

> Kwa hakika methali ni mkusanyiko wa mambo
> mengi ujuzi wa lughashuhuda za vitendo
> matukio mbalimbali, kumbukumbu, hekima kubwa n.k.

Maelezo ya Mlacha (1981) yanatuelekeza kwa dhana kuwa methali husheheni maadili, mila, falsafa na mielekeo ya jamii ambayo huhifadhiwa kwa lugha ya ufasaha. Methali ni ngumu kueleweka na kufasirika hasa kwa ye yote ambaye ni mgeni katika jamii husika. Hapa inabainika kuwa methali hustawi vizuri katika hisia za watu wa utamaduni maalum. Hisia hizi hutofautiana kati ya jamii moja na jamii nyingine. Maelezo muafaka zaidi ya maana ya methali yametolewa na Mulokozi (1989:14) ambaye ameeleza kuwa:

> Methali n semi fupi fupi.
> Hueleza kwa muhtasari fikira
> au mafunzo mazito yaliyotokana
> na uzoefu wa kijamii. Mara
> nyingi maelezo hayo huelezwa kwa kutumia
> tamathali hasa sitiari na mafumbo. Methali
> ni utanzu tegemezi ambao kutokea kwake
> hutegemea fani zingine, kwa mfano maongezi
> au majadiliano mazito katika miktadha maalum
> ya kijamii. Baadhi ya methali huwa ni vielelezo au vifupisho
> vya hadithi fulani inayofahamika vizuri kwa wanajamii.

Maelezo ya Mulokozi (1989) yamenukuliwa kwa kirefu kwa sababu kwa mujibu wa maoni yetu, yamejumlisha sifa bainishi za utanzu wa methali. Sifa hizi zimeelezwa na Mtesigwa ( 1989: 2) kama:

Expanded Features
Complete Documents

(i) Usemi huo uwe mfupi na wenye
Urari wa maneno japokuwa maneno
Hayo si mepesi na ya kawaida.

(ii) Usemi huo ukubalike na watumiaji wa
lugha inayohusika hasa kwa sababu:

(a) Unalinganisha na kupatanisha vizuri mambo katika hali mbalimbali au zaidi zinazolenga ukweli ule ule
(b) Unatokana na maadili au vitendo vya kila siku vinavyochipuka kutoka katika jamii ya lugha ile.
(c) Unaleta maana au unatoa funzo mahsusi kwa watumiaji wa jamii inayohusika.

(iii) Usemi umwezeshe mwanajamii ang'amue maana yake ya ndani.

Kutokana na fafanuzi hizo zote kile kinachobainika ni kuwa methali ni semi fupi zenye maana nzito na huwa zimejaa hekima ndani yake. Semi hizi hutumia lugha ya mkato yenye mapigo maalum ambayo huleta ladha ya ushairi. Methali hutumia tamathali mbalimbali kama tashibihi, stiari, kejeli na chuku. Pia zinatumia lugha ya picha, viashiria n.k.

Methali huwa na maana ya ndani na ya nje. Katika muktadha huo methali zimeelezwa kama mafumbo ambayo yanahitaji ufafanuzi au ufumbuzi uli unaozingatia mazingira, hali na wakati. Methali huwa ni aina moja ya usemi ambao umekusudiwa kusema jambo maalum kwa njia ya fumbo. Methali ni sanaa ya maneno inayosanifu amali za jamii inayohusika kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi. Methali ni utanzu uliojaa uhai na wenye lugha yenye nguvu na maisha, urari wa maneno na busara nzito ya jamii. Methali huwa na sifa ya kuchora picha na kupatanisha picha hiyo na funzo. Sanaa ya methali hutegemea sana uteuzi wa maneno na ufundi wa kuyapanga ili kuwasilisha ipasavyo ujumbe unaokusudiwa.

Expanded Features
Complete Documents

Kwa hivyo twaweza kusema kuwa methali ni msemo unaotumiwa kuelezea kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili kutoa adili au onyo fulani kwa lengo la kushauri, kusifu, kuonya, kutahadharisha. Hali hii inaoana na maoni ya Nkwera (1978:97) kuwa:

> Methali ni semi au kauli
> zenye busara na mafunzo
> kuhusu maisha na mahusiano
> ya watu.

Methali huwa zinakariri ukweli fulani katika maisha ya wanadamu katika jamii fulani. Ukweli na umuhimu wa methali yo yote hutegemea mazingira inamotumika. Zinatumiwa kumjuvya mtu ukweli fulani au kumshtua apate kudadisi mambo au kujisahihisha anapokiuka matarajio ya jamii.

## Muundo wa Methali

Sentensi za methali huwa na muundo wa kipekee. Muundo huo husaidia kutofautisha methali na sentensi zingine . Methali nyingi huwa na muundo wenye sehemu mbili, sehemu ya kwanza ambayo huanzisha wazo na ya pili ambayo hulikanusha au kukamilisha wazo hili.

Muundo wa methali waweza kuangaliwa katika viwango viwili:

(i) Kiwango cha mpangilio
(ii) Kiwango cha maudhui

Muundo huu husaidia methali katika kuwasilisha maudhui yake na pia kuzifanya kueleweka kwa urahisi. Kila sehemu ya methali huwa na maudhui yake maalum. Picha ya sehemu moja haiwezi kujisimamia bila kuunganishwa na picha ya sehemu ya pili.

Kisintaksia methali huwa ni fupi sana. Ufupi wake huwa umefumbata matendo mapana sana yanayoweza kuelezeka kirefu kwa maneno ya kawaida. Ufupi wa methali ni

Complete Documents
Expanded Features

mpango ambao pia husaidia kuweza kuzikumbuka kwa urahisi zaidi na kupata ujumbe wa maadili yake vyema.

Sentensi za methali kwa kawaida huwa hazibadiliki. Maneno yanayofanya sentensi ya methali kuwa kamili mara nyingi ni yale yale. Mpangilio wa maneno ya methali inapobadilishwa ni pale tu msanii ana nia nyingine tofauti iwapo si kutojua methali anayotumia.

Methali huwa na sehemu mbili muhimu. Kila sehemu huzingatia jambo fulani ambalo linafanya methali iweze kukamilika. Sehemu ya kwanza mara nyingi huweza kutumika badala ya methali nzima lakini sehemu ya pili ni nadra sana ijisimamie kivyake. Sehemu ya kwanza mara nyingi huwa ndefu zaidi kuliko sehemu ya pili. Urefu huo unatokana na ukweli kwamba ndiyo chanzo au kiini cha methali nzima. Kwa sababu ya dhima hiyo sehemu hiyo inapaswa kufafanua zaidi ujumbe unaolengwa katika methali. Sehemu ya pili ni fupi kuliko ya kwanza. Sehemu ya pili hueleza matokeo ya kufanya vile ulivyoelezwa kwenye sehemu ya kwanza. Mifano ya mpangilio huu unadhihirika katika methali nyingi. Kwa mfano:

Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.
Ukienda kwa wenye chongo,
fumba lako jicho.

Hata hivyo kuna methali chache ambazo hazifuati mpangilio huu. Kuna baadhi ya methali ambazo sehemu ya pili huwa ndefu kushinda sehemu ya kwanza ama sehemu zote huwa sawa. Kwa mfano:

Hasira hasara
Chema chajiuza kibaya chajitembeza.

Methali hizi mbili zina sehemu sawa. Mifano ya methali ambayo sehemu ya pili ni ndefu kushinda ya kwanza ni:

Complete Documents
Expanded Features

Baniyani mbaya, kiatu chake dawa.

Masikini haokoti, akiokota huambiwa kaiba.

## Muundo Kimaudhui

Katika methali kuna sehemu mbili kimaudhui. Sehemu ya kwanza hutoa maelezo ya kitendo au matendo ambayo iwapo yatatokea kitendo cha pili kitatokea. Kwa hivyo sehemu ya kwanza huwa ni matayarisho na sehemu ya pili ni tegemeo.

Usipoziba ufa, utajenga ukuta." Katika methali hii mtu anaonywa kuwa asipozuia madhara yanapoanza hana budi kukabiliana na hasara kubwa baadaye.

Muundo mwingine wa kimaudhui katika methali ni ule wa kutumia tamathali. Tamathali hutawala sana umbuji wa methali kwa vile karibu methali zote hutumia tamathali. Muundo wa kimaudhui unaangalia vitendo viwili tofauti. Kitendo cha kwanza kinakuwa kimetayarishwa kama msingi. Kitendo cha pili kinategemewa kutokea iwapo kitendo cha kwanza kitafanywa.

## Usanii katika Methali

Methali huwa na urari wa maneno, busara na mvuto wa lugha. Methali hutumia tamathali mbalimbali za usemi. Methali hulinganisha hali mbili tofauti. Hali hizi huwezekana kwa vile methali huwa na sitiari ndani yake. Baadhi ya mbinu zinazotumiwa kuwasilisha ujumbe wa methali ni:-

### (i) Tashibihi

Kama tulivyodekeza katika vitendawili, tashbiha ni tamathali ambayo hulinganisha watu au vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno kama 'kwamba, na 'mithili ya' ( Senkoro 1982:14): Mifano ya methali zinazotumia mbinu hii ni:

Utajiri ni kama umande

Ujana ni kama moshi

Ufalme ni kama maua

Complete Documents
Expanded Features

Kunga nyingine inayotumika katika methali ni

**(ii) Stiari**

Sitiari kama tashbiha hulinganisha vitu viwili ama watu wawili bila kutumia viunganishi-linganishi. Katika mbinu hii vitu na watu hulinganishwa kama kwamba watu au vitu hivyo ni sawa kabisa. Kwa mfano:

Mapenzi ni majani, huota popote
Kukopa arusi, kulipa matanga
Ulimi ni upanga

(3) **Balagha/Chuku**

Mbali na matumizi ya sitiari kuna matumizi ya balagha na chuku. Katika mbinu hii maneno hutiwa chumvi. Lengo la chuku ni kutilia mkazo. Methali hutumia maneno ambayo yana mchomo fulani wa kuibua hisi maalum. Maneno hayo huwa yamechaguliwa kwa uangalifu kuibua hisia na kusisitiza ujumbe au funzo lililokusudiwa katika methali. Mfano wa matumizi haya ni 'Chovya chovya humaliza buyu la asali'.

## Kejeli

Kejeli ni mbinu ambayo hutumiwa kwa lengo la kumdharau, kumchekelea au kumfanyia mzaha mtu. Kuna methali ambazo maneno yake yakitazamwa kwa juu juu hupingana na ukweli unaojidhihirisha katika hali ya kawaida. Kwa kutazamwa kiholela unaonekana kama kichekesho au upuuzi lakini yakiangaliwa kwa makini na kwa undani zaidi ukweli na busara yake hubainika.

"mfinyanzi hulia gae"
Hindi ndiko kwenye nguo na
Wendapo uchi wako
Wagombanao hupatana

Expanded Features
Complete Documents

Methali nyingine huundwa kutokana na vidokezo au matukio halisi katika jamii. Baadhi ya methali hutumia matukio ama hadithi. Matukio yanayotumiwa ni yale yenye misingi yake katika historia ya jamii hasa yale ambayo yaliachia jamii kumbukumbu au funzo fulani.

Mbinu hii imetumiwa sana hasa katika methali za makabila mbalimbali. Kwa mfano katika jamii ya Wakikuyu tuna methali.

Ciakorire Wacu Mugunda

Zilimkuta Wacu kwa Shamba.

Methali hii iliundwa kutokana na kisa cha mwanamke mmoja kwa jina Wacu. Mwanamke huyu alikuwa hapendani na mumewe ambaye alikuwa na bibi mwingine. Siku moja Wacu alienda shambani na mumewe na bibiye waliamua kuchinja mbuzi ili wakule kabla ya Wacu kutoka shambani. Baada ya mumewe Wacu na bibiye kuchoma mbuzi, mwewe alikuja na akachukua kipande cha nyama kwa jina "ngerima" ambacho ndicho kilithaminiwa sana na jamii ya Wakikuyu.

Hata hivyo kwa vile nyama hiyo ilikuwa na joto jingi, mwewe alishindwa kustahimili joto la nyama hiyo, ikaanguka karibu na Wacu ambaye alikuwa analima. Wacu alichukua nyama hiyo na akakaa chini na kuila kwa furaha. Methali hiyo iliundwa kwa kuwafunza wanajamii kuwa bahati ya mtu haiwezi kuzuiliwa.

Katika Kiswahili tuna methali kama, " ukienda kwa wenye chongo nawe fumba lako jicho".

Mshika mbili moja humponyoka
Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

Methali huvutia zaidi iwapo inatolewa kwa maneno machache au mafupi. Kwa mfano:-

Expanded Features
Complete Documents

Mla, mla leo mla jana kalani?

Neno lililopigiwa mstari limefupishwa. Methali pia hutumia lugha ya ushairi au lugha yenye mapigo ya kimuziki mifano:

Haba na haba hujaza kibaba
Hasira hasara
Mpanda hovyo hula ovyo

Mapigo huweza kujitokeza katika umbo la takiriri. Mbinu hii mbali na kusisitiza ujumbe husisitiza hisi na wakati, na kwa njia hiyo maana ya methali hujifunua wazi zaidi mifano:

Haraka haraka haina baraka
Bandu bandu humaliza gogo
Chukururu si ndo ndo ndo.

Je methali zina dhima gani katika jamii?

## Dhima ya Methali

Kama Mlacha (1981) anavyodokeza matumizi na madhumuni ya methali hayana kipimo. Kinyume na hadithi na vitendawili ambavyo hutumiwa katika nyakati na mazingira maalum hususa saa za jioni baada ya kazi nzito ya mchana kutwa methali hutumiwa katika nyakati na mazingira mbalimbali na hali zote. Kutoka enzi za mababu zetu, Waafrika wamekuwa wakitumia methali katika furaha na starehe zao, huzuni na misiba yao na kazi na shughuli zao zilizowasibu na kuwahusu katika maisha na uhai wao wote.

Expanded Features
Complete Documents

Kwa hivyo methali zimetumiwa kama ghala na kielezo thabiti cha utamaduni wa Mwafrika kinachoeleza utamaduni wake, mila, desturi na miiko ya jadi yake. Methali hutumiwa kama njia moja ya kujenga mandhari ya kuaminika kuhusu jamii inayotumia methali hizo. Kwa mfano katika riwaya ya Achebe ya Shujaa Okonkwo (1973) na ya kezilahabi Gamba la Nyoka (1978) methali zinatumiwa kujenga uhalisia wa mandhari na utamaduni wa jamii zinazohusika.

Mlacha (1985) anatueleza kuwa methali zina maadili ambayo humsaidia mwanadamu kwa kumwongoza kwenye misingi bora ya maisha. Anaendelea kueleza kuwa kuna methali za aina mbili:

(1) za masuto
(2) za mauidha

Methali za mauidha zimeelezwa kuwa zile zenye lengo la kuonya, kuusia kushauri na kufunza. Methali za masuto zina lengo hilo lakini maneno yake huwa ya kukaripa na hata kukemea. Maneno ya methali hizi huwa makali kwa masikio na yanapotumiwa katika lugha ya kawaida huashiria dalili ya utovu wa nidhamu au heshima au lugha ya adabu. Maneno hayo huwa hayatumiwi mbele ya umati wa watu au watu wazima au wageni.

Aina zote mbili za methali huwa zinalenga kwenye ukweli wa maisha. Zinatolewa kutoa maonyo, mafundisho na husaidia kurekebisha tabia za watu wa jamii moja. Methali za mauidha hujumuisha hali za kupongeza au kuunga mkono, kufariji na kuhimiza wanajamii waongezi juhudi katika kazi zao. Methali za masuto huwa na nia ya kushambulia matendo mabaya kwa nia ya kumrekebisha mtu na katika kutimiza lengo hilo mbinu ya kejeli yaweza kutumiwa.

Dhima kuu ya methali ni kufunza na kumlea binadamu ili aoane na matakwa ya jamii yake. Methali pia hutumiwa kwa dhima ya kukashifu matendo mabaya. Kukashifu mara nyingi hufanywa kwa mbinu ya kejeli. Methali hutumiwa kumkejeli mtu ama kumsema

Expanded Features
Complete Documents

kwa maneno ya dharau, mzaha na kumsimanga . Kejeli katika methali huonyesha zaidi kutofaulu kwa matendo. Kwa mfano:

Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
Mpanda ngazi hushuka
Aliye juu mngonjee chini

Matendo mabaya pia hushtumiwa kwa kutumia methali. Kwa mfano:

Fadhili ya punda ni mateke.

Methali pia hutumiwa kuonya na kutahadharisha. Methali zinazotumiwa kwa lengo hili huwa zimejikita kwenye hekima na falsafa ya maisha. Kwa mfano:

Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

Methali za kuonya na kutahadharisha zaweza kutumiwa kwa kujikosoa au kwa kujuta. Methali hizi humfanya mtu aweze kuoana yale yanayoweza kumfika na hivyo anashauriwa ajitahadharishe mapema ili kuepuka balaa.

Mbali na kuonya, methali hutumiwa kufariji, kuliwaza na kupongeza. Binadamu katika harakati za kujiendeleza hukabiliwa na matatizo mengi. Matatizo hayo huweza kumfanya mtu akate tamaa na hali hiyo yaweza kuwa kikwazo kwa maendeleo ya jamii. Katika mazingiria ya aina hiyo jamii nyingi zimezua methali kujaribu kutuliza wanajamii ambao huenda wakatamauka kabla ya kutimiza miradi yao. Mifano ya methali za kuhimiza ni:

Baada ya dhiki faraja
Hakuna refu lisilo na ncha
Mstahamilivu hula mbivu

Pamoja na kuliwaza na kufariji methali hutumiwa kwa nia ya kupongeza matendo mazuri na umuhimu wa kuongeza juhudi.

Mfano:

Kidole chema huvishwa pete
Mtaka cha mvunguni sharti ainame

Complete Documents
Expanded Features

Kinga na kinga ndipo moto uwakapo

Methali zingine hutumiwa kuonyesha uhusiano unaotarajiwa miongoni mwa wanajamii. Methali hizi huonyesha tabia zinazopaswa kuwepo kati ya wanajamii k.m.

Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

Methali hii inatumiwa kuwaeleza vijana kuwa ni wajibu wao kuchukua maoni ya wazee kwa makini kwani wasipofanya hivyo huenda wakapatwa na maafa katika maisha yao.

Methali ya:
Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu

Methali hii inahimiza watoto wachukue mafunzo wanayopewa na wazazi wao ama sivyo ulimwengu unawangoja. Mafunzo ya ulimwengu huwa na maafa yake. Uhusiano kati ya watu wa aila moja pia unasisitizwa kwa kutumia methali k.m.

Damu nzito kuliko maji
Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe

Methali za sampuli hii huwa na dhima ya malezi ya udugu na urafiki. Katika muktadha huu methali zaweza kuchukuliwa kama picha ya maisha kwa ufupi, ukweli wa namna ya kuishi na watu wa jamii yako.

Methali zina kumbukumbu ya dini, uchawi, ndoa, serikali, sheria, au jambo lo lote la asili ambalo linaingia kwenye maisha ya jamii. Methali hujumlisha mafundisho makubwa kuhusu raha, taabu mabaya au mazuri.

Dhima nyingine ya methali ni kupamba lugha au maongezi. Kama tulivyodokeza hapo awali, methali hutumia picha kama njia ya kufumba hekima. Methali pia hutumia kinga ya marudio-rudio ili kusisitiza ujumbe na kuingiza falsafa na hekima ndani yake. K.m.

Moto hauzai moto
Mwana wa nyoka ni nyoka

Marudio ya aina hii husababishwa na ukweli wa hali ya maisha lakini kuna marudio mengine ambayo hutumiwa kwa nia ya kuongeza ladha ya lugha katika sentensi kwa kurudia maneno yanayofanana kwa mfululizo:

Haba na haba hujaza kibaba

Haraka haraka haina baraka

Ndu ndu ndu si chu ru ru

Ukijua huu huu hujui

Complete Documents
Expanded Features

**Uchanganuzi wa Methali**

Katika kuchambua methali ni muhimu kuelewa kuwa methali ni mafumbo ambayo yanahitaji ufumbuzi. Katika juhudi za kufumbua methali ni muhimu kuelewa kuwa mawazo ya methali huwa yameshikana na utamaduni, desturi na hadhi ya jamii maalum. Kwa hivyo uchambuzi wa methali huhitaji ujuzi wa utamaduni na mazingira yaliyozaa methali. Ukweli unaopatikana kwenye methali nzito na maana yake hueleweka tu kwa mtu ambaye ana ujuzi wa mila, desturi, itikadi, falsafa na mienendo ya jamii iliyozaa methali.

Methali huwa na maana ya wazi na maana fiche na mchambuzi wa methali apaswa kuzingatia maana hizo zote.

Mbali na kuchambua maana ya methali, mchambuzi hupaswa kuchambua matumizi ya lugha katika methali. Methali tumeshaona kuwa hutumia lugha ya kipicha pamoja na tamathali za usemi pamoja na ishara mbalimbali. Ili kufanikisha uchambuzi ni muhimu kuchunguza tamathali za usemi zilizotumika katika kuwasilisha ujumbe katika methali. Mbinu za uwasilishaji wa maudhui ya methali ni nyingi. Kuna matumizi ya tashibha sitiari, kejeli, balagha, chuku, tanakali za sauti na ishara mbalimbali. Mchambuzi wa methali apaswa kuchunguza kunga hizi zote na dhima zake katika kufanikisha ujumbe wa methali.

## MAREJELEO


Abudu, M. (1974) Methali za Kiswahili. Maana na matumizi. Kitabu cha kwanza Nairobi: Foundation Books Ltd

__________ na Baruwa A. (1981) Methali za Kiswahili. Kitabu cha pili na cha tatu.. Nairobi: Shungwaya Publishers

Achebe, C. (1973) Shujaa Okonkwo. Nairobi: East African Publishing House.

Balisdya, M.L. (1981) “Tanzu za Fasihi Simulizi” Misingi ya Nadharia ya Fasihi. Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni. Zanzibar

Kezilahabi, E. (1978) Gamba la Nyoka Arusha: E.A Publications

Kirumbi, P.S (1975) Misingi ya Fasihi Simulizi. Shingwaya Publishers.

Nairobi Kuhenga, C. (1977) Tamathali za usemi. Dar-es-Salaam : E.A L.B

Mlacha, S.A.K. 91985) “Dhima ya methali katika malezi” Kiswahili. Juzuu 52/1 and 52/2 Janda la TUKI Dar-es-Salaam

Complete Documents
Expanded Features

(1981) “Methali kama chombo muhimu katika jamii”. Makala ya Semina ya Fasihi simulizi TUKI Dar-es-Salaam
Msuya, P.A (1977) “Fasihi ya Methali” Mulika Na. 9 Jarida la TUKI. Dar-es-Salaam
Mtesigwa, P.C.K. (1989) “Methali ni nini?”. Kiswahili Juzuu 56. Jarida la TUKI Dar-es_Salaam
Mulokozi, M,M (1989) “Tanzu za Fasihi Simulizi”. Mulika na 21. TUKI Dar-es-Salaam
Ngole, S.Y.A na Honero, L (Wahariri) (19820. Fasihi Simulizi ya Mtazania: Methali TUKI Dar-es-Salaam
Nkwera, F.M.V (1978) Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo. Dar-es-Salaam. Tanzania Publishing House.
Parker, A.C (1981) “Tamathali za usemi katika methali za Kiswahili. Takiriri” Makala ya Semina ya fasihi simulizi Dar-es-Salaam: TUKI
Senkoro, F.E.M.K. (1982) Fasihi Dar-es-Salaam: Press and Publicity Centre,

## MHADHARA WA KUMI

**Tanzu za Fasihi Simulizi**
**Ushairi Simulizi – Nyimbo**

Baada ya mhadhara huu utaweza kueleza;-

(i) Maana ya ushairi simulizi

(ii) Maana ya nyimbo usanii, maudhui na dhamira ya nyimbo

(iii) Aina ya nyimbo na dhima yake kwa wanajamii

Katika kufafanua dhana ya ushairi katika muktadha wa fasihi simulizi, Balisdya Matteru, 1987:4) amesema:

> Ushairi: Ni fungu
> linalojumlisha tungo
> zote za fasihi simulizi
> zenye kutumia mapigo: Kwa utaratibu maalum.
> mapigo ya kimziki
> Mathlani mapigo hayo yaweza kupangwa kwa muwala wa urari………”

Anaendelea kueleza kuwa

> “ama mapigo
> hupangwa kufuatia
> mapigo ya kazi,
> mdundo wa ngoma
> au ala nyingi

Complete Documents
Expanded Features

za muziki,
makofi na miondoko
ya uchezaji".

Maoni ya Balisdya Matteru (1987) yameendelezwa na Mulokozi (1989:7) ambaye anatueleza kuwa

Ushairi katika
fasihi simulizi
hupambanuliwa
na lugha ya kawaida
kwa namna unavyopanga
na kutumia lugha
na mbinu za
kimuktadha.
Kauli za kishairi
Hupangwa kwa
Kufuatia wizani
(rhythm) maalumu,
mawimbi ya
sauti na mara
nyingi lugha ya
mkato na mafumbo hutumika. Vile
vile uimbaji au
maghani ( badala
ya usemaji) pengine
hutumika
kuwasilisha shairi
kwa hadhira.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa kile kinachobainika ni kuwa ushairi ni aina ya fasihi inayotofautiana na hadithi na tamthilia hasa katika umbo na matumizi yake ya lugha. Ushairi hutumia lugha ya mkato yenye kueleza maudhui yake kimuhtasari na huyaficha maudhui hayo ndani ya taswira na ishara. Mara nyingi ushairi hutumia maelezo ya muhtasari na yenye kuachana na sarufi na mpangilio wa lugha wa nje na wa kila siku. Muhtasari wa maelezo huweza kufikiwa kwa njia mbali mbali. Njia kuu mbili ni ile ya tamathali, picha na ishara.

Mbali na ushairi kuwa na mapigo ya kimuziki, mpangilio maalum wa maneno na mkato wa maelezo , ushairi huwa na ladha katika mlio. Mlio uletao ladha katika ushairi huweza kupatikana kwa njia nyingi. Njia moja kuu ni kutumia vina. Wakati mwingine mlio

Complete Documents
Expanded Features

hupatikana kwa kutumia takiriri, tanakali na mrudiorudio wa maneno. Pamoja na hayo ushairi huwa na maudhui. Maudhui hayo yaweza kuwa mazito ama mepesi.

Utanzu wa ushairi wa fasihi simulizi hujumlisha nyimbo na maghani ya aina mbali mbali.

Kwa hivyo kutokana na maelezo hayo twaweza kubainisha ushairi simulizi kwa kuzingatia sifa zifuatazo:-

(i) Kuwepo kwa mapigo yenye utaratibu maalum wa kimuziki.
(ii) Matumizi ya lugha ya mkato yenye kujenga picha na tamathali aidha yenye mpangilio maalum.
(iii) Kuwepo kwa mvuto katika mlio ili kuleta ladha.

Mapigo ya kimuziki hujitokeza katika sura tofauti katika tenzi na mashairi. Mapigo huhesabiwa kwa urari wa mizani. Mapigo huweza kufuata mshindo wa kazi, mwendelezo wa mawazo na utoshelevu wa sentensi ama kauli zilizo ndani ya utungo.

Lugha ya mkato hutokana na matumizi ya picha taswira, tamathali za usemi hususan picha za ashirio. Aidha lugha ya mkato hujengwa kwa kutumia mipangilio mbali mbali ya maneno inayokata na kupunguza idadi ya maneno katika kueleza jambo. Mvuto na mlio wa shairi kama tulivyodokeza hapo awali hutokana na matumizi ya vina, takiriri na taathira za tanakali za sauti.

Vipera vya ushairi kama tenzi, mashairi, nyimbo n.k. hutofautiana kwa vipengele vichache vichache hapa na pale. Aidha tofauti hizo zipo katika vigezo vya ushairi vinavyotumiwa. Vipera hivyo ni;-

## Nyimbo

Wataalamu kadhaa wametoa maana mbalimbali ya nyimbo Mulokozi (1987: 7). Amesema kuwa

“wimbo ni kila
kinachoimbwa

Complete Documents
Expanded Features

Maelezo ya Mulokozi hayajatueleza kinagaubaga maana ya wimbo. Katika kuchangia mada hii Matteru katika makala yake yaitwayo "Fasihi simulizi na uandishi wa Kiswahili", amesema:-

nyimbo ni aina
ya ushairi
unaoimbwa
peke yake
au kwa kuhusishwa
na ngoma au
pia na kucheza
kwa mwimbaji
wake.

Maelezo muafaka zaidi kuhusu maana ya nyimbo yanapatikana katika makala ya Matteru (1987: 6) anapoeleza:-

Nyimbo ni tungo
za kishairi
zenye kutumia
mahadhi, melodia,
mkongojo, mapigo
na muwala. Nyimbo
huweza kuimbwa na
mtu mmoja pekee ama na wazumi
wake wakiitikia
mkarara.

Kuhusu mpangilio wa nyimbo, Matteru anaeleza kuwa:

Nyimbo zina mfuatano
au mpangilio maalum
wa sauti, mwendo,
picha na ishara.

Thonya anaelekea kukubaliana na Matteru anaposema ( Nyimbo).

…..ni aina ya ushairi uliotiwa
sauti na
uliokusudiwa
kuimbwa na
kuleta maana
ya ujumbe
kwa jamii.

Expanded Features
Complete Documents

Freuchen (1962: 321) katika kuchangia maelezo ya nyimbo asema:

> Nyimbo ni mawazo yanaoimbwa na watu baada ya kusukumwa
> na nguvu maalumu. Mawazo hayo hayawezi kutolewa kwa
> hadhira katika mazungumzo ya kawaida yakaeleweka
> ama kuleta athari iliyokusudiwa……..mawazo
> ya mwanadamu yanasukumwa na nguvu maalum
> iliyozingirwa wakati huo kama
> vile furaha, hofu, uchungu………..mawazo yaweza
> kumfurika mtu kichwani na
> kumfanya apumue kwa mashaka na moyo kumdunda.
> Mwanadamu hujikuta Akiathirika kwa namna fulani………
> halafu kunakuwa na matukio mapya.Maneno yatakayohitajika
> katika kulieleza
> Tukio hili
> Jipya yatajitokeza
> Yenyewe. Maneno
> Hayo ndiyo yatakayounda
> Wimbo mpya".

Freuchen anasisitiza dhana kuwa kazi ya kisanaa kama wimbo haina budi kutokana na mazingira. Mazingira ndiyo yanazalisha hisia na hatimaye mawazo kwa msanii wa wimbo ili aweze kufanya kazi yake. Maelezo tulionukuu yanatudhihirishia ugumu ulioko katika kueleza dhana ya nyimbo (wimbo). Hata hivyo maelezo tuliotoa yanatupa fununu kuhusu sifa za nyimbo. Mulokozi (1989:9) ametoa sifa hizo hivi:-

(i) Muziki wa sauti ya mwimbaji au waimbaji
(ii) Muziki wa ala ( kama ipo)
(iii) Matini au maneno yanayoimbwa
(iv) Hadhira inayoimbwa
(v) Muktadha, unaofungamana na wimbo huo kwa mfano sherehe, ibada, kilio n.k.

Kwa hivyo katika nyimbo, panapaswa kuwa na wazo maalumu ambalo linawasilishwa kwa hadhira husika kwa njia ya sauti. Sauti zinazotumiwa hutofautiana katika mwendo wake wa kuimbwa. Pia nyimbo zapaswa kuwa na mpangilio maalum. Nyimbo zinapoimbwa hutumia vipengele vingi katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wake kwa hadhira inayolengwa. Vipengele hivyo huwa si maneno au mazungumzo wala ni vidokezo, miguno miliolio, toni, vituo na kiimbo.

Complete Documents
Expanded Features

## Maudhui ya Nyimbo

Nyimbo zimejikita katika kutoa mafundisho ya hekima, malezi na busara za wahenga. Nyimbo zingine zilitokana na kusifu mafanikio fulani katika jamii k.m. ushindi wa kazi, ushindi katika vita na kadhalika.

Nyimbo pia zilitumiwa kukashifu kundi fulani ambalo lina tabia isiyoridhisha. Nyimbo zingine zilimbwa kwa lengo la kupunguza uchovu na udhia baada ya wanajamii kufanya kazi mbalimbali hasa kazi za sulubu. Nyimbo nyingi zilichota maudhui kutoka kwa shughuli za kijamii kama mtoto kuzaliwa, mvulana kubalehe au msichana kuvunja ungo, kijana kuoa na mwali kuolewa, sherehe, mtu kujinusurisha na majanga na mikasa k.m. mipao na ngoma za virombo, yaani ngoma na ibada za kuchumbua na kupunga mashetani; mtu kuuguzwa na hatimaye mtu kuliliwa anapofariki n.k. ( Nkwera 1978:87). Maudhui ya nyimbo hutegemea hadhira inayolengwa. Hadhira katika nyimbo yahusu watu licha ya kuwa hata vitu vingine visivyokuwa watu, navyo vyaweza kuwa hadhira ya nyimbo hizo. Pale ambapo hadhira si binadamu, binadamu huwa hadhira fichu ( indirect audience) ambayo hatimaye itabidi iathirike kutokana na maadili yanayopatikana katika nyimbo. Kuna aina nyingi za hadhira. Kuna hadhira ya mtu mmoja hadi mamilioni. Pia kuna hadhira za aina mbalimbali, hadhira za watoto, vijana, wazee, wanawake waume na kadhalika.

## Dhamira za Nyimbo

Je nyimbo huwa na dhamira gani?

Dhamira ni kiini cha suala linaloshughulikiwa na mtunzi katika kazi ya fasihi. Ni wazo mahsusi katika kazi hiyo. Mawazo yanayoshughulikiwa yaweza kuwa makuu au madogo. Katika nyimbo ni muhimu dhamira zioane na hadhira ili ujumbe uliokusudiwa uweze kupokelewa ipasavyo. Kwa hivyo ni wajibu wa msanii kupima hadhira yake na kusanifu nyimbo zake kulingana na hadhira anayolenga.

Kwa kutumia kigezo cha maudhui na dhamira kuna nyimbo za aina nyingi kama bembea, tumbuizo, ngoma za mavigani, za michezo ya kawaida na za siasa.

Complete Documents
Expanded Features

Pia kuna nyimbo ambazo huimbwa kwa kutumia vyombo/ala za muziki au bila kutumia vyombo/ ala hizo.

## Aina za Nyimbo

Mulokozi (1984:89) ametoa makundi kumi na tano kama ifuatavyo:

(1) Tumbuizo-nyimbo za furaha ziimbwazo kuwafurahisha watu wenye matukio mbalimbali k.m. ngomani au harusini
(2) Bembea ( bembelezi)
Nyimbo za kubembeleza watoto
(3) Kongozi-
Nyimbo za kuaga mwaka katika jamii ya Waswahili
(4) Nyimbo za dini k.m. Kasida za kumsifu mtume
Nyimbo za Wakristo za ibada za jadi n.k.
(5) Wawe- Nyimbo za kilimo
(6) Tenzi
Nyimbo ndefu za kimasimulizi au za mawaidha
(7) Tendi:-
Nyimbo ndefu za masimulizi juu ya matendo ya mashujaa
(8) Mbolezi:
Nyimbo za kilio au maombolezo
(9) Kimai
Nyimbo zinazohusu shughuli za baharini ( kimaji)
(10) Nyiso
Nyimbo za jandoni
(11) Nyimbo za vita
Nyimbo ziimbwazo na askari wakati wa vita
(12) Nyimbo za uwindaji
Huimbwa na makundi ya wawindaji na wasasi wakati wa shughuli au sherehe zao.
(13) Nyimbo za taifa ( anthems)
Nyimbo za kusifia taifa au kabila
(14) Nyimbo za watoto
Nyimbo ambazo watoto huimba wakati wa michezo yao.

**(15) <u>Nyimbo za Kazi</u>**

Hili ni kundi kubwa la nyimbo. Karibu kila kazi ifanywayo na watu huwa na nyimbo zake k.m. Kilimo ( wawe), kutwanga, kupepeta, kusuka, kuchuuza, useremala , uvuvi , uashi , ufuaji chuma, uchuuzi na kadhalika. Kutokana na mgao wa Mulokozi inabainika kuwa baadhi ya makundi ya nyimbo yaweza kuwekwa pamoja. Kwa mfano:

Expanded Features
Complete Documents

## Nyimbo za Kazi

Katika kundi hili twaweza kuweka nyimbo zote ambazo zinahusu kazi zinazofanywa na binadamu. Hapa tunapata nyimbo kuhusu kilimo, uvuvi, uwindaji, useremala na usukaji. Nyimbo hizi hutegemea kazi inayofanywa na watu katika nyakati mbalimbali. Nyimbo za kazi huwa katika makundi mbalimbali kulingana na kazi zenyewe. Kwa hivyo wakulima, wafinyanzi na wachuuzi watakuwa na nyimbo zao kulingana na kazi zao.

## Nyimbo za Watoto

Katika tapo hili tuna nyimbo za aina mbalimbali kwa mfano kuna nyimbo ambazo huimbwa kuwabembeleza watoto katika makabila mbalimbali. Nyimbo za kuoongelea watoto huwa na utaratibu maalum. Waswahili pamoja na makabila mengine ya Kiafrika huwa na desturi ya kuwaongoa ( kuwaimbia) watoto wao wachanga nyimbo nzuri ili wapate kulala au wapate kunyamaza ikiwa wanalia. Nyimbo hizo huimbwa kwa sauti nzuri na mahadhi mazuri yenye kupendeza masikio ya mtoto mchanga. Hali hiyo ndiyo iliyozua methali “wimbo mui huongelewi mwana”. Kwa mujibu wa imani ya Waswahili mtoto akiongolewa wimbo mzuri atakuwa mtoto mzuri na akiongolewa wimbo mbaya wimbo huo utamwathiri na akue kuwa mtoto mbaya mfano wa wimbo huu ni:-

Silie mama silie
ukilia waniliza
wanikumbusha makiwa
makiwa ya baba na mama
wanioza dume kongwe
halisafiri halendi
kazi kumega matonge ( Thonya, 978)

Mbali na nyimbo za kuwabembeleza watoto tuna nyimbo ambazo huimbwa na watoto wakati wa michezo yao. Watoto hutumia nyimbo hizi kujiburudisha na kujitumbuiza wakati wanapojumuika pamoja kwa mfano:

Watoto wa mjini
wamezoea
wakiona DISCO

Expanded Features
Complete Documents

wanadoea
wakiulizwa nini
Nataka mdundiko
Mdundiko
Mdundiko
Havinitishi tishi tishi
Havinibaishi , ishi, ishi
Ule mpango vipi,
Vipi?
Vipi?
(Balisdya Matteru, 1987:5)

### Nyimbo za Ngoma

Aina nyingine ya nyimbo ni nyimbo za ngoma. Nyimbo hizi huimbwa kwa lengo la kujifurahisha katika mikutano au sherehe mbalimbali. Nyimbo hizi huimbwa wakati wa kucheza ngoma. Hadhira ya nyimbo hizi huwa ya aina mbili:-

(i) Wale watazamaji wa ngoma ambao wanatazama na kusikiliza wakiwa wana nia ya kupata ujumbe unaowasilishwa katika nyimbo hizo.

(ii) Wale wanaocheza ngoma

Jamii ya Wakamba ni mfano wa jamii ambayo ina sifa sana kwa upande wa nyimbo za ngoma.

Pamoja na nyimbo hizo tuna nyimbo za tohara, harusi, jando unyago na mazishi. Maudhui ya nyimbo hizi huoana na sherehe inayohusika. Kwa mfano nyimbo za harusi huonyesha umuhimu wa ndoa katika jamii na pia husifu bibi na bwana harusi. Nyimbo za tohara husisitiza umuhimu wa tohara na kuhitimu kuwa mtu mzima. Maudhui ya nyimbo hizi hujikita katika lengo maalumu. Huwa ni kuwapa moyo na kuwapa ujasiri ili waweze kukabiliana na tohara bila uwoga. Baadhi ya nyimbo husifu wale waliofuzu katika tohara bila uoga huku wakikemea wale walioonyesha dalili za uoga wakati wa tohara. Nyimbo za unyago na jando zaweza kuwekwa katika tapo hili. Nyimbo za jando na unyago hazipaswi kuimbwa nje ya mazingira yaliyokusudiwa. Katika jamii ya Waluhya, Wameru na Wakisii kuna nyimbo ambazo huimbwa baada ya wavulana kutiwa jandoni.

Complete Documents Expanded Features

## Hitimisho

Nyimbo za fasihi simulizi ni moja ya zana ama vyombo muhimu vya utamaduni ambavyo huelekeza na huonyesha wanajamii ni maisha yapi mazuri na ni yapi mabaya. Nyimbo hufichua mambo mengi katika jamii. Nyimbo zikitumiwa vyema zinaweza kuongoza jamii kufikia malengo yaliyokusudiwa na wanajamii. Nyimbo huelimisha, huburudisha na huonyesha maendeleo ya nchi, huhuzunisha na hutumiwa kuwalilia wale walioaga dunia.

Kutokana na dhima hizo za nyimbo, msanii wa nyimbo anapaswa kuelewa hadhira yake, aelewe lugha ya jamii husika. Lugha inayotumiwa katika nyimbo lazima iambatane na hekima, ufasaha na ukweli wa matukio kama vile masikitiko, huzuni, chuki, upendo, uchawi, na uzalendo.

Nyimbo pia zapaswa kwenda sambamba na mabadiliko ya kijamii kwa misingi ya uchumi, siasa, na utamaduni. Msanii wa nyimbo ana wajibu wa kujuhusisha kwa dhati na jamii yake kwa upande wa mawazo, matendo n.k. Nyimbo zikifuata mkondo huo zaweza kutekeleza lengo la mabadiliko yaliyokusudiwa katika jamii husika.

| |
|---|
| Kwa kuzingatia nyimbo katika kabila lako, eleza maana ya nyimbo, aina ya nyimbo na dhima ya nyimbo katika maisha ya wanajamii |

## MAREJEO


Abudu, M. na Baruwa A. (1981) Methali za Kiswahili Maana na matumizi. Nairobi :Shungwaya Publishers.
Balisdya, M.L. ( Bi Matteru) (1979-80) "Utafiti, mbinu na ukusanyaji wa fasihi simulizi na hatima Yake" Lugha Yetu Na. 34-36 BAKITA. Dar-es-Salaam (1981) Kitangulizi cha Fasihi Simulizi.Muswada

- Fasihi simulizi na uandishi wa Kiswahili ( Makala)
- "Preliminary Remarks on Song in Tanzania". ( Makala)
- (1987) "Tanzu na fani za Fasihi simulizi". Mulika na 19. TUKI. Dar-es-

Salaam Finnegan R. (1977) Oral Literature in Africa. London : Oxford University Press. Kirumbi P.S (1976) Misingi ya Fasihi Simulizi. Shungwaya Publishers. Nairobi
Momanyi C. (1989) Fasihi Simulizi. ( Makala)

Complete Documents
Expanded Features

Mulokozi M.M. (1989) "Tanzu za Fasihi Simulizi". Mulika na 21. TUKI Dar-es-Salaam
Musokile, M. (1981) "Nafasi ya Nyimbo za Fasihi simulizi katika jamii inayobadilika. Makala ya Semi ya Fasihi Simulizi. TUKI . Dar-es-Salaam
Nkwera, F.V.M. (1978) Sarufi na Fasihi. Sekondari na Vyuo. Tanzania Publishing House. Dar-es-Salaam
Thonya, L.M. (1978) Misingi ya Kiswahili. Dar-es-Salaam: Black Star Agencies.

## MHADHARA WA KUMI NA MOJA

**Tanzu za Fasihi Simulizi**
Ushairi Simulizi – Maghani
Baada ya mhadhara huu utaweza kueleza:-

(1) Maana ya maghani
(2) Vipera vya maghani
(3) Dhima ya maghani kwa wanajamii

Kama tulivyoeleza katika mhadhara uliopita, ushairi simulizi unaweza kugawanywa katika mapato mawili:-

(i) Nyimbo
(ii) Maghani

Kwa vile tumeshughulikia utanzu wa nyimbo sasa tutajikita kuangalia utanzu wa maghani.

Maghani ni nini?

Kwa maelezo ya Balisdya Matteru: (1987:7)

" Maghani ni tungo za kishairi
zilizokusudiwa kutongolewa
bila ya kutumia
melodia wala
mahadhi yo yote
bali hutongolewa
kwa kutumia sauti
kati ya uimbaji na

Complete Documents
Expanded Features

uzungumzaji ukisisitizwa
utumizi wa mapigo mwendo
na kasi inayohitajika
kiimbo ( cha sauti)
huwa ni muhimu katika
kutia ladha na hata maana.
Wakati mwingine kiimbo
kisichoenda juu
wala chini.
Pahali pengine sauti
ya juu na chini katika
kiimbo imetumika kuleta ladha
na uzito wa maana.

Katika utanzu huu wa maghani zinaingia fani nyingi za kishairi zinazotongolewa kama vile majigambo, na vighani vya watoto vya kazi. Hata hivyo Mulokozi (1989:9) anaeleza maghani kama ushairi unaotolewa kwa kalima badala ya kuimbwa. Anasema kuwa maghani ni ya aina mbili:-

(a) Maghani ya kawaida
(b) Maghani ya masimulizi ( narrative)

## Maghani ya Kawaida

Maghani ya kawaida hujumlisha fani mbali mbali za ushairi simulizi kama vile mashairi ya mapenzi, siasa, maombolezo kazi, na dini. Ushairi huo hughaniwa badala ya kuimbwa na kusemwa tu.

## Sifo

Sifo ni tungo za kusifu. Sifo nyingi husifu watu kama mashujaa, na watawala. Hata hivyo kuna sifo ambazo husifu vitu vingine kama wanyama, mimea, mnazi, na pesa. Mbali na kusifu, sifo zingine hukashifu na kukejeli. Vipera muhimu vya sifo ni:-

(i) Vivugo
(ii) Pembezi
(iii) Tondozi

**Vivugo ( Majigambo)**

Complete Documents
Expanded Features

Kivugo ni ghani la kujisifia. Kwa kawaida kivugo hutungwa na kughaniwa na mhusika ambaye analenga kujisifu yeye mwenyewe. Kivugo hutungwa kwa ufundi mkubwa kwa kutumia kunga kama istiari, vidokezo, ishara, takiriri na mara nyingine hutumia vina.

Yule anayejigamba ambaye mara nyingi huwa mwanamume hujitungia shairi lake ambalo lina misingi yake katika tuiko maalum katika maisha yake k.m kuingia jandoni, kuoa, kurjea kutoka vitani, kufanikiwa katika jambo ngumu kama vile kukabiliana na mnyama mkali, kushinda mchezo, kesi mahakamani na kufanikiwa masomoni.

Baadhi ya majigambo huwa marefu sana na huwa na masimulizi ndani yake hata ingawa mengi ni mafupi. Vivugo vingi hueleweka kwa urahisi kwa hadhira iliyolengwa kwa vile hujikita katika kueleza mambo ambayo yanafahamika kwa hadhira na wakati mwingine huwa wameshuhudia mambo hayo.

Watu ambao hawana uhusiano na vivugo husika hupata taabu sana kuvielewa hasa iwapo hawana ujuzi kuhusu historia ya mtunzi. Muundo wa kivugo hutegemea shabaha na jadi ya utunzi unaowakilishwa.

Kivugo chaweza kubainishwa kwa sifa kama:-

(i) Jina halisi na/au jina la sifa la mhusika
(ii) Sifa ya nasaba yake ya kuumeni
(iii) Sifa ya nasaba yake ya kuukeni
(iv) Maelezo kuhusu matendo matukufu aliyoyafanya
(v) Ahadi za kutenda makubwa zaidi kwa ajili ya mkubwa wake ambaye aweza kuwa mzazi, mtawala umma n.k,.
(vi) Kujikabidhi rasmi kwa mkubwa

Kiasili, kivugo hakikuandikwa kilitungwa papo kwa hapo. Hata hivyo siku hizi vivugo hutungwa kwa kuandikiwa na baadaye husomwa wakati wa sherehe kama za harusi.

## Tondozi

Hizi ni tungo za kusifu watu, wanyama au vitu. Pembezi pia huwa ni aina ya tondozi ambayo hukusudiwa watu wa aina fulani tu.

Complete Documents
Expanded Features

Ghani zenye kutondoza ni nyingi sana. Kitu chochote chaweza kusifiwa kwa mfano mti, nchi, mlima, mji, ng'ombe, gari na ndege.

Miongoni mwa vitu vinavyotondozwa sana ni mifugo hasa ng'ombe. Wanyama wa pori kama simba, na ndovu hutondozwa. Sifa zinazotolewa katika tondozi huwa ni za kistiari na hasa hukusudiwa binadamu. Tondozi ambazo zinamhusu binadamu moja kwa moja ndizo nyingi zaidi zikilinganishwa na tondozi kuhusu vitu vingine. Tondozi kuhusu binadamu hujikita katika kusifia wapenzi, adui, watani, waume, na watoto.

## Ghani – Masimulizi

Ghani za masimulizi ni zile ambazo hutambwa ili kusimulia hadithi, historia au tukio maalumu. Ghani hizi mara nyingi huambatanishwa na muziki wa ala. Mtunzi wa ghani huitwa yeli au manju na kwa kawaida huchukuliwa kama bingwa wa kupiga ala fulani ya muziki. Mifani ya ala zinazotumiwa katika ghani za masimulizi ni zeze, marumba, ngoma na njuga.

Vipengele ambavyo hubainisha ghani za masimulizi ni:-

(i) Ziwe tungo za kishairi
(ii) Zisimulie hadithi au tukio kwa kirefu ( iwe hadithi kamili)
(iii) Zitungwe papo kwa hapo wakati wa utongoaji.

Vipera vya ghani za masimulizi ni vingi. Mifano yao vipera hivi ni:-

(i) Rara
(ii) Ngano
(iii) Sifo
(iv) Tenzi

Expanded Features
Complete Documents

## Rara

Rara ni hadithi fupi nyepesi za kishairi zenye sifa za kusisimua. Rara nyingi huimbwa lakini zaweza kughaniwa zikiambatana na ala za muziki. Rara nyingi husimulia mambo ya kubuni hata ingawa kuna chache ambazo husimulia matukio ya kweli kama kutangazwa kwa uhuru, na mauaji. Rara nyingi huumbwa pamoja na ala za muziki kama zeze, marimba.

## Ngano

Hizi ni hadithi za kimapokeo zinazotumia wahusika kama wanyama, miti, watu n.k. Ngano hueleza au huonya kuhusu maisha. Kipera hiki hujumuisha fani kama:-

**(a) Istiari**

Hii ni hadithi ambayo maana yake ya wazi inawakilisha maana nyingine iliyofichika yaana hadithi nzima kama sitiari.

**(b) MBAZI**

Hizi ni hadithi fupi ambayo mafunzo yake hutolewa kama kielelezo wakati wa maongezi au kwa kumkanya mtu.

**( c) Kisa**

Hii ni hadithi fupi ya kufurahisha kuhusu tukio la kweli.

Ngano hizi huingia katika kundi la ghani masimulizi pindi au masimulizi yanapoambatanishwa na ala za muziki badala ya kusimuliwa tu. Juu ya sifa hizo ngano huwa na sifa zifuatazo:-

(i) Hueleza matukio katika mpangilio fulani mahususi.

(ii) Huwa na wahusika yaani watendaji au watendewa katika matukio yanayosimuliwa.

Expanded Features
Complete Documents

(iii) Hutumia lugha ya kimaelezo.

(iv) Utambaji na utoaji wake huweza kuambatana na vitendo au ishara.

(v) Huwa na maudhui ya kweli au ya kubuni na yenye funzo fulani kwa jamii.

## Sifo

Sifo huweza kuingia katika kundi la ghani masimulizi wakati zinapoingia masimulizi katika utondozi wake. Baadhi ya vivugo na pembezi badala ya kumsifu tu mhusika, husimulia kwa kirefu matukio yanayoambatana na sifa zake k.m. namna alivyoenda vitani, matatizo yaliyomkabili, mapambano aliyoyashiriki au kushuhudia na ushindi aliopata na baadaye kurejea. Mambo haya yanapoingia katika sifo, yanaifanya kuwa ghani masimulizi ( Mulokozi,`1989:13).

## Tendi

Tendi ndio utanzu mashuhuri zaidi katika kundi la ghani masimulizi. Kimapokeo tendi ni ushairi unaochukua muundo wa masimulizi. Utendi ni ushairi wa matendo ambao husimulia visa kwa kutumia mapigo ya kimuziki na pia ishara picha na tamathali aidha vina na visaidizi vinavyojenga milio ya aina aina.

Tendi huwa ni utungo mrefu wenye kusimulia matukio ya kishujaa yenye uzito wa kijamii au kitaifa. Matukio haya huweza kuwa ya kihistoria lakini tendi nyingi huchanganya historia na visakale au visasili.

| Tendi huwa na sifa zipi? |
|---|

Mulokozi (1989: 13) ametoa sifa zifuatazo:-

(i) Ni masimulizi

(ii) Hutolewa kishairi

(iii) Huhusu matukio ( kisa kimoja) muhumu ya kihistoria au kijamii

(iv) Hueleza habari za mashujaa au ushujaa

(v) Huwasilishwa kwa kughanwa au kuimbwa pamoja na ala ya muziki

(vi) Hutungwa papo kwa hapo ( hautungwi kabla na kuhifadhiwa kichwani kwanza ili baadaye utolewe kwa ghibu)

Complete Documents
Expanded Features

(vii) Hivyo hutwalia na muktadha wa utungaji na uwasilishaji wake kwa jamii

Katika fasihi simulizi, tendi hutofautiana na mashairi mengine hasa kwa sifa moja: urefu wake. Katika lugha zote tendi huwa ndefu. Tendi huwa na beti nyingi kuliko mashairi mengine. Kutokana na sifa hiyo tendi huwa na uwezo wa kueleza jambo kwa tafsili na kwa kinaganaga zaidi. Tendi husimulia habari kwa urefu. Katika fasihi simulizi tendi huwa ni hadithi za masimulizi kwa lugha ya mkato zaidi kuliko hadithi za kawaida au na nathari.

Sifa nyingine inayotafautisha tendi na mashairi ni ufupi wa mistari ya tendi. Mistari ya tendi nyingi ni mifupi mifupi na mara nyingi huwa haizidi mizani kumi na moja au mbili. Isitoshe mistari hiyo huwa haijagawanywa kwa vipande na kwa hivyo haina vituo.

Tendi husimulia habari kwa ufasaha na mvuto mkubwa hivi kwamba katika muda mfupi msikilizaji aweza kufahamu mambo mengi ya historia.

Tendi hutumiwa kwa lengo la kuasa, kwa kutumia fani hii. Wanajamii huonywa, huelimishwa na kupewa mawaidha kwa njia ya hekima. Mfano mzuri ni Utendi wa Mwana Kupona.

Tendi pia hutumiwa kumtaja mtu, wasifu wake au kueleza kitu kilivyo kwa jumla, kwa mfano, utenzi wa Liyongo. Siku hizi tendi hutumiwa kutoa wasifu wa watawala au viongozi. Mifano ni Wasifu wa Moi, na Wasifu wa Kenyatta .

Tendi ni sanaa inayoambatana na hali fulani ya kijamii hasa ile yenye vuguvugu ya mapambano na yenye asasi kama vile ufalme. Tendi ni mojawapo wa vipera ambavyo vimeathiriwa na mabadiliko ya maisha. Mazingira ya kuipalilia na kuiendeleza hayapo tena. Pengine njia muafaka ya kuhifadhi tendi ni kuzirekodi.

Baadhi ya tendi muhimu za Kiafrika ni Sundiata (Mali) Mwindo (Zaire), Liyongo (Kenya), Shaka ( Afrika ya Kusini) Luanda Magere,(Kenya) , na Wang'ombe(Kenya)

Expanded Features
Complete Documents

**Ngonjera**

Neno 'ngonjera' halijulikani lililotokana na nini ama lilitoka wapi. Mnyampala na wenzake ( UKUTA) Usanifu wa Kiswahili na ushairi Tanzania, ndio waliokuwa wa kwanza kulitumia mnamo mwaka wa 1964. Hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa neno hili lilitumiwa kabla ya hapo.

Katika ngonjera za Ukuta Mnyampala andakuwa ndiye mwanzilishi wa utanzu huu. Mnyapala ameungwa mkono na J.S.M Mwangomwango.

> Ukweli ni kwamba utanzu wa ngonjera ulikuwepo tangu zamani, una umri sawa na ushairi wa Kiswahili. Ukweli ni kwamba Mnyampala na wenzie waliuhuisha tu lakini hawakuaanzisha. Katika jamii za waswahili katika hadhara yo yote kulitokea manju/malenga/mngoi akasimama na kutoa wimbo wake ambao pengine ufuatishiwa wake na sauti maalum au pengine usemwe tu. Akimaliza mwenziwe naye ainuke naye atoe wimbo wake pengine uwe ni jawabu au fumbo la mshairi aliyetangulia. Mpango wa namna hii wapatikana kwa manju wa Kipemba. Mvita pia kulikuwa na "kufunga nyama". Malenga wawili watakuwa hawaonani wala pengine hawajuani watatengwa kwa pazia na watakuwa wamezungukwa na watu. Malenga wa kwanza 'atafunga nyama' yaani atafumba fumbo lake kwa shairi. Malenga wa pili atakuwa akiuliza akijibiwa kwa mashairi mpaka "amfungue nyama" yaani alifumbue hili fumbo na pengine atambue yule mfumbaji pia. Akishindwa basi atampa mji. Yule mfumbaji ndipo naye amfumbulie hili fumbo (Chiragdin, Utangulizi wa <u>Malenga wa Mvita</u>)

Kaskazini zaidi pia kuna mpango wa malenga wawili kujibizana na kati yao huwapo shaha wa malenga (mkuu wa manju). Mmoja akishindwa yule shaha "humvika guni yaani humtia ila/kwa kushindwa katika utungaji wa mashairi. Mpango wa namna hii unaendelea mpaka nyakati za sasa. Katika nchi ya Tanzania kuna mtindo wa ngonjera ambapo watu wawili husailiana na kujibizana kwa mashairi.

Complete Documents
Expanded Features

'Mkufuu na Mwanafuu' (Malenga wa Mvita, Nassir 1974:15) ni mfano wa ngonjera. Tukiafiki kauli ya mnyampala kuwa yeye ndiye aliyeanzisha ngonjera tutakuwa tukiafiki kuwa katika jamii za Waafrika hatukuwa na vitendawili kwani vitendawili ndivyo vilizaa ngonjera. Ngonjera kwa maana ya nyimbo za malumbano zimekuwepo tangu jadi. Malumbano haya yako katika jamii za Waluhya kwa njia ya mafumbo. Mashairi kama haya tunayo katika jamii ya Wakikuyu kwa jina la "Gichandi".

Katika sehemu zingine mashairi au nyimbo hizi ziliitwa diriji, lelemana au tari. Ngonjera hizi hutofautiana jinsi tamaduni zinavyotofautiana na toka kabila moja hadi kabila lengine lakini ni dhahiri kuwa fani hii ilikuwepo katika fasihi simulizi ya makabila mengi, Waswahili wakiwemo. Kile kinachobainika ni kuwa ngonjera ni drama ambayo hutumia ushairi.

- Huwa imejengwa juu ya majadiliano ama mabishano kuhusu suala fulani.
- Kutokana na mjadala mambo mbalimbali huwekwa wazi wazi ambao hufanya upande mmoja ushinde au ushindwe na ujiunge na ule ulioshinda. Ngonjera ikiingiza utendaji inakuwa ni drama.

Kumalizia twaweza kuona kuwa ngonjera ni kazi yo yote ya ushairi muradi iwe na wahusika wanaozungumza. Pia yaweza kuwa na vitendo vinavyoandamana au kusindikizana na maneno yanayosemwa. Urari wa ngonjera ni ule wa fani zingine za shairi.

## MAREJELEO

Biebuyck, D. na Mateene, - K (19690 The Mwindo Epic of the Banyanga University Press of California Press.

Finnegan, R. (1970) Oral Literature in Africa. Oxford University Press London.

Kijumwa, M. (1973) Utenzi wa Fumo Liyongo (mh) Abdilatif Abdalla. TUKI Dar es Salaam

Kunene, D. (1971) Heroic Poetry of the Basotho. Clarendon: Oxford University Press.

Mbele J. (1986) The Hero in the African Epic. Ph.D Thesis. Madison. Wisconsin Mpanje J. and White, L. (1983) Oral Poetry from Africa Longman. New York

Matteru, M.I. Balisdya (1987) 'Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi". Mulika na. 19 TUKI Dar es Salaam

Mulokozi M.M. (1989) "Tanzu za Fasihi Simulizi" Mulika Na 21. TUKI. Dar es Salaam

Complete Documents
Expanded Features

Nabhany S. na Abubakar A. ( Wahariri) (1972) Utendi wa Mwana Kupona. Utendi wa Ngamia na Paa. Heinemann Educational Books Ltd. Nairobi
Nassir, A. (1971) Malenga wa Mvita. Oxford University Press, Nairobi. Niane,
T. Sundiata: An Epic of Old mali (Tr. Pickett, G.D) London: Longman Okpewho
i. (1979) The Epic in Africa. Columbia University Press. New York.
________(1977) 'Does the Epic Exist in Africa? Some Formal Considerations". Research in African Literatures Vol. 8 pp. 171-200. Austin: University of Texas Press.

**MHADHARA WA KUMI NA MBILI**

**Tanzu za Fasihi Simulizi**

**Taarab**

Baada ya mhadhara huu utaweza kueleza

1. Maana ya taarab
2. Sifa za utanzu wa taarab kama fani ya fasihi simulizi
3. Dhima ya taarab katika jamii

## Maana ya Taarab

Maana ya Taarab ni ngoma ya kusisimua. Kamusi ya Kiswahili- Kiingereza ya F. Johnson inaeleza taarab kama muziki wa gambusi na zeze wenye kufuatana na mwimbaji. Neno 'taarab' ni la asili ya Kiarabu 'taarab' lenye maana ya furaha, kusherehekea karamu, kuimba na kupiga muziki. Mbali na neno lenyewe kuwa la kigeni, ngoma na muziki unaombatana na taarab ni ngeni. Kwa hivyo kwa mizani hizo mbili si ajabu kuona ni kwa nini wataalam wengi wamedai kuwa huu si utanzu wa fasihi simulizi ya Kiafrika. Wenye kuendelezea mtazamo huu wanadai kuwa kwa kila njia taarab ni muziki wa kigeni. Inasemekana kuwa taarab hujitenga na ngoma zingine hasa kwa zile ala zake zinazotumiwa na isitoshe kwa nidhamu ya ngoma yenyewe.

Ngoma ya taarab hutumia ala za muziki wa Kiarabu kama gambusi, (uddi) zeze ( fidla) , ganuni, nay, dumbak na nika ( Saleh 1980). Ala hizi ndizo halisi na za kuelezea nyimbo za taarab. Ala zingine hutumika kuongeza uzito wa sauti za juu ya zile za misingi. Ala hizi ni kama: gitaa, akodiani, ogani mandolini na tarumbeta.

Complete Documents
Expanded Features

Nidhamu ya taarab ni tofauti na ngoma nyingine. Taarab ni ngoma ya nyimbo na vinanda. Kinyume na ngoma zingine tuzijuazo katika ngoma ya taarab hakuna kucheza. Wapiga ngoma na vinanda hujikusanya mahali pamoja na wasikilizaji huwakabili au huwazingira. Ngoma ya Taarab inapoanza wasikilizaji huwa kimya kabisa na jukumu lao huwa ni kutega masikio tu kwa milio ya vinanda na sauti za maneno ya mtiribu wa ngoma yenyewe.

## Chanzo na Maendeleo ya Taarab

Taarab ni muziki wa kigeni ambao ulijikita katika ardhi ya Waswahili kati ya miaka 1870-1888 wakati wa utawala wa Sultan Barghash Bin Said. Inasemekana kuwa Sultan Barghash alikuwa mpenda muziki sana na alikuwa anaburudishwa kwa ngoma ya taarab. Inadaiwa kuwa Sultan huyu alikuwa mpenda muziki sana.

Mlama (1981:43) naye aeleza kuwa ngoma ya taarab iliingizwa nchini Tanzania kutoka Uarabuni na Uhindini. Aeleza kuwa Taarab ililetwa Afrika Mashariki kwanza katika Unguja mnamo miaka ya mwanzoni ya 1900. Sultan wa Unguja Seyyid Ali bin Hamid aliagiza wapigaji taarab kutoka Misri waje wamtumbuize. Wenyeji walivutiwa na muziki huo na katika miaka iliyofuata wakajifunza kuimba na kupiga vyombo vya muziki vya taarab ( Mlama 1981:43).

Kimaudhui nyimbo za Taarab zilikuwa za kumsifu na kumtukuza Sultan na suria yake. Wakati mwingine ngoma ya taarab ilisifu na kukomaza mapenzi ya jumuiya ya kifalme. Mara nyingine iliwaburudisha na kuwachekesha wakubwa; wachezaji wa taarab walikuwa wanaajiriwa katika nyumba za wafalme kuwastrehesha na vinanda vyao.

Baada ya Sultan Barghash kutoka mamlakani taarab ilipungua nguvu zake kwa sababu wafalme waliofuata walikuwa watawa na hapakuwa na utawala wa utulivu. ( Saleh 1980:35). Katika enzi hizo nyimbo za taarab ziliimbwa kwa kiarabu ambayo ndiyo iliyokuwa lugha ya mtawala. Kati ya mwaka wa 1905 hadi mwaka wa 1920 vikundi vya nje yaani ya kiraia vilianzishwa. Ngoma ya taarab ilipata umaarufu kati ya mwaka wa 1920 na 1950 wakati wa Siti Binti Saad (Wasifu wa Siti Binti Saad). Siku ziliposonga mbele taarab ilizidi kuingia katika mfumo wa amali ya jamii ya unguja. Mabadiliko ya

Complete Documents
Expanded Features

kwanza yalianza wakati watribu walipoanza kutumia mashairi ya Kiswahili. Haya mashairi yalikuwa yakiimbwa kwa mahadhi ya nyimbo za Kiarabu walizojifunza watribu kutokana na sahani za santuri. Vile vile mashairi mengine yaliimbwa kwa mahadhi ya kihindi lakini nidhamu ilibakia vile vile. Wakati wote wa ukoloni taarab ilisaidia kupalilia tabaka la watawala. Haikuwa ikijishughulisha na mapambano ya wananchi na migogoro yao na uovu wa kitabaka na kibepari. Nyimbo zake aghalabu zilikuwa za mapenzi na kusifu ubwana na ubibiye.

Wakati huu taarabu iliwavutia Waswahili na ikaanza kuchanganya uimbaji na mitindo ya Waswahili. Ilianza kujitenga na uarabu na mahadhi yake yakawa ya Waswahili. Maudhui ya taarab ambayo hapo awali yalijikita katika mapenzi kati ya wake na waume yakaanza kubadilika. Waarabu walianza kuchota maudhui yao kutokana na matashi shida na raha za Waswahili katika mazingira yao. Washiriki wa taarab wakawa wengi na ikaenea katika sehemu kubwa ya visiwa na kufika Mrima. Ni wakati huu ambapo nyimbo za Kiswahili zilipoanza kusikika katika sahani za santuri.

Marehemu Siti Binti Saad ndiye aliyekuwa mtribu wa kwanza kutolesha sahani za santuri zenye nyimbo za taarab. Hadi hivi leo kuna watribu wanaondelea kutoa sahani hizo.

## Je Taarabu ni fasihi simulizi?

Kama ilivyo katika fani za Fasihi simulizi, nyimbo za taarab hurithiwa aghalabu kwa kufundishana kwa mdomo. Nyimbo nyingi hasa za miaka thelathini na arobaini nyuma hazijulikana watunzi wake na si ajabu ikiwa kuna mabadiliko ya maneno ndani ya mashairi yake ambayo yalizuka kwa ajili ya watu kupokezana na mdomo. Inasemekana kuwa hapo zamani nyimbo za taarab zilikuwa ni za kubuni papo hapo kwenye hafla. Mwimbaji mashairi hupandwa na jazba ya muziki akatoa wimbo uliokamilika kishairi kwa kuusanifu wakati ule ule.

Complete Documents
Expanded Features

Hivi sasa kuna watungaji wa nyimbo za taarab, watungaji wa muziki. Wapiga vinanda vya taarab hujifunza kwa kusikiliza. Waimbaji vile vile huwa wanafuata mwendo wa kawaida ya taarab. Wanajifunza nyimbo kwa kusikiliza wakati zinapoimbwa na kuhifadhi sauti na maneno yake pamoja.

## Maudhui na Sanaa ya Taarab

Tangu nyimbo za taarab zianze kutumia mashairi ya kiswahili hadi leo kumechimbuka nyimbo nyingi sana kutokana na hisi za watribu. Baadhi ya nyimbo zimedumu kadri ya miaka kumi na tano hadi ishirini.

Maudhui ya nyimbo za taarab yaweza kugawanywa katika matapo yafuatayo, nyimbo za mapenzi, uasherati na ugoni.

Katika tapo hili nyimbo nyingi huwa ni zile zinazoashiria mapenzi ya mke na mme. Katika miaka kabla ya uhuru taarab ilijishughulisha zaidi na nyimbo za mapenzi. Kuna mapenzi ya aina nyingi ambayo yanazungumziwa katika nyimbo za taarab. Kuna mapenzi kati ya mke na mume, mapenzi ya wazee, mapenzi ya jamii, mapenzi ya kindugu, mwisho kuna mapenzi ya nchi. Nyimbo za taarab zimetumiwa kama chombo cha siasa. Katika nyimbo hizi maudhui ya kisiasa huwa yanasisitizwa kuliko maudhui mengine.

## Muundo wa Taarab

Nyimbo za taarab zinatungwa kwa mitindo kadha. Kuna zile ambazo zina mistari mitatu, mine, mitano n.k. Mizani ya mistari ya beti za taarab huwa kumi na mbili ama kumi na sita.

Nyimbo za taarab za beti zenye mistari mitatu huwa hazina vituo na kwa hivyo huwa haziitikiwi na zikiitikiwa kiitikio huwa ni kurejelewa kwa mstari wa mwisho katika kila ubeti. Katika nyimbo zenye beti za mistari mine mwimbaji huimba mistari mitatu na waitikiaji hudakia mstari wa nne ambao aghalabu huwa ni kituo cha aina moja katika beti zote. Vile vile katika nyimbo za beti zenye mistari mitano kiitikio chake huwa mistari

Complete Documents Expanded Features

miwili ya mwisho ya kila ubeti na kituo hicho huwa hakibadiliki. Nyimbo nyingi za taarab huwa na beti tatu au nne na wimbo huchukua muda wa dakika nane hadi kumi.

Kwa upande wa lugha nyimbo za taarab hutumia kiswahili cha hali ya juu. Kama inavyobainika katika muundo wa taarab, kuna matumizi ya mtindo wa lugha ya kishairi hasa kwa vile kuna uzingativu wa kaida za ushairi wa kiswahili. Urari wa vina na mizani na arudhi zingine za ushairi wa kiswahili ni baadhi ya sifa za taarab. Matumizi ya lugha ya kishairi husababisha matumizi ya lugha ya kiishara na mafumbo. Hali hii hufanya nyimbo za taarab kuw ngumu kueleweka. Mfano

Nakuonya tahadhari punguza kulivaidia
Sega langu la asali najua walinyatia
Utakufika muhali vya watu kuvivamia
Sega langu la asali macho walikondolea
Walinzi wake wakali mashujaa walotimia
Hata tembe mwenye hali hatathubutu kusogea
Walinzi wake ambao wakali wasochelea
Bunduki na marisasi wameshinda kufyatua
Mikuki na zao ngao ni bure wamekimbia
Seuze wa mwanakao jima imachokipata
Umepigwa mpumbao mate unakimezea
Wameshindwa wenye vyao seuze wewe papia

Hebu wacha kujigamba huna unachokipata
Hawi tembo na simba umewashinda ukuta
(Wimbo ulioimbwa na Seif Salim na kunukuliwa na Mlama 1981:43)

Hata ingawa ni muhimu kwa watunzi wa nyimbo za taarab kuzingatia arudhi za utunzi, maudhui ndiyo huzingatiwa zaidi. Shairi au wimbo wa taarab huchukuliwa kuwa hafifu iwapo maudhui yake hayakukamilika hasa iwapo alipotoka katika juhudi za kufuata

Complete Documents
Expanded Features

arudhi kwa upande wa vina, mizani, na vituo. Nyimbo nyingi za taarab huwa na vina vya mwisho tu na nyingine huwa na vina ambavyo hubadilika kwa kila ubeti.

Mwimbaji akiimba vizuri aweza kuwavuta wasikilizaji kiasi cha kuwafanya waamke kwenda kumtunza. Hivyo basi katika taarab kama ilivyo katika fani zingine za fasihi simulizi fanani hupata uhakiki wake papo hapo. Isitoshe akimaliza kuimba anapigiwa makofi na hoi hoi za wasikilizaji zaweza kumfanya aimbe wimbo wake tena. Basi si ajabu kuwa taarab ni ngoma inayoshirikisha watu wengi sana na inapendwa sana na watu wa mwambao. Hata hivyo mizizi ya athari za ukoloni ni mrefu sana kiasi kuwa mashabiki wa ngoma za taarab hupendezwa sana na taarab zenye mahadhi ya Kiarabu.

Katika utendaji wa ngoma hii mafanani huwa hawatendi kitu mbali na mwimbaji kusimama na kuimba. Wapiga ala hucharaza ala nao waitikiaji hungoja mpaka ubeti uishe ili waitikie. Hadhira huwa haina nafasi ya kushiriki na fanani katika kutenda ngoma yenyewe. Nyimbo za taarab kinyume na fani zingine za fasihi simulizi hazitungwi na kuwasilishwa papo hapo, mtunzi, mwimbaji. Wapiga ala na pia waitikiaji hufanya mazoezi kabla ya kuwasilisha utunzi wao kwa hadhira.

Taarabu hupigwa harusini, michezoni na vilabuni mwa pombe. Katika starehe za mtu binafsi au katika dhifa maalum. Nyimbo za taarab hazina matukio; zaweza kuimbwa nje au ndani, penye watu ama pasipo watu. Kile kinachosisitizwa ni kuwa taarab haina mazingira maalum. Ngoma ya taarab yaweza kupigwa popote na watribu huweza kuvaa vazi lo lo lote.

Katika kutamba taarab kuna mipaka kwa vile mtiribu hawezi kuongeza kitu cho chote ambacho hakijafanyiwa mazoezi hapo awali. Madoido ya mwimbaji hayana nafasi wakati taarab inapoendelea. Mtribu hulazimika kujifunga na mambo yale tu ambayo washiriki wote waliyafanyia mazoezi kwayo; uhuru wake huwa katika matumizi yake ya sauti apendavyo kwa maghani na pia kuweka shada, misokoto na mikato ya maneno katika mapigo ya mahadhi ya nyimbo.

Complete Documents
Expanded Features

Washiriki katika nyimbo za taarab huwa watu wa tabaka la kati na hadhira huwa watu wa tabaka la juu au la kati tu. Katika fani nyingi za fasihi simulizi hakuna mategemezi ya maneno pekeee bali huambatanishwa na vifaa vingine kama miguno ya sauti n.k. Vile vile katika taarab vyombo vingi vya kimuziki hutumiwa kuchangia uwasilishaji. Kama tulivyodokeza hapo awali, vyombo vingi vinavyotumika katika taarab ni za asili ya kigeni. Mifano ya vyombo hivyo ni kama fidla, udi, dumbak, firimbi au nai n.k.

Muziki katika taarab kama katika kazi yo yote ya fasihi simulizi hutumiwa kwa lengo la kuiteka na kuinyanyua hadhira katika utamu, ladha na anasa za tafrija pamoja na kuzikoleza hisi kwa maneno yanayoimbwa.

Waitikiaji ni watu muhimu katika taarab kwa vile nyimbo nyingi za taarab huwa na viitikio. Waitikiaji hudaka kiitikio kila baada ya mwimbaji kumalizia kuimba ubeti mmoja wa wimbo. Dhima kubwa ya waitikiaji ni kupumzisha mwimbaji. Pamoja na hayo sauti za waitikiaji huleta mabadiliko kwa watazamaji au wasikilizaji ili wasichoshwe na sauti moja ya mwimbaji.

Aghalabu waitikiaji huwa ni wake na waume lakini kuna uwezekano wa kuwa na waume tu au wake pekee. Hata hivyo baadhi ya nyimbo huwa hazina viitikio na kwa hivyo huwa hazina waitikiaji.

Taarab hata ingawa ni ngoma iliyoingizwa katika jumla ya ngoma za Waswahili, imechukua muundo tofauti na ule wake wa asili. Hivi leo ngoma ya taarab hulingana na maisha ya Waswahili. Umbo la ngoma hii sasa huchukua sura tofauti na iliyokuwa mwanzo. Taarabu imeathiriwa na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Lugha yake pia inaenda sambamba na athari ya muziki wa Kiarabu huenda ikapotea na taarab ibainike kama aina ya pekee ya muziki wa Kiswahili.

## Dhima ya Taarab

Complete Documents Expanded Features

Taarab ya sasa ni tofauti na ile ya wakati wa ukoloni. Tofauti kubwa imejikita katika maudhui na nyimbo zake. Isitoshe taarab imekuwa maarufu zaidi kuliko hapo zamani. Pamoja na hayo maendeleo yake ni makubwa hasa kwa upande wa utungaji wa maneno na muziki wa nyimbo bila kutegemea ule muziki wa nyimbo za kiarabu. Pamoja na hayo kumezuka vipengele vingine vya mazingira yanayotumia taarab. Mifano ni sherehe za kiserikali. Hii ni dhihirisho kuwa kuna muumano mkubwa kati ya taarab na maisha ya jamii. Kwa sababu hii siku hizi taarab inashughulikiwa na serikali. Zamani nyimbo za taarab zilitumiwa kuendeleza maslahi ya wakoloni, ya ubepari, ubwanyenye, ukabaila, utajiri na ubinafsi. Nyimbo hizi hazikuwa na faida yo yote kwa wananchi ila hasara ya kutawaliwa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kama zilivyo tanzu zingine za fasihi simulizi ambazo dhima yake ni kufunza na kuendeleza amali za jamii pamoja na falsafa yake, basi na taarab huwa na dhima hiyo hiyo. Leo hii taarabu ina dhima kubwa katika kuongoza jamii. Taarab katika jamii yaweza kuwa chombo kikubwa kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Zama hizo taarab ilitumiwa kupalilia utawala wa kidhalimu. Hata hivyo yaweza kuwa na lengo la

| |
|---|
| Toa ushahidi unaodhihirisha kuwa taarabu ni utanzu wa fasihi simulizi |

kuendeleza amali na falsafa ya jamii. Taarab pia huwa na wananchi kuendeleza amali na falsafa ya jamii. Taarab pia huwa na dhima ya kuburudisha wananchi baada ya saa za kazi. Isitoshe na taarab hutumika katika sherehe zote za jamii kutoka za watu binafsi hadi shughuli za serikali.

## MAREJEO

Khatib, M.S (1981) "Taarab ni Fasihi Simulizi 7" Makala ya Semina ya Fasihi Simulizi. Tuki Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam

Mlama, P.O 91981) "Sanaa za Maonyesho. Taarab na sanaa zinazoweza kusaidia kuimarisha Lugha ya Kiswahili" Lugha Yetu Namba 38. Jarida la BAKITA

Complete Documents
Expanded Features

Robert, Shabaan (19) Wasifu wa Siti Binti Saad

Saleh, S.S (1980) “Nyimbo za Taarab Unguja.” Lugha Yetu Namba 37 Jarida la BAKITA.

## MHADHARA WA KUMI NA TATU

### Tanzu za Fasihi Simulizi

### Sanaa za Maonyesho

Baada ya mhadhara huu utaweza kueleza:

1. Maana ya sanaa ya maonyesho kama utanzu wa fasihi simulizi
2. Sifa zake
3. Dhima yake katika Jamii

Kuna istilahi nyingi ambazo zimetumiwa kwa dhana ya maonyesho. Baadhi ya istilahi hizi ni:

a) Michezo ya kuigiza
b) Rando
c) Tamthilia
d) Vichekesho
e) Sanaa ya utendaji

Sanaa ya maonyesho ni moja kati ya tanzu za fasihi simulizi ambayo ina umbo la tamthilia.

Je tamthilia ni nini?

Tamthilia huwa ni tungo wenye kuigizwa mbele ya hadhira. Mara nyingi michezo ya kuigizwa huwa ni mfululizo wa visa vinavyohusu binadamu na tabia zake kama uoga, uzembe, ujasiri au mambo ya ajabu na ya kawaida.

Kila mchezo huwa na wahusika au washiriki. Mchezo waweza kuelezwa kimya au kwa kusimulia mambo fulani. Mambo yanayosimuliwa huwa yanahusiana na maisha ya

Complete Documents
Expanded Features

binanadamu na lengo lake huwa ni kueleza fikira fulani, kuburudisha, kuendeleza utamaduni au kuelimisha watazamaji.

**CHANZO CHA SANAA YA UTENDAJI**

Kuna nadharia nyingi kuhusu chimbuko la sanaa ya utendaji. Nadharia moja ni ile inayoitwa nadharia maarufu, (Mmbaga 1981: 136). Nadharia hii inadai kuwa sanaa ya maonyesho imeibuka kutokana

SANAA YA MAONYESHO

- Istilahi zinazotumika kwa dhana ya sanaa ya maonyesho
  - Michezo ya kwigiza
  - Tamthilia
  - Rado
  - Vichekesho
  - Sanaa ya utendaji
  - Sanaa ya maonyesho ni moja ya tanzu za fasihi simulizi ambazo huwa na umbo la tamthilia

Tamthilia ni nini

- Utungo wenye kuigizwa mbele ya hadhura
- Mara nyingi michezo ya kuigizwa huwa ni mfululizo wa visa vinavyohusu binadamu na tabia zake kama uoga, uzembe, ujasiri au mambo ya ajabu na ya kawaida
- Kila mchezo huwa na wahusika au washiriki
- Mchezo waweza kuelezwa kimya kimya au kwa kusimulia mambo fulani ambayo yahusiana na maisha ya binadamu kwa lengo la kueleza fikira fulani, kuburudisha, kuendeleza utamaduni au kuelimisha watazamaji

**Chanzo na Mifano ya Sanaa ya Utendaji**

Complete Documents
Expanded Features

Kuna nadharia nyingi kuhusu chimbiko la sanaa ya utendaji. Nadharia moja ni ile inayoitwa nadharia maarufu (Mmbaga 1981:136) Nadharia hii inadai kuwa sanaa ya maonyesho imeibuka kutokana na vitendo vya dhati kama ibada, jando, matambiko n.k.

Nadharia ya pili ni ile inayodai kuwa sanaa ya maonyesho imeibuka kutokana na fasihi simulizi hasa utambuzi wa hadithi na utongoaji wa mashairi.

Miongoni mwa wa wanasanaa ambao wamesshghulikia sanaa ya maonyesho ni Penina Mlama (1981:150-171). Dhana nne kulingana na Mlama zinapaswa kuzingatiwa katika sanaa yoyote ya maonyesho: hizi ni dhana ya inayotendeka, mtendaji, uwanja wa kutendea na watazamaji. Matambiko kama kupeana mtoto jina, kuingia jandoni na unyagoni, kuoa na mazishi ni mifano ya sanaa za maonyesho zinazopatikana katika jamii za Kiafrika. Michezo ya utotoni chambilecho Saifu Kiango (1981: 171-173) pia ni mifano mizuri ya sanaa za maonyesho. Mara nyingi watoto huigiza nafasi ya baba na mama bila kuingia katika nyadhfa hizo katika udhati wa maisha. Katika zama hizi watoto wana weza kuigiza nafasi ya mwalimu, mhubiri na hata tabibu. Ukweli ni kwamba karibu tanzu zote za fasihi simulizi tulizozungumzia kama methali, vitendawili, nyimbo, sifo, ngano na hurafa zinashirikisha uigizaji wa aina fulani. Kwa hivyo, zinaweza kuingia katika kitengo cha sanaa ya utendaji.

Marejeleo

Kiango, S.D. “Maendeleo ya Mchezo wa Kuigiza”, Urithi wa Utamaduni Wetu. Wahariri, C.K Omari & M. Mvungi. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House, 1980.

Mlama, Penina. “ Maendeleo ya Sanaa za Maonyesho katika Jamii za Asili”, Urithi wa Utamaduni Wetu. Wahariri, C.K. Omari & M. Mvungi. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House, 1980.

**Heri Njema**